**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA NANE**

**Kikao cha Sita - Tarehe 20 Juni, 2007**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Anna S. Makinda) Alisoma Dua*

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 48

**Vigezo vya Kubaini Mahitaji ya Hospitali za Wilaya**

**MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA** aliuliza:-

(a) Je, Serikali imejiwekea vigezo gani vya kubaini mahitaji ya msingi ya Hospitali ya Wilaya hususan aina na idadi ya majengo, vitanda, vifaa mbalimbali, aina na idadi ya wataalam?

(b) Kwa kupitia vigezo hivyo. Je, hali ya Hospitali ya Lushoto ikoje, na kuna mpango gani wa kurekebisha kasoro zilizopo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Balozi Abdi Hassan Mshangama, Mbunge wa Lushoto lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali za Wilaya zinajengwa kwa kuzingatia michoro rasmi (*Standard Plans*) iliyoidhinishwa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Vigezo vya Hospitali ya Wilaya ni kama ifuatavyo:-

**1. Majengo:**

(i) Jengo la Utawala (*Administration Block*);

(ii) Jengo la wagonjwa wa nje *(OPD);*
(iii) Kliniki ya kina mama *(MCH Clinic);*
(iv) Chumba cha Upasuaji (*Theatre*);
(v) Maabara;
(vi) Chumba cha *X-ray;*
(vii) Chumba cha Ufuaji *(Laundry);*
(viii) Chumba cha Huduma za UKIMWI (*Care and Treatment Centre);*
(ix) Chumba cha Dawa (*Pharmacy*);
(x) Jengo la matengenezo ya vifaa vya hospitali (*Health Care Technical Service);* na
(xi) Wodi saba kwa mchanganuo ufuatao:-
- Wodi ya watoto;
- Wodi ya wanawake magonjwa ya kawaida;
- Wodi ya wazazi (*Anti-natal, Labour na Post natal);* na
- Wodi ya wanaume upasuaji.

**2. Idadi ya Watumishi:**

Watumishi wa kada mbalimbali wapatao 154 kama ifuatavyo:-

Madaktari *(MO) 2,* Madaktari Wasaidizi *(AMO) 10* - wakiwemo Wataalam wa Usingizi *(AMO Anaesthesia*) – 2, Macho *(AMO Ophthalmology* – 1, Akili *(AMO Psychiatric* – 1, na Mionzi *(AMO Radiology*) – 1, Wengine ni Maafisa Wauguzi – 10, Wauguzi – 39, Wafamasia – 3, Watumishi wa Maabara – 5, Afya ya Mazingira – 3, Mafundi Sanifu Mionzi – 3, Wazoeza Viungo – 2, Maafisa Tabibu – 13, Wahudumu wa Afya – 25, Famasia – 3, Huduma za Meno (*Dental*) – 4, na watumishi wengine wa Utawala 32.

**3. Idadi ya Vitanda:** Idadi ya vitanda vinavyohitajika katika Hospitali ya Wilaya ni kuanzia 101 – 175 kutegemea na idadi ya watu *(population*) katika Wilaya husika.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Wilaya ya Lushoto kwa kukidhi baadhi ya vigezo vilivyotajwa hapo juu imekuwa ikipata vifaa kutumia mfumo uliowekwa na Wizara ya Afya ambapo fedha kwa ajili ya manunuzi ya vifaa hupelekwa moja kwa moja *Medical Stores Department (MSD).* Vyanzo vingine vya fedha vinavyotumika kununulia vifaa ni fedha za Mfuko wa Afya wa Jamii *(CHF)*, fedha za kuchangia gharama na mchango toka mapato ya Halmashauri.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo linaloikabili Hospitali ya Wilaya ya Lushoto kwa sasa ni uchakavu wa majengo na upungufu wa wafanyakazi hasa Madaktari na Wauguzi. Kuhusu uboreshaji wa majengo, Serikali kupitia Mkakati wake wa kukarabati vituo vya Afya na Hospitali, Hospitali zote za Wilaya katika Mkoa wa Tanga ikiwemo Hospitali ya Wilaya ya Lushoto zitakarabatiwa katika Mpango huo. Katika Hospitali ya Wilaya ya Lushoto, mpango huu umelenga kujenga jengo jipya kwa ajili ya wagonjwa wa nje *(OPD)* na pia kuboresha miundo mbinu ya maji katika hospitali hiyo pamoja na kujenga jengo jipya la kuhifadhia maiti. Kwa upande wa watumishi, Serikali imeweka utaratibu wa kuwapanga watumishi wa afya wanaotoka vyuoni moja kwa moja bila

kufanya usaili, utaratibu ambao ulianza mwaka wa fedha 2005/2006. Serikali pia imekuwa na mkakati wa kuwaendeleza watumishi walio na sifa kidogo ili waweze kuwa na sifa zinazostahili na pia waweze kujaza nafasi wazi ambazo kwa sasa hazina wataalam. Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto imekuwa ikitenga fedha katika Bajeti zake kwa lengo la kuwaendeleza watumishi wake.

**MHE. ABDI H. MSHANGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza. Wilaya ya Lushoto ni Wilaya kubwa yenye watu wengi. Hospitali hii ya Wilaya ya Lushoto haina gari la kubebea wagonjwa na uwezo wa Halmashauri katika eneo hilo ni mdogo. Je, Serikali inaweza kutusaidia Wilaya ya Lushoto kupata gari la kubebea wagonjwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Hospitali za Wilaya Serikali inafanya kila jitihada kuhakikisha kwamba Hospitali ya Wilaya inapata gari la kubebea wagonjwa. Lakini tatizo letu ni ufinyu wa Bajeti. Kama mlivyoona kwenye Bajeti iliyopita ni magari ya wagonjwa 22 tu ambayo yalinunuliwa kwa mwaka 2005/2006. Kwa mwaka 2006/2007 ni magari 35 tu ambayo yamegawiwa. Kwa hiyo, kulingana na upungufu huo baadhi ya Wilaya inabidi zingoje mpaka hapo hali ya kifedha itakapokuwa nzuri. Ni nia ya Serikali kukidhi mahitaji hasa kwa kila Wilaya.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Hospitali za Wilaya zilijengwa kwenye maeneo ambayo wakati ule idadi ya watu ilikuwa ndogo na hakukuwa na uwezekano wa kuzipanua. Je, Serikali itakubaliana na mimi kwamba kuna haja sasa ya kupitia Sera ya Afya na kuangalia utaratibu wa kujenga Hospitali kubwa sio lazima za Wilaya kwa kuzingatia uwingi wa watu. Kwa mfano jimbo la Bumbuli lina watu 150,000, jimbo la Mlalo lina watu 150,000 na Lushoto karibu idadi hiyo hiyo zote zinategemea hospitali moja?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba majengo ya Hospitali mengine yalipojengwa sasa hivi yameonekana ni madogo na kwamba kuna umuhimu wa kubadilisha aina ya majengo ambayo tunajenga. Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii sasa hivi inalifanyia kazi jambo hilo ili kuweza kuona kwamba ni jinsi gani ramani za majengo itakuwa kwa kulingana kwanza na mahali kama ukubwa wa mahali penyewe wa kiwanja, ukubwa wa hospitali na idadi ya watu.

Kwa hiyo, Wizara inalifanyia kazi na kuona kwamba zile ramani zilizotumika kama za zamani baadaye tutawapatia ramani nyingine nzuri.

Na. 49

**Madiwani Kama Nguzo Muhimu ya Uwakilishi**

**MHE. MARTHA M. MLATA (k.n.y. MHE. JUMA H. KILLIMBAH)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Madiwani ni nguzo muhimu ya uwakilishi wa wananchi katika ngazi ya Serikali za Mitaa, na wao ndio wawakilishi wa wananchi kwa karibu sana, wahamasishaji wakubwa wa shughuli mbalimbali za maendeleo, wasimamizi wa Bajeti za Halmashauri husika na pia ndio waidhinishaji wa matumizi na mapato ya Halmashauri; na kwa kuwa, sasa Madiwani wameondolewa kuwa Wajumbe wa kupanga zabuni za ununuzi katika Halmashauri:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba, imewanyima wananchi haki ya usimamizi wa kodi zao kwa maana ya "*No taxation without representation"?*

(b) Je, Serikali haioni kuwa, inasababisha rushwa kwa kukabidhi mamlaka kwa Wakuu wa Idara wa Halmashauri, na matokeo yake ni kuwa, utekelezaji wa miradi unakuwa katika viwango hafifu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juma Hassan Kilimbah, Mbunge wa Iramba Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa Serikali imewaondoa Waheshimiwa Madiwani katika Bodi za Zabuni za Halmashauri. Kuondolewa kwa Madiwani kumefanywa chini ya Kanuni za Manunuzi za Serikali za Mitaa Tangazo la Serikali Namba 49 la tarehe 21 Machi, 2003.

Kwa mujibu wa kanuni hizo, Bodi za Zabuni za Halmashauri huundwa na Watendaji Wataalam wa Halmashauri. Aidha, kifungu cha 28(3) cha Sheria za Manunuzi ya Umma Namba 21 ya mwaka 2004 kinaeleza kwamba Mamlaka za Serikali za Mitaa zitaunda Bodi za Tenda chini ya Afisa Mhasibu kufuatana na Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 1982.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni ya kuwaondoa Waheshimiwa Madiwani katika Bodi za Zabuni za Halmashauri ni kuwapa nafasi zaidi ya kuhoji na kusimamia utendaji wa Bodi hizo kupitia Kamati ya Fedha za Halmashauri na Mabaraza ya Halmashauri ambayo hupata taarifa ya Bodi za Zabuni. Muundo wa sasa wa Bodi za zabuni za Halmashauri hauwanyimi wananchi haki ya usimamizi wa kodi zao, bali unaimarisha zaidi haki na madaraka ya Madiwani kama wawakilishi wa wananchi kuhoji na kusimamia matumizi ya fedha za walipa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi za Zabuni ni chombo kinachotekeleza maamuzi ya Baraza la Madiwani ambayo yameidhinishwa katika mpango na Bajeti husika. Utaratibu uliomo katika kanuni umezingatia "*checks and balance*" tangu zabuni

inapotangazwa, inapofanyiwa uchambuzi wa kitaalam, inapojadiliwa na Bodi na uamuzi kutolewa hadi kufunga mkataba Mwenyekiti wa Halmashauri husika ndiye anayesaini mkataba wote wa tenda zote za Halmashauri. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba kama Waheshimiwa Madiwani watatimiza wajibu wao kikamilifu, Usimamizi wa mali za Halmashauri na uwakilishi wa wananchi vitakuwa vimetekelezwa.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, muundo na utaratibu huu hausababishi kuwepo kwa rushwa kwa vile Kanuni za Manunuzi za Serikali za Mitaa pamoja na Sheria ya Manunuzi ya Umma Namba 21 ya 2004 zimeweka misingi imara ya uwazi, uwajibikaji na uzingatiaji wa sheria.

Watendaji wanapaswa kuhakikisha kwamba utoaji wa zabuni unafuata sheria, kanuni na taratibu zilizopo. Suala la watendaji kudai rushwa halistahili kuwepo iwapo kila Diwani atatimiza wajibu wake wa kuwasimamia na pale itakapobainika kwamba kuna vitendo vya rushwa au upendeleo sheria zilizopo zitachukua mkondo wake dhidi ya wahusika. Kwa mantiki hiyo, Madiwani wana nafasi nzuri zaidi ya kuhoji kwa maana ya kuleta "*checks and balance"* wakiwa nje ya Bodi kwa sababu wao ndio wanaotoa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge katika Halmashauri zao wazisimamie kikamilifu Bodi za Zabuni za Halmashauri ili zitende kazi kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia masuala ya Manunuzi ya Umma.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ningependa kuuliza swali moja la nyongeza.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri haoni kwamba kuwanyima Madiwani kuingia katika Bodi za Tenda ni kuwanyima haki wananchi kwa uwakilishi wao sahihi ndani ya Bodi za Zabuni na kama anavyojua kwamba heri kuziba ufa kuliko kujenga ukuta kwa kusubiri Madiwani waje wahoji wakati mambo yakiwa tayari yameshaharibika?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kusema kweli wananchi wanawakilishwa ipasavyo katika Bodi za Tenda za Halmashauri. Kama nilivyoeleza huko mwanzoni kwamba tenda yoyote ikishatangazwa *"process*" zote zikishamalizika Mwenyekiti wa Halmashauri ndiye anayesaini ile mikataba. Yeye ni mwakilishi wa wananchi na ni mwakilishi wa Madiwani wote.

Pili, tenda hiyo ikishamalizika *procedure* zote zinaripotiwa kwenye Kikao cha Fedha cha Halmashauri. Kama tunavyofahamu kwamba vikao vya Fedha na Mipango vinakaa kila mwezi. Kwa hiyo, Mkurugenzi Mtendaji anatakiwa kuripoti kwamba tenda fulani imetangazwa na imefikia katika *stage* gani. Pale wananchi wanawakilishwa kwa sababu Madiwani wana uhuru wa kuhoji kuanzia pale na baadaye inapelekwa kwenye Baraza la Madiwani. Pale pia wanaweza wakaingilia uhalali na kutokuwa halali kwa tenda iliyotangazwa.

**MHE. JUMA S. NKUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kuniona.

Kwa kuwa nafuatilia majibu mazuri ya Naibu Waziri na anatuelekeza kwamba Bodi ikishamaliza kazi yake inapeleka tena kwa Mwenyekiti wa Halmashauri au Meya ambaye hakuwepo kwenye Bodi na anasaini vitu ambavyo havifahamu. Je, ni utaratibu mzuri huu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu uliopo ni utaratibu mzuri kabisa. Kwa sababu wakati wa kusaini anatakiwa Mwenyekiti, Mwanasheria wa Halmashauri pamoja na Mkurugenzi wanasaini wote kwa pamoja. Wakati ule Mwenyekiti ana uhuru wa kuhoji chochote kile ambacho anaona kimekwenda kinyume na sheria huo ndio uwakilishi wa wananchi.

**WAZIRI MKUU**: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Naibu Waziri kwa jibu lake zuri sana. Lakini nataka kusisitiza kuwa utaratibu huo ni mzuri na hatimaye tulipata uzoefu hapa Dodoma kilichotusaidia tukajua kwamba wizi umetokea ni siku ile Mwenyekiti amepokea zile tenda ili ayasaini akagundua kuna wizi zikachukuliwa hatua na watu wakasimamishwa kazi. Kwa hiyo, utaratibu huu ni mzuri unafanya kazi vizuri tuendelee kuutumia. *(Makofi)*

Na. 50

**Uuzaji wa Hisa za Kampuni ya Twiga Cement**

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali iliuza hisa zake za Kampuni ya *Twiga Cement* kwa wananchi; na kwa kuwa, walionunua hisa hizo baada ya miezi miwili walirejeshewa asilimia sabini (70%) ya fedha walizonunulia bila kuelezwa sababu ya kufanya hivyo kwa maandishi:-

(a) Je, ni sababu gani zilizosababisha kurudisha asilimia 70 ya fedha walizonunulia hisa?

(b) Je, *DSE* iko tayari kurudisha fedha hizo pamoja na riba?

(c) Je, Serikali haioni kuwa, kwa kufanya hivyo *DSE* imekiuka mkataba walioingia na watu walionunua hisa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO)** alijibu:-

Kwa niaba ya Mheshimiwa waziri wa Fedha napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mbunge wa Pangani, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia waraka matarajio wa mauzo *(Prospectus*) ilitangaza kuuza hisa 19,143,884 zilizokuwa na thamani ya shilingi 5,742,399,445/= katika Kampuni ya *Tanga Cement.* Maombi yaliyopokelewa kutoka kwa wananchi yakawa ni ya kununua hisa 80,703,051 zenye thamani ya shilingi 24,211,215,300/=. Kwa matokeo haya, Serikali ililazimika kurejesha kwa wananchi fedha za ziada zilizokusanywa na *DSE* na hisa 61,559,167 zenye thamani ya shilingi 18,467,750,100/= bila ya riba kwa sababu Serikali haikuwekeza kokote fedha hizo. Makubaliano katika Waraka maalum wa Mauzo *(Prospectus)* yalitajwa wazi kwamba, endapo maombi yatazidi hisa zinazouzwa, wananchi watarejeshewa fedha zao za ziada. Kwa maelezo haya Mkataba ulikuwa Waraka Matarajio wa Mauzo "*Prospectus"* na Mkataba huo haukuvunjwa.

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Lakini kwanza ili kuweka kumbukumbu sahihi katika majibu yake alitaja *Tanga Cement* na sio *Tanga Cement* ni *Twiga Cement.* Naamini kwamba *DSE* imeanzishwa kwa kufuata taratibu za Kimataifa *(International Standard)* na kwa utaratibu huo ni kwamba utaratibu unasema "*first come first served"*. Sasa kama Serikali imetoa waraka huu ambao ni "*Prospectus*" kwamba hisa zikizidi fedha zitarejeshwa. Tayari tunaishusha hadhi ya *DSE* kwa kuendesha taratibu za hisa Kimataifa na hivyo basi nataka kusema kwamba Benki pamoja na "*Brookers"* na wale ambao …

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge Rished

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Naam!!!

**NAIBU SPIKA:** Ukituhutubia tu utatuharibia, uliza swali.

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Swali ni kwamba Benki na *Brookers* wamekusanya fedha za wanaotaka kununua hisa na hatimaye wakazirejesha baada ya mizei miwili. Je, huoni kwamba kitendo hicho hawakuwatendea haki walionunua hisa na kwa kufanya hivyo inabidi warudishe hisa hizo kwa sababu wao wamewekeza katika hisa hizo? Serikali tunatarajia itauza hisa za *NMB.* Je, kwa utaratibu huu wataweka viwango hisa ngapi kila mmoja anunue au watawacha wazi kila mmoja anunue hisa ambazo anamudu hatimaye msije mkatoa waraka wa "*Prospectus"*?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO)** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kweli kuna taratibu za Kimataifa. Lakini vile vile ni ukweli kwamba *DSE* ina sheria zake. Kwa hivyo tunafuata zile sheria ambazo zina-*govern DSE.* Mkataba uliokuwepo ni "*Prospectus*" na kulikuwa na "*Stock Brookers*" ambao kwa kawaida wanamshauri mtu yoyote ambaye anataka kununua hisa. Sasa hatuwezi kwenda nje ya zile taratibu ambazo zilikuwa zimewekwa kwenye "*Prospectus"*.

Pili, fedha hizi zilikuwepo kwa kipindi cha miezi miwili na kiutaratibu huwezi kuwekeza hizo fedha katika kipindi cha miezi miwili kabla maamuzi hayajafanyika nani wameshinda na nani hawakushinda. Baada ya utaratibu huu wote kufanyika fedha zilirudishwa kwa wahusika katika muda wa siku mbili na kila mmoja alipata fedha zake. Suala la pili, kuhusu *NMB*. Utaratibu umeandaliwa wataalamu wameteuliwa sasa hivi wanashughulikia *prospectus* haijatolewa si vizuri nikataja yale yatakayokuwemo katika *prospectus* kabla hata wataalam hawajatoa ushauri wao Serikalini.

Na. 51

**Fedha Iliyotengwa Kwa Ajili ya Mikopo ya Wananchi**

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali katika Bajeti ya Mwaka 2006/2007 ilitenga shilingi bilioni moja kwa kila Mkoa kwa ajili ya mikopo kwa wananchi:-

(a) Je, Serikali imekopesha watu wangapi hadi sasa hapa nchini?

(b) Je, ni watu wangapi Wilayani Mpwapwa na Mkoa wa Dodoma kwa ujumla wamepatiwa mikopo hiyo hadi sasa?

(c) Kwa kuwa, wananchi wengi wanashindwa kuipata mikopo hiyo kutokana na masharti magumu ya Benki. Je, Serikali itatumia utaratibu gani mwingine wa kuhakikisha kwamba, wananchi wengi wanapata mikopo hiyo bila usumbufu wowote?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. JEREMIAH S. SUMARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, napenda kujibu swali la Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, swali lake lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba hadi kufikia tarehe 31 Mei, 2007, kupitia Mfuko wa Uwezeshaji, Benki za *NMB* na *CRDB* zilikwishatoa mikopo kwa jumla wajasiriamali 21,789 kutoka Mikoa yote Tanzania Bara yenye thamani ya shs. 17,970,046,659/=. Utoaji wa mikopo hii bado unaendelea kupitia Benki hizo mbili.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, hadi tarehe 31 Mei, 2007, idadi ya wajasiriamali waliopata mikopo hii katika Mkoa wa Dodoma ni 594, yenye thamani ya shs. 243,269,333/=

Kati yao wanaotoka Wilaya ya Mpwapwa ni wajasiriamali 119 waliokopeshwa jumla ya shs. 48,650,000/=

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Masharti ya Mikopo hii yamerahisishwa ili kuwawezesha wananchi wa kawaida kukopa kwa ajili ya kuendesha miradi yenye kuwapatia mapato. Unafuu wa mikopo hii inatokana na:- kwamba mikopo inatolewa bila kuweka dhamana, riba haizidi 10% waombaji hawatakiwi kuandaa michanganuo ya miradi, mwombaji hadaiwi kulipia ada ya mkopo na kadhalika.

Hata hivyo lipo tatizo la Benki hizo mbili kutofika maeneo ya mbali na Makao Makuu ya Wilaya na kwa baadhi ya Wilaya hakuna matawi ya Benki. Katika kutatua tatizo hili Serikali kupitia Benki Kuu inakamilisha utaratibu wa aina ya pili wa utoaji mikopo hii utakaohusisha Taasisi ndogo ndogo za kifedha zilizoko mikoani ili zipewe sehemu ya fedha hizo nao wawakopeshe wajasiriamali ambao kwa sasa hawafikiwi na Benki hizi. Hivi sasa Benki Kuu inafanya zoezi la kuzitambua Taasisi hizo kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Baada ya kuzitambua zitaingia Mkataba na Serikali ili zishiriki kutoa mikopo hii yenye masharti nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa Serikali inafanya tathmini kuhusu mafanikio na matatizo yaliyojitokeza katika mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa mpango huu ili kuuboresha tunapoingia mwaka wa pili wa utekelezaji. Maoni ya Waheshimiwa Wabunge na wadau wote yatazingatiwa katika tathmini hii. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa jibu lake zuri nina swali la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba niwatu 119 tu ndiyo waliopata mikopo katika Wilaya ya Mpwapwa na kwa kuwa Wilaya ya Mpwapwa ina idadi zaidi ya watu 150,000. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana na ushauri wangu kwamba kwa kuwa tumehamasisha wananchi wameunda *SACCOS* katika Kata kwanini Serikali inaogopa kupeleka fedha hizi kwenye *SACCOS* ili wananchi wengi waweze kupata mikopo hiyo?

Swali la pili, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba pamoja na kwamba hii riba ya asilimia 10 ya Benki za *CRDB* na *NMB*. Lakini kwa kuwa wananchi wanashindwa kuchukua mikopo hii kutokana na hii kutokana na hii riba ya asilimia kumi. Je sasa Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana na mimi kwamba riba ikiwa ndogo wananchi wengi watapata mikopo wakiwemo wananchi wa kata za Matomondo, Kimagai, Mima na Kata nyingine za Wilaya za Mpwapwa?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza mikopo hii inatolewa kwa makundi matatu. Kundi la kwanza ni mjasiliamali mmoja mmoja. Kundi la pili ni vikundi ambavyo vimetambulika rasmi kwenye ngazi ya Kata au kwenye ngazi ya Wilaya na hata kwenye ngazi ya Kijiji chenyewe na kundi la tatu ni la *SACCOS*. Kwa hiyo, nakubaliana kabisa na Mheshimiwa

Mbunge wa Mpwapwa kwamba tuendelee na mpango huu wa kutoa mikopo si tu kwa haya makundi mawili ya kwanza lakini vile vile mikopo itolewe kwa *SACCOS*; na Mikopo hii inatolewa kwa *SACCOS* pale ambapo zenyewe zimekuwa tayari zimeomba. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba *SACCOS* yoyote kwenye Jimbo lake la Mpwapwa pale ambapo itakuwa imeomba mikopo itafanyiwa tathimini ya kawaida za kibenki na watapewa mkopo. *(Makofi)*

Sisi tunaamini kwamba kama Serikali riba ya asilimia kumi ni ndogo na ninafuu kuliko riba ambayo inapatikana mahali pengine popote. Kwamba haiwezekani kushuka chini ya kumi na kweli tukawa tunawatendea hawa wananchi wenyewe haki. Kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Mbunge wa Mpwapwa aendelee kuwahamasisha wananchi kwenda kuomba mikopo hii lakini vilevile atusaidie kuwatangazia wananchi kwamba haiwezekani mahali popote hapa nchini sasa hivi kupata mkopo wa riba nafuu chini ya asilimia kumi ambayo Serikali imeidhinisha.

Na. 52

**Mwanafunzi Aliyeuawa na Polisi Mkoani Mbeya**

**MHE. ZITTO K. ZUBERI** aliuliza:-

Kwa kuwa mwezi wa Novemba mwaka 2000 Polisi Mkoani Mbeya walimuua kwa kipigo mwanafunzi Michael Sikupya wa Sekondari ya Iyunga, Mbeya. Na kwa kuwa uchunguzi wa mauaji hayo unafanywa na Jeshi la Polisi:-

(a) Je, Serikali ipo tayari kutoa matokeo yake na kunipa nakala ya uchunguzi huo?

(b) Je, Serikali imechukua hatua gani dhidi ya askari waliofanya mauaji hayp?

(c) Je, ni lini Jeshi la Polisi litaomba radhi kwa wazazi wa marehemu?

**NAIBU WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zitto Kabwe Zuberi Mbunge wa Kigoma Kaskazini, lenye sehemu (a),(b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka hatua hii tuliyofikia Serikali haikubaliani na Mheshimiwa Zitto kwamba mwaka 2000 Polisi Mkoani Mbeya walimwua kwa kipigo mwanafunzi Michael Sikupya wa Sekondari ya Iyunga, Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilichotokea ni kwamba mnamo tarehe 26 Novemba, 2000 majira ya ya saa 2.30 usiku wanafunzi wa Shule ya Sekondari Iyunga walifanya vurugu kubwa shuleni hapo zilizosababisha Askari Polisi kwenda kwenye tukio hilo kwa madhumuni ya kutuliza ghasia hizo. Katika kutuliza ghasia hizo wakati eneo lote la

shule likiwa kwenye giza Askari na wanafunzi walijeruhiwa kwa mawe yaliyokuwa yakirushwa na wanafunzi. Katika vurugu hizo baadhi ya wanafunzi walikamatwa akiwemo marehemu. Wakati wenzake wanahojiwa Kituoni marehemu na Askari aliyejeruhiwa walikimbizwa Hospitali ya Rufaa Mbeya kwa matibabu ambako marehemu alilazwa kwa matibabu zaidi na kufikia tarehe 3/12/2000 alifariki dunia akiwa hospitali.

Kutokana na mashaka yaliyojitokeza kuhusu kifo hicho jalada la Polisi lilifunguliwa ili kufanya uchunguzi wa kina kuhusu kifo hicho na baada ya upelelezi ilionekana kuwa ni vigumu kuthibitisha mahakamani shitaka la mauaji dhidi ya Askari Polisi au mtu mwingine yeyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia hali hiyo Mkurugenzi wa Mashtaka nchini *(DPP)* alielekeza kwamba shauri hilo lifanyiwe utafiti wa kifo cha marehemu yaani *inquest* na hivyo kufunguliwa shauri Na. 152/2003 na kufikishwa Mahakamani.

Mnamo tarehe 3 Aprili, 2007 shauri liliendelea kusikilizwa na mashahidi wawili walitoa ushahidi wao na kwa sasa shauri limepangwa kusikilizwa tena mnamo tarehe 2/7/2007. Kutokana na shauri hili kuwa mbele ya Mahakama hatutakuwa tunazingatia Sheria za Nchi kulijadili suala hili ndani ya Bunge hili kwa hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo Jeshi la Polisi kwa misingi ya kibinadamu na kuwa na kutambua uchungu wa kifo cha kijana huyu linatoa pole kwa wazazi, ndugu, jamaa wa marehemu na wengine wote walioguswa na msiba huo. *(Makofi)*

**MHE. FATMA M. MAGHIMBI**: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Endapo itaathibitishwa Mahakamani kwamba Askari hawa wamemwua kijana huyu na suala hili linafanana kabisa na lile tatizo lililotokea enzi ya Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi alipokuwa Waziri. Je, ikithibitika Waziri pamoja na Naibu wake wako tayari kujiuzulu kama ustaarab alioufanya Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi?

**NAIBU SPIKA**: Tutangoja kwanza Mahakama ithibitishe halafu tutaamua. Tunaendelea na swali linalofuata. Wizara ya Mifugo.

Na. 53

**Kuhamishwa kwa Wafugaji - Mbeya**

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA** aliuliza:-

Kwa kuwa jitihada za Serikali ya Mkoa wa Mbeya kuwahamisha wafugaji kutoka mabonde na maeneo muhimu kimazingira zimefanikiwa kwa kiwango kikubwa Mkoani humo; na kwa kuwa, wafugaji waliovamia Bonde la Ziwa Rukwa Jimbo la Songwe wanahamishiwa maeneo ya Milimani – Mbangala na Lipyu ambako mahitaji muhimu kama malambo na majosho hayapo; na kwa kuwa Serikali iliahidi

kushughulikia miundombinu yote inayohusika kabla mifugo haijahamishiwa katika maeneo hayo;-

(a) Je, ni lini Serikali itaanza kushughulikia suala la miundombinu hiyo?

(b) Kwa kuwa maeneo wanayohamishiwa bado yana mbung'o wengi sana. Je, Serikali inaweza kufungua kituo cha kupambana na wadudu hao ili mifugo inayopelekewa huko isiendelee kudhurika?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Guido Gorogolio Sigonda, Mbunge wa Songwe, napenda kutoa maelezo mafupi yafuatavyo:-

Mwezi Aprili, mwaka wa 2006, Serikali ilitoa tamko kuhusu uharibifu na uchafuzi wa mazingira katika maeneo oevu na vyanzo vya maji. Tamko hilo, pamoja na mambo mengine liliwataka wafugaji na mifugo yao kuondoka katika maeneo hayo. Mkoa wa Mbeya ulifanikiwa kuwaondoa takriban ng'ombe 303,254 kutoka Bondo la Ihefu ambapo inakisiwa kuwa ng'ombe 100,000 kati ya hao walihamia Wilaya ya Chunya. *(Makofi)*

Baadhi ya wafugaji hao walihamia katika Bonde la Songwe kutokana na kuwepo kwa maji na malisho ya kutosha. Hata hivyo, kutokana na uharibifu wa mazingira na migogoro iliyoanza kujitokeza kati ya wafugaji na wakulima, Serikali iliingilia kati ili kunusuru hali hiyo kwa kuwahamishia wafugaji katika maeneo ya milimani ya Mbangala na Lupa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa 2006/2007, Serikali iilanza kujenga miundombinu katika maeneo walikohamishwa wafugaji, kwa kutoa kiasi cha shilingi milioni 230 za kujenga malambo katika Wilaya ya Chunya (lambo moja), Kilwa (Malambo manne), Lindi Vijijini (malambo mawili), Kisarawe (lambo moja) na Nachingwea (malambo mawili). Fedha hizo zimetumika pia kujenga majosho katika Wilaya za Kilwa (majosho mawili), Nachingwea (majosho mawili), Lindi Vijijini (majosho mawili) na Rufiji (josho moja).

Hata hivyo, kutokana na kuchelewa kutolewa kwa fedha, ujenzi wa baadhi ya miundombinu ulichelewa kuanza hivyo Kazi hiyo inaendelea. Aidha, katika mwaka wa fedha wa 2007/2008, Serikali kupitia Mpango wa Maendeleo ya Kilimo Wilayani – *DADPs*, itajenga majosho matatu Wilayani Chunya katika vijiji vya Mwiji, Mbangala na Lupa.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba maeneo mengi ya Wilaya ya Chunya yakiwemo yale walikohamishiwa wafugaji, yana mbung'o wengi. Wadudu hawa pia hupatikana kwa wingi katika Mikoa mingine ya Kigoma, Rukwa, Tabora, Manyara, Kagera, Arusha, Pwani na Lindi. Serikali kwa kushirikiana na wafugaji katika maeneo yenye mbung'o hutumia mbinu mbalimbali za kuangamiza wadudu hao. Teknolojia zinazotumika ni pamoja na matumizi ya vitambaa vyenye dawa na chambo, mitego na mifugo iliyoogeshwa kwa kutumia dawa yenye uwezo wa kuua kupe na mbung'o pia.

Kutokana na kusambaa kwa mbung'o katika maeneo mengi nchini kama nilivyoeleza, ni gharama kubwa kwa Serikali kusambaza na kuendesha vituo vingi vya kudhibiti mbung'o. Wizara hutumia wataalam wake wa kituo cha Utafiti wa Mbung'o na Malale kilichoko Tanga pamoja na wale walioko katika Halmashauri za Wilaya kuanzisha vituo vya muda kwa kazi hiyo na kuhamia maeneo mengine baada ya kuweka mitego. Utaratibu huu umetuwezesha kupunguza mbung'o kwa kiasi kikubwa katika baadhi ya maeneo. Mbinu nilizozitaja, licha ya kuwa rafiki wa mazingira, ni endelevu kwa vile utekelezaji wake unashirikisha wafugaji wenyewe.

**MHE. GUIDO G. SIGONDA**: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa maelezo mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza kwa kuwa Serikali ya Mkoa pamoja na Wilaya yake zimetekelezwa hili agizo ambalo limekubaliwa vilevile na wafugaji.

Je, sasa hivi kama wafugaji wale kwa sababu miundombinu bado haijakamilika kama wafugaji wataanza kurejea kwenye maeneo hayo yule atakayelaumiwa ni Serikali au wafugaji wenyewe?

Swali la pili, miaka ya nyuma katika maeneo haya ambayo mifugo imepelekwa kulikuwa na kituo cha kupambana na Mbung'o. Majengo bado yapo lakini kituo hicho kilistishwa baada ya mifugo kupelekwa katika maeneo mengine. Sasa hivi mifugo imeanza kurejea. Je, Serikali haioni kwamba sasa ni wakati muafaka wa kurejesha kituo hicho?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio yaliyopatikana katika kuwahamishia wafugaji kwenye maeneo muafaka si vizuri sisi wenyewe tuyaangushe kwa kuwaruhusu kurejea. Kwa hiyo, Serikali inatoa wito wafugaji hawa na wananchi wote kwa ujumla waunge mkono uwamuzi huu mzuri wa Serikali ambao na wananchi wenyewe na wafugaji waliuafiki kwa moyo thabiti kabisa na tunawapongeza sana katika hilo.

Kuhusu, uwezekano wa kurejesha kituo alichokisema Mheshimiwa Mbunge, Wizara inaahidi kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge kuliangalia suala hili ili kusudi uamuzi muafaka uweze kuchukuliwa.

Na. 54

**Vyuo Vikuu Kufungua Matawi Sehemu Mbalimbali Nchini**

**MHE. JANET B. KAHAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa pamoja na nia nzuri ya Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine wa elimu nchini wakiwemo watu binafsi kujitahidi kuongeza idadi ya vyuo vikuu nchini, kumeibuka wimbi la vyuo vikuu hivyo kufungua matawi sehemu mbalimbali nchini, mfano Chuo Kikuu cha Mzumbe, Morogoro kilichoanzishwa siku za hivi karibuni tayari kina matawi Mbeya na Dar es Salaam, Chuo cha Tumaini kilichopo Iringa tayari kina kina matawi Moshi, Mbeya na Dar es Salaam:-

(a) Je, ni utaratibu gani unaotumiwa kukiruhusu Chuo Kikuu kuwa na matawi sehemu mbalimbali za nchi, ukiacha Makao yake Makuu?

(b) Je, Serikali haioni kwamba, utaratibu huo unaweza kutoa mwanya wa kutoa elimu duni na hivyo watu kuhitimu wakiwa na upeo mdogo wa fani husika hasa kwa kuzingatia kuwa, udhibiti wa mitihani wa Chuo husika pekee, licha ya kwamba inaweza kuwa na lengo la kuwapa watu wengi nafasi za vyuo hivyo pengine kwa gharama nafuu?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Janeth Kahama, naomba na mimi kuungana na mimi na Waheshimiwa Wabunge wenzangu pamoja na Watanzania wote kuwapongeza sana *Taifa Stars* kwa kazi nzuri waliyoifanya na kuwaombea dua ili wasonge mbele na hatimaye tushinde huko Ghana mwakani.

Baada ya pongezi hizo naomba sasa kwa Niaba ya Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia kujibu swali la Mheshimiwa Janeth Kahama lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 19(2) cha sehemu ya Tatu ya Sheria Namba 7 ya Vyuo Vikuu ya mwaka 2005 kinaviruhusu vyuo vikuu kuanzisha aina za matawi kulingana na Hati Idhini *(Charter)* ya chuo. Maamuzi yakishafanywa na vyombo vya chuo husika, chuo huomba kibali cha Kamisheni na utaratibu wa kukagua tawi hilo hufuatwa kulingana na Kanuni za Usajili za 2006 kabla ya kibali kutolewa. Utaratibu huu ndio uliofuatwa kutoa kibali kwa Chuo Kikuu Mzumbe kuendesha programu katika Kampasi za Dar es Salaam na Mbeya.

Aidha, mambo muhimu ya kutolewa maelezo katika kuwasilisha maombi hayo ni pamoja na:-

- Sehemu ambako chuo kinatarajiwa kujengwa na taratibu zinazofuatwa kupata hati ya ardhi ya chuo;

- Vyanzo vya fedha za ujenzi na uendeshaji

- Ø Miundombinu ya shughuli za taaluma na uongozi kama vile maktaba, chumba cha kompyuta, maabara, karakana, Ofisi n.k.;
- Ø Muundo wa uongozi wa chuo;
- Ø Programu za masomo zinazokusudiwa;
- Ø Idadi ya juu ya wanafunzi wanaotarajiwa kujiunga;
- Ø Mpango mkakati wa kipindi kisichopungua miaka mitano kueleza ukuaji wa chuo unavyotarajiwa;
- Ø Taratibu za kudahili wanafunzi na masharti ya kujiunga na masomo;
- Ø Gharama za masomo kwa mwaka;
- Ø Idadi, sifa za kitaaluma na uzoefu wa wanataaluma;
- Ø Taratibu za kuhakiki ubora wa elimu itakayotolewa;
- Ø Kanuni za mitihani, masharti ya kuhitimu masomo; na
- Ø Vyeti, stashahada na shahada zitakazotolewa.

Kamisheni huunda Kamati ya wataalam kutembelea eneo la chuo kukagua na kujadiliana na wenye chuo na uongozi wa mradi.

Taarifa ya wakaguzi hujadiliwa na Kamati ya Ithibati ya Kamisheni na baadaye Kamisheni yenyewse ambapo maamuzi na maelekezo hutolewa.

Kwa hiyo, Kamisheni ya Vyuo Vikuu Tanzania inasimamia moja kwa moja uanzishwaji wa matawi hayo ikiwa ni pamoja na kuzingatia mahitaji katika eneo husika.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu huu wa uanzishwaji wa matawi kama nilivyoeleza hapo juu hautoi mwanya wa kutoa elimu duniu. Aidha, zipo hatua mbalimbali za kudhibiti ubora wa elimu ya juu kwa kushirikisha vyombo mbalimbali kama Baraza la Vyuo Vikuu la Afrika Mashariki ambalo lina utaratibu wa kuangalia ubora wa mitaala ifundishwayo katika Vyuo/Matawi hayo.

Aidha, kuna Kamati za kitaaluma na wakaguzi kutoka nje ya nchi *(Accreditation Committees and External Examiners)* ikiwa ni pamoja na Kamisheni ya Vyuo Vikuu Tanzania inayosimamia ubora wa elimu ya juu katika Vyuo Vikuu na matawi yake kwa kuzingatia vigezo vilivyoainishwa katika sehemu (a) hapo juu, kazi ambayo ni ya

kudumu. Chuo ambacho hushindwa kufikia viwango hivyo husimamishwa kutoa masomo husika.

Aidha, ningependa kueleza zaidi ya kwamba Chuo cha Tumaini kilichoko Iringa hakina matawi Arusha, Moshi na Dar es Salaam bali Chuo Kikuu cha Tumaini Moshi (Makao Makuu) ndicho chenye matawi Arusha, Iringa na Dar es Salaam.

**MHE. JANET B. KAHAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na nashukuru pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa shabaha kubwa ya kuanzisha matawi katika vyuo hivi ilikuwa ni kuwawezesha wananchi wenye sifa ya kujisajili na kuendelea na masomo. Je, Wizara au Serikali imetumia mpaka leo mbinu gani au itatumia mbinu gani kuhamasisha wananchi wengine ili waweze kujiunga na vyo hivi na hasa katika eneo la masomo ya Sayansi na kwa wasichana?

Swali la pili ninataka kujua je, katika vyuo hivi kuna wanafunzi wowote wanaotoka nchi za nje na kama wapo katika nchi zipi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara yangu inahamasisha sana wananchi kujiunga na vyuo vikuu husasan watoto wa kike na tunazo programu mahususi kwa ajili ya wasichana hasa wa sayansi ambao tunawachukua katika vyuo kikuu lakini pia katika vyuo vya ufundi kwa kuwapa masomo special kwa masomo yale ambayo hawakufaulu vizuri ili waweze kuyafaulu na kujiunga na vyuo vikuu.

Pia tumeanzisha matawi hasa katika Chuo Kikuu Huria kila Mkoa na sasa hivi katika Mikoa wameanzisha matawi katika Wilaya. Hii yote ni njia ya Wizara kuhakikisha kwamba wananchi wengi wanafikiwa na elimu hii ya juu.

Na. 55

**Wanafunzi wa Kitanzania Wanaosoma Ukraine**

**MHE. HALIMA J. MDEE** aliuliza:-

Kwa kuwa taarifa kutoka Ubalozi wa Uingereza nchini Ukraine zinaonyesha kwamba wanafunzi wapatao ishirini na tisa (29) wametelekezwa na Serikali kwenye Vyuo mbalimbali nchini Ukraine. Hali iliyosababisha wanafunzi hao kujisalimisha na kuomba hifadhi kwenye Ubalozi wa Uingereza Jijini Keiv.

(a) Je, Serikali inasema nini kuhusiana na tukio hilo na inachukua hatua gani?

(b) Kwa kuwa taarifa zilizopo zinaonyesha kwamba Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia imekataa kuwatambua wanafunzi hao licha ya kwamba, iliwaahidi mikopo ya masomo tangu mwezi wa sita mwaka jana. Je, Serikali inasema nini juu ya hiyo?

(c) Kwa kuwa Ubalozi wa Uingereza – Ukraine uliipa Serikali ya Tanzania ofa ya kuwasaidia kuwalipia vijana hao, na kuwapa misaada mingine ya kibinadamu endepo tu Serikali ya Tanzania ingeandika barua kurudisha fedha hizo kwa Serikali ya Uingereza.

Je, kwanini Serikali haikupeleka jibu hadi leo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Halima Mdee, Viti Maalum napenda kutoa maelezo ya awali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa masomo 2005/2006 wanafunzi130 walipata udahali katika vyuo vikuu mbalimbali nchini Ukraine. Kati ya hao ni wanafunzi 84 tu ndio walikamilisha taratibu za kuondoka nchini pamoja na taratibu za kupata mkopo kutoka Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu na hivyo wakaweza kujiunga na masomo nchini Ukraine. Wengine 46 hawakuweza kukamilisha taratibu hizo na hivyo hawakuweza kuondoka kwa mwaka huo wa masomo.

Kwa mwaka wa masomo 2006/2007 taratibu za utoaji mikopo zilibadilika na wanafunzi hawa walishauriwa wajiunge na vyuo vya elimu ya juu ya ndani ya nchi. Wanafunzi 17 kati ya hao 46 walikubali kutafuta udahili katika vyuo vya elimu ya juu hapa nchini na hadi sasa wanaendelea na masomo. Wanafunzi 29 wenye matatizo nchini Ukraine ni kati ya wale 46 ambao hawakukubali ushauri wa Serikali wa kutafuta udahili hapa nchini na hivyo wakaamua kwa utaratibu wao binafsi kwenda Ukraine.

Aidha ikumbukwe kuwa kwa mwaka wa masomo 2006/2007 Serikali haikukopesha mwanafunzi yeyote mpya wa mwaka wa kwanza nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya naomba sasa nijibu swali la Mheshimiwa Halima Mdee (Viti Maalum) lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Naibu Spika, si kweli kwamba Serikali imewatelekeza wanafunzi waliokwenda nchini Ukraine. Kwa kuwa wazazi wao waliamua wao wenyewe kwa nia ya kuwapatia watoto wao elimu ya juu, waliwapeleka watoto hao kwenda kusoma nje ya nchi kwa gharama binafsi. Serikali haiwajibiki na gharama za mafunzo kwa wanafunzi waliokwenda Ukraine kwa udhamini binafsi. Hatua iliyochukuliwa na Serikali ni kuwapatia ofa ya tiketi kwa kil mwanafunzi ili waweze kurejea nyumbani.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu haikuwaahidi wanafunzi hao kuwapata mikopo kwa ajili ya gharama za mafunzo yao.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haijawahi kupata barua yoyote kutoka Ubalozi wa Uingereza nchini Ukraine kuhusiana na Ofa ya kuwasaidia wanafunzi hao.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika nashukuru. Kwa kuwa kumbukumbu za Wizara batch 6, 7 na 8 zinaonyesha wanafunzi ambao walikubaliwa mikopo ambao na hawa tunaowazungumzia wapo na vyuo ambavyo wanakwenda kusoma. Sasa naomba Mheshimiwa Naibu Waziri aniambie hizo pesa ambazo ndani ya kumbukumbu zako zipo zilikwenda wapi na akina nani waliosomeshwa?

Swali langu la pili ni dogo tu linasema kwamba kulikuwa kuna mawasiliano baina ya Chuo Kikuu cha Kakov na Wizara na mawasiliano hayo yalitokana kwamba kulikuwa na delay ya hawa wanafunzi hali ambayo iliwafanya kwenda shule na Wizara ikaomba ihifadhi hizo nafasi zao hadi Septemba 2006 na Wanafunzi hao.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mdee, swali tena sio habari tena *be brief.*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa  Naibu Spika ndiyo naelekea huko. Na wanafunzi walipokwenda Bodi ya Mkopo, Bodi iliwahakikishia kwamba Mikopo yao ipo kwa sababu mabadiliko haya ya 2006 hayatawahusu. Sasa naomba Mheshimiwa Naibu Waziri aniambie ilikuaje mabadiliko ya mwaka 2006 hayawahusu wakati tayari walikuwa wameshapata pesa huko nyuma?

**WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika kwanza nimpongeze Mheshimiw Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini la pili nataka kueleza mpango uliokuwa unatumika baada ya kuwapata wanafunzi ambao wanatakiwa kupewa *scholorship* wale wanafunzi 130 ambao walikuwa eye marked kwa ajili ya kwenda masomoni wakingojea taratibu zikamilishwe ikiwa ni pamoja na kuwa na *passport* kuwa na Visa tiketi na mambo mengine walikuwa tayari wanapangwa katika makundi ambayo mnayaita batches 1, 2 hadi hiyo 7 anayoizungumzia. Lakini waliochukuliwa ni wale tu ambao walikuwa wamekamisha taratibu hizo na kuweza kuondoka nchi. Kwa hiyo kuwekwa kweny batch haikuwa na maana kwamba is automatic ilikuwa ni lazima kwanza ukamilishe utaratibu.

Pili, kwamba kulikuwa na mawasiliano na Wizara kwamba chuo hicho kingewawekea nafasi wanafunzi ambao walikuwa hawakutimiza masharti huu mkataba haukuwepo wala mawasiliano ya namna hii hayakuwepo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri nakushukuru, mengine mtajadili kwenye hotuba ya Waziri.

Na. 56

**Tatizo la Soko la Bidhaa Nchini**

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA** aliuliza:-

Kwa kuwa biashara ya viungo imeshamiri katika nchi za Uarabuni; na kwa kuwa wanawake nchini wanasumbuka sana kutafuta soko kwa ajili ya bidhaa zao:

Je, ni lini Serikali itaandaa mikakati maalum wa kuwatafuta soko wanawake katika nchi hizo kama wanavyofanyika wenzetu wa nchi nyingine?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kutambua umuhimu wa baishara ya bidhaa za mazao ikiwemo viungo ndani ya nje ya nchi imeandaa mikakati mbalimbali ya kukuza mauzo ya bidhaa hizo nchi za nje ikiwa ni pamoja na nchi za Uarabuni na mikakati hiyo ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuidhinisha mpango wa kukuza mauzo ya bidhaa nje (*DTIS*) ambao moja ya malengo yake ni kubainisha mazao yenye thamani ya juu katika soko la kimataifa ikiwa ni pamoja na viungo. Wizara yangu inawasiliana sasa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuona namna bora zaidi ya kuuza viungo nje

(ii) Kuanzisha Kituo cha Biashara cha Dubai (Dubai *Trade Centre*) ambacho kitakuza mahusiano ya kibiashara kati ya Tanzania na nchi za Uarabu kwa kutangaza bidhaa za Tanzania na pia kuwaunganisha wafanyabiashara wakiwemo wanawake na masoko ya nchi za Kiarabu. Mwambata wa kibiashara ameshateuliwa na kituo kitaanza kazi rasmi katika mwaka wa fedha wa 2007/2008.

(iii) Serikali ya Muungano inajadiliana na Serikali ya India kwa lengo la kuwezeshwa kupata soko la viungo toka Tanzania huko India.

(iv) Kuviwezesha vikundi vya wajasiliamali wanawake kushiriki katika maonyesho ya kimataifa ili kujifunza mbinu mbalimbali za biashara ya kimataifa na kutangaza bidhaa zao. Kwa mfano mwezi Aprili 2007, Tanzania ilishiriki katika maonesho ya kimataifa ya *Canton* huko China na vikundi vya wanawake vilishiriki katika maonesho hayo. Ujuzi walioupata katika maonesho haya utasaidia kupata masoko katika nchi za kiarabu na kwingineko duniani.

(v) Kutoa mafunzo ya ubora wa bidhaa za viungo na dira ya ufungashaji wa bidhaa unaokidhi mahitaji ya masoko nchi za Uarabuni na nchi nyingine duniani.

Mheshimiwa Spika, ni imani ya Wizara yangu kuwa utekelezaji wa mikakati niliyoitaja utaweza kuwasaidia wanawake na wananchi kwa ujumla kuweza kupata masoko ya bidhaa za viungo nchi za Urabuni na kwingineko duniani.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza na pia namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Nchi za Bara Hindi ikiwemo India, Pakistan na Bangladesh wamefaulu sana katika kupeleka bidhaa zao hizi nchi za Uarabuni. Na kwa kuwa hivi karibuni alikuja Mtaalam, Dr. Mohamed Yunus, ambaye ameanzisha Benki, *Gramine Bank* huko Bangladesh kwa ajili ya kuwasaidia wajasiriamali.

Je, Serikali kupitia Mtaalam huyu, kwa nini isimwombe kutupatia wataalam ambao wataweza kuwepo nchini ili kutoa mafunzo kwa ajili ya kusindika bidhaa hizi na kuzisafirisha nje?

**NAIBU SPIKA:** Dr. Yunus ni Mtaalam wa mambo ya Benki, inayoitwa *Gramine Bank.* Waziri unaweza kujibu?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ulivyosema Mtaalam huyo aliyemtaja Mheshimiwa Mbunge ni Mtaalam wa Benki za Wananchi, hapa nchini tukiziita *SACCOS*. Kwa hiyo, madamu alishakaribishwa hapa nchini kuja kutoa ushauri juu ya uanzishaji wa *SACCOS* ambayo madhumuni yake ni kuhamasisha Wajasiriamali, bila shaka na hata Taasisi zingine za kuwafanya wananchi waweze kufanya biashara zinaweza zikazingatia.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ni lazima tukubali kwamba leo swali moja limeshindikana. Tathmini ni kwamba yanapoulizwa maswali ya nyongeza, watu wanaanza hadithi, halafu hata Waheshimiwa Mawaziri wanaanza na historia fulani, halafu ndipo wanaanza kujibu maswali. Sasa, nadhani kwa maswali 10 kwa saa moja, tukianza historia kweli hatutakuwa tunamaliza. Fikiria hapo nimekwenda *rough* sana, hakuna maswali mawili ya nyongeza, bado imeshindikana.

Kwa hiyo, naomba historia za maswali zisiwepo na muulizaji unapouliza swali, historia isiwepo. Tunakoiga *Commonwealth*, hakuna habari za namna hiyo. Kwa hiyo, tunapiga hotuba badala ya kuuliza maswali. Kwa hiyo, naomba tujaribu kufanya hivyo kusudi tuwatendee haki wale wote wanaouliza maswali yao kwa mujibu wa utaratibu.

Waheshimiwa Wabunge, siku ya kuchangia Ofisi ya Waziri Mkuu ni siku tano, siku mbili kwa ajili ya TAMISEMI pamoja na siku ambayo Waziri Mkuu mwenyewe anaisoma na siku ya kujibu. Kwa hiyo, tuna nafasi nyingi sasa katika Wizara hii ya Fedha. Kiutaratibu haina tofauti sana uchangiaji Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara ya Fedha na Mipango. Hakuna tofauti kwa sababu unaweza kuogolea *anywhere*.

Kwa hiyo, naomba wale wanaosema tutachangia kwa Waziri Mkuu, warudi kwa Wizara hii. Waseme yale yale waliyokuwa wanataka kumwambia Waziri Mkuu, waseme leo kwa sababu wote Serikali nzima iko hapa. Kwa hiyo, naomba sana msiombe tu kwamba tutachangia kwa Waziri Mkuu, itakuwa *loaded* mno. Kesho sisi tutakuwa na nafasi. Tunategemea kumaliza kesho kabla ya asubuhi. Kwa hiyo, tunao muda. Tafadhali ombeni kuchangia Wizara hii na watakaobaki tutawapeleka Ofisi ya Waziri.

## HOJA ZA SERIKALI

**Hali ya Uchumi kwa Mwaka 2006, Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2007/2008 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2007/2008**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika hoja hii. Kwanza kabisa, naunga mkono hoja zote mbili. Pia ninawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wa Wizara ya Mipango na Waziri wa Fedha pamoja na Wataalam wao wote kwa maandalizi mazuri haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sipendi kupoteza muda kwa kurudia yale mambo mazuri ambayo wenzangu wamesema. Lakini, ningeopenda nianze na jambo moja la msingi kwamba kujitawala hasa ni kujitegemea, ndio tafsiri yake. Wale ambao tumekuwa hapa Bungeni muda mrefu na hata hawa wenzetu waliokuja juzi, tutakubaliana kwamba kwa historia ninayokumbuka mimi, kila bajeti ya Serikali, Serikali ilikopa kwa Mabenki kwa kupitia kuuza *bond* zake.

Kwa mara ya kwanza katika historia, safari hii Serikali haikopi ndani ya nchi. Haya ni mafanikio makubwa sana na huko ndiko kujitegemea. Hii maana yake nini? Kwa Serikali kutokukopa kwenye Mabenki, Mabenki yatakuwa na fedha ya kutosha kuweza kukopesha wananchi kwa ajili ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, ningependa kusema mambo yafuatayo:- La kwanza, natoa ushauri kwamba kama kuna mambo mazito na ambayo Mbunge angependa kuyasema, mimi nafikiri kuhutubia habari za *Internet* haitoshi kuwa ndio ushahidi sahihi. Kwa sababu baadhi ya mambo tunayoyafahamu sisi wengine tumeyafanyia *research*. Kwa mfano, suala lililozungumzwa kuhusu fedha ambazo zinasemekana zimepotea au zimetoka vibaya Benki, bahati nzuri mimi naweza kusema *with authority* kwa sababu nimeishafanya *research* na nina habari zote zinazohusiana na jambo hili, zote ninazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kushauri tu, kwanza takwimu si sahihi. Takwimu sio dola milioni 200, ni dola milioni 131, ndio takwimu sahihi. La pili, baadhi ya wafanyabishara wanaweza wakatumia ujanja wa kuwatumia Wabunge waje wasemee mambo yao au tofauti zao katika biashara. Na jambo hili linahitaji kuliangalia. Mimi kwa bahati nzuri habari hii naijua kutoka kwa mhusika mwenyewe ambaye ni Mtanzania na mwingine ni Mzimbabwe yuko South Africa. Nimezungumza na nafahamu habari hii. Kwa hiyo, mimi nafurahi kwamba Serikali yetu imekubali kwamba jambo hili litafanyiwa ukaguzi. Ukaguzi utakapofanyika, tutajua wote ukweli wa jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi ningependa niseme kwa kifupi sana juu ya jambo hilo. Lakini, vile vile liko suala la Jengo. Mimi nilishawahi kuwa Mjumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi. Tulipata nafasi ya kutembelea Jengo la Benki Kuu. Wajumbe wengi tuliridhika kwamba utaratibu kwanza wa kupata Mkandarasi ulifuatwa.

Waombaji walikuwa wengi, wakachujwa wakabaki sita, na katika sita hao Kampuni ya Kwanza iliyokuwa imepewa tulivyoambiwa wakati ule kwenye Kamati yetu ilikuwa Kampuni ya Sweden ambayo ni Kampuni kubwa sana Duniani, *SAKANSKA* ndio waliopewa kwanza. Walipojitoa wenyewe, ndio ikapewa Kampuni nyingine ya Ujenzi ambayo inafanya kazi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilipokuwa Mbunge miaka ya kwanza kabisa, nilipata nafasi ya kuwa Mkurugenzi wa Bodi ya Bima baada ya kutaifishwa. Lile Jengo la Kitega Uchumi la sasa, wakati ule sisi tulipoamua kujenga ilikuwa 40,000/=, Jengo la Bima, wakati ule mwaka 1967. Na wakati ule tuliandikwa na magazeti kwamba tumetumia fedha vibaya. 40,000/= tumetumia vibaya!

Leo lile jengo ukitaka kuliuza ni mamilioni ya fedha. Kwa hiyo, hatukuwa tumekosea. Hata Jengo hili la Benki Kuu, kwa sasa tunaweza tukadhani ni gharama kubwa. Lakini, baada ya mika 10 ijayo, tutafurahi kwamba waliotutangulia walifanya busara kujenga jengo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nieleze vile vile kwa sababu ukisema mambo haya ni kana kwamba Benki yetu ni chafu sana au kuna mambo hovyo sana. Mimi nimefanya utafiti pia, kwa Afrika kama ukipanga benki, ukitaka kuziweka benki kwa mfumo wa kumi bora, Benki Kuu ya Tanzania itakuwa Miongoni mwa Benki nzuri na inayofanya vizuri katika kumi bora za Afrika. Kwa mfano, mwaka 1995, *Reserve* ya Tanzania ilikuwa milioni 271.

Baada yamiaka 10 tumepanda kutoka milioni 271 na kufika bilioni 2.4, *Reserve* zetu hizo. Hata leo pamoja na matatizo ya mwaka jana kwamba mvua hazikuwa nzuri, kulikuwa na ukame, njaa ilitokea, lakini, bado hata hivi nazungumza, nimetoka ku-*check*, akiba *(Reserve)* zetu leo tukizungumza ni bilioni 2.2. Kwa hiyo, lazima tujisifu kwamba tunafanya kazi nzuri na kusimamia uchumi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niliona hayo mambo mawili niyaseme. Sasa, baada ya hayo ningependa niseme mambo machache yafuatayo yanayohusu uwezeshaji:-

Sivyo vizuri mtu ukisema, useme jambo linalokuhusu, si nzuri maana yake, kwanza Duniani mtu anayejisifu, hana sifa, inatakiwa wenzako ndio wakusifu. Mimi sasa ni miongoni mwa Watanzania wazalendo waliowekeza vizuri. Mimi ni mwekezaji na napenda nitumie nafasi hii kuishukuru Serikali yangu Awamu ya Tatu na Nne kwamba mafanikio yaliyosema kwenye magazeti na aliyosema Rais alipofika Sumbawanga baada ya kufungua kile kiwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba shukrani zangu ziende kwa Serikali maana ndiyo iliyoniwezesha na Waheshimiwa Wabunge bila kutia chumvi, na kwa kuwa wahusika Mabalozi zaidi ya Saba walifika Rukwa kwenye kongamano na walitembelea Kiwanda, wenyewe wazungu wa Ulaya, Mabalozi, wamekubali kwamba kile kiwanda cha Sumbawanga kwa *East Africa* ni cha Kwanza na kina *Europian Srandards*, kina hadhi ya Kimataifa ya Ulaya. Mimi naweza kufanya biashara ya nyama na ya Ulaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi ili kuondoa hisia kwamba tukisema wawekezaji, maana yake ni wageni. Lazima tulikate jambo hili. Sisi Wabunge tulikatae jambo hili. Sisi Wabunge tulikatae napenda vile vile na Serikalini na katika Vyombo vyetu vya Benki wao waamini vile vile kwamba sisi Waswahili tunaweza vile vile. Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu *process* niliyopita mimi siwezi kuieleza hapa, nitawapotezea muda kwa sababu itachukua muda mrefu sana.

Lakini, nimepata usumbufu mkubwa sana mpaka kufika pale nilipofika. Kwa sababu ya hisia tu kwamba sisi tauwezi, wako watu wanapata mikopo kwa kupiga simu kwenye Benki, wako watu wamepata mikopo kwa Maaofisa wa Baadhi ya Benki kwenda nyumbani kwao kuandika miradi. Lakini, ninyi wote humu hakuna anayeweza kufanya hivyo, kwa sababu kuonekana tu mweusi ni kasoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nimepata uzoefu mkubwa kwa jambo hili. Kwa hiyo, mimi natoa wito mambo mawili:- La kwanza, Serikali yetu imedhamiria kuwawezesha wazawa – Watanzania Wazalendo. Ninapendekeza urasimu upunguzwe. Lakini vile vile napendekeza kwamba kule Benki Kuu kiwekwe kitengo au Idara Maalum ambayo itashughulikia uwezeshaji, kazi yao iwe ni hiyo tu. Itasaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, mimi niko tayari sasa ikiwa kuna Wabunge ambao wangependa kuhangaika na kushughulikia mambo haya. Mimi niko tayari kushirikiana nao na kutoa *free consultancy*. Naomba tukubaliane Waheshimiwa kwamba Ubunge usiwe ajira. Ubunge uwe ni uwakilishi, maana hata hao wanaotukana kwamba ooh sijui tunadai mapato, wanadhani tumeajiriwa, hapana, tumechaguliwa na wananchi tuwawakilishe. Kwa hiyo, naomba wenzangu mimi niko tayari kama nilivyosema kushirikiana nanyi katika jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile katika suala hili la uwezeshaji ambalo Serikali imeamua kulifanya, nashauri mambo mawili:- La kwanza, tuwajue Watanzania. Tunao watu wamesoma katika fani mbali mbali; Kilimo, Viwanda, Utalii, hao tuwasaidie ili waweze kuingia katika kuwa na ubia. Wenzetu kwa mfano, ukifika kama Dubai au nchi za wenzetu kule, mgeni hawezi kupata usajili wa kuanzisha Kiwanda au Kampuni mpaka kuwe na mwananchi wa nchi hiyo. Sisi tukitaka kufanya, inakuwa mgogoro. Kwa hiyo, mimi naomba hayo iwe *deliberate to process* kwa sababu ndivyo tulivyosema katika Ilani na katika Sera kwamba kila Kampuni ya Watazania ndiyo itamiliki asilimia kubwa zaidi kuliko wale wageni.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo mawili mengine ambayo ningependa niyaseme hapa:- La kwanza ni kuwa Bandari yetu ya Dar es salaam ikisimamiwa vizuri, ni Mgodi. Ni mgodi mkubwa sana. Pili, utalii na uwindaji wa kitalii vyote kwa pamoja vikisimamiwa vizuri, kwa kweli ni zaidi ya dhahabu, kwa sababu uwekezaji katika uwindaji na utalii siyo mkubwa sana kama vile mgodi.

Tatu, wenye migodi yote iliyo hapa Tanzania, ningeomba Wizara ya Mipango na Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na Viwanda na Biashara, tukubaliane kwamba

kinachoweza kuwasaidia Watanzania na wananchi kupata manufaa kwa migodi hii ni kufanya biashara ili mazao na mahitaji yao yote yatoke nje, wanunue vitu vya hapa hapa Tanzania kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu ningependa niseme kuwa kwa utaratibu uliopo sasa wa Kilimo, naishauri Serikali itoe upendeleo kwa *TFC* ambao hawa wanaweza kusambaza mbolea vizuri zaidi kuliko kampuni za watu binafsi, maana yake wana nafasi na ni Shirika letu tulisaidie.

Pia, ninapendekeza kuwa Serikali yetu ianzishe Kanda za Maendeleo ili kinachowezekana iwe kwanza ni kuandaa Miundombinu katika kila eneo tunakotaka kupeleka watu kuanzisha viwanda. Kwa sababu sasa hivi, kwa mfano ukifika katika Mikoa, utakuta hakuna maeneo ya kuweka viwanda. Ukienda kuwaalika hao wawekezaji wakija watakuta hakuna umeme, hakuna maji. Kwa hiyo, naomba tukubaliane kuwa na *Zone* hizo na Serikali isaidie kutanguliza miundombinu ili iweze kusaidia wale wanaowekeza viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, napenda tena kurudia kusema ahsante sana. Naishukuru Serikali na naomba wote tushirikiane kwa sababu maendeleo ya nchi yetu hawezi kule Rais wa nchi, ni sisi wenyewe. Na napenda nifurahi kusema wenzetu kwa upande wa upinzani wanatambua na wamesifu Serikali kwamba ni sikivu. Kwa hiyo nina hakika tutakwenda wote pamoja na tutaendelea kushirikiana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo ya nchi hayaletwi na mtu, yanaletwa na watu na ni wajibu wetu sisi wenyewe kushirikiana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. KABWE ZUBERI ZITTO:** Mwongozo wa Spika!

**NAIBU SPIKA:** Ndiyo!

**MHE. KABWE ZUBERI ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 55(3) na naomba nisome: “Hali kadhalika Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba Mwongozo wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema katika kikao cha siku hiyo kwa kumwomba Spika atoe ufafanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni na Taratibu za Bunge, na majibu ya Spika, yatakuwa kama yalivyoelezwa katika fasiri ya (2) ambayo iko juu ya fasiri hii”. Sasa, wakati Mheshimiwa Mzindakaya, Mbunge mzoefu, Mbunge ambaye amekaa Bungeni muda mrefu zaidi kuliko Wabunge wote, akizungumza na licha ya kwamba ametumia muda mrefu kujaribu kuisemea Serikali, lakini alikuwa anakunywa maji. Sasa, Je, suala hili linaruhusiwa Wabunge kuingia na maji ndani ya Bunge, kuingia na chupa za maji? Ahsante!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zitto, ahsante! Suala hili katika Kanuni zetu halitamki popote. Hajakosa wala hajakukosea! Halijatamkwa mahali popote. Pia, kwa

sababu anaumwa alipewa kibali. Lakini, haliko kwenye Kanuni. Vile vile na pipi nao hazimo kwenye Kanuni.

Waheshimiwa Wabunge, Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara Mheshimiwa Shellukindo, anaomba awatangazie wajumbe wake wakutane saa 5.00 katika chumba namba 432 ghorofa ya nne. Halafu, tunao *Boy Scouts* na *Girl Scouts* wetu wawili wasimame. Hawa ni *special guests* ndio maana nimewatambulisha. Wengine wote karibuni.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi asubuhi hii ya leo. Kwanza, naomba nianze kwa kuwapongeza Mawaziri wote wawili; Waziri Ngasongwa na Waziri Zakia H. Meghji, kwa kuwasilisha vizuri hoja zao katika Bajeti hii tunayoendelea nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kuipongeza timu yetu ya Taifa kwa ushindi wa goli moja dhidi ya Bukinafaso nyumbani kwao. Na hii sasa ni dalili kwamba ile hali ya Tanzania kuwa kichwa cha mwendawazimu, inaanza kupungua. Nashukuru sana!

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia kuwatakia kila lililo jema na rehema kwa Mwenyezi Mungu wale Watanzania wenzetu waliopata ajali kule Mkoani Singida kupitia Basi la Mohamed *Trans*. Wale ambao ni wagonjwa hadi sasa, wapate nafuu haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwangu mimi Bajeti hii ni nzuri. Ni nzuri kwa sababu inapunguza kwa kiasi fulani kutegemea wenzetu kutusaidia. Mambo yaliyoko katika Bajeti yana kila dalili kwamba sasa tunatakiwa tujifunge mikanda wenyewe, tuzalishe yanayotokana na sisi wenyewe. Katika hali hiyo, moja kwa moja naomba niunge mkono kwa asilimia 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nina ushauri mchache kwa Serikali. Ushauri wangu wa kwanza ni kuhusu suala la Elimu. Mimi nimefurahi katika vipaumbele vyetu, Wizara ya Elimu imepewa karibu asilimia 18 ya Bajeti yetu. Kwa kweli hili ni jambo zuri maana Dunia ya sasa ni ya Sayansi na Tekinolojia. Katika Sayansi na tekinolojia, Elimu inakuwa ndio msingi wa kila kitu. Kwa hiyo, napenda kuipongeza Serikali kwa kuipa kipaumbele kikubwa suala la Elimu. Lakini, naomba Wizara ya Elimu pamoja na kupewa pesa nyingi kidogo, ifanye jambo moja. Tusi-*concertrate* tu kujenga zile shule na mambo yanayoendana na hayo, tuangalie pia walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tuna tatizo la walimu. Mimi walimu wangu wa Tandahimba pale, nimeenda Newala, juzi nilikuwa shule ya Chang’ombe pale, wote wanalalamika kwamba mwalimu aliyeajiriwa mwaka jana na mwalimu aliyeajiriwa miaka kumi iliyopita, wote bado wako katika madaraja yale yale. Kwa nini? Huku ni kuwavunja moyo! Kama kweli tunataka kuendeleza Elimu yetu ni lazima tuhakikishe pia tunawapa motisha ya kutosha walimu wetu na motisha ni pamoja na kuwapandisha madaraja ikiwa ni pamoja na mishahara na posho zingine. Lakini pia, shuleni kule tuna

matatizo makubwa. Shule nyingi zina matatizo ya umeme, zina matatizo ya maji na mabweni pia. Bahati mbaya Mkoa wangu unaongoza kweli kwa idadi kubwa ya watoto wanaoacha shule kwa sababu wanapewa mimba. Mimi nadhani suluhisho ni kutusaidia tuwe na mabweni. Kwa hiyo, tuanze pole pole. Kwa kuwa mwaka huu ndio tunaiongea hii, angalau mwakani basi, tuanze pole pole Wilaya 40, Wilaya 40 tukijenga mabweni. Nafikiri tunaweza tukajaribu kuiboresha Elimu yetu kwa mapana na katika stahili inayofaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu wa pili ni kuhusu hii Bajeti. Mimi nimeisoma kwa umakini, nimeona karibu asilimia 70 yaBajeti hii inahusu manunuzi ama ya vifaa au huduma. Sasa, uzoefu nilionao na bahati nzuri niliwahi kufanya kazi ya kuwa *Procurement Officer* huko nyuma, uzoefu nilionao, Wakurugenzi wa Halmashauri pia Ma- *DAP* wametupa matatizo sana, wamekuwa wakichangia sana kutuletea hati chafu kwenye Wizara na kwenye Halmashauri zetu. Kwa sababu wao wakiamka wakitaka jambo lao, wanasema bwana eeh, mimi nataka hili leo lifanyike!

Ukimwambia bwana kuna *Ethical Codes* za kazi zetu hivyo, siyo hivi, lazima tufuate *procedure*, anakwambia bwana eeh mimi ndiye *DAP* hapa. Na kwa sababu Maafisa Ugavi wale *(Pocurement Offers)* wanaogopa kuachishwa kazi maana wanaweza wakajengewa hoja yoyote. Anaogopa kazi ataikosa, basi anamua kufanya hivyo hivyo anavyotaka mkubwa wake. Matokeo yake hati chafu na mambo yasiyoridhisha kuhusu utendaji wa fedha. Sasa rai yangu kwa Serikali: Tuanzishe *Derectorate of Procurement and Supplies* ili kuwapa nafasi angalau wawe *level* moja na Ma-*DAP* wale. Kwa sababu leo akisema kitu ambacho ni *contrary* na utaratibu, basi atamkatalia kwa sababu hawa wote si wako kwenye *rank* moja, wewe Mkurugenzi wa Utawala, mimi Mkurugenzi wa Ununuzi na vifaa. Lazima tufuate *Ethical Code*, hakutakuwa na hali iliyopo sasa. Mimi nachelea sana kwa kuacha hivi ilivyo, huko mbele tutaendelea kuleta matatizo ya matumizi mabaya ya fedha za Umma kwa sababu tu kuna baadhi ya Ma-*DAP* wetu au Wakurugenzi wetu siyo waadilifu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina suala la barabara. Kwanza nataka niipongeze Serikali. Mimi kwa mara ya kwanza nimepata matumaini kweli tarehe 1. Tarehe 1 nikiwa kwenye Kamati pale niliopata habari kwamba Mkamu wa Rais, Mheshimiwa Dr. Shein anafanya ziara Mkoani Mtwara. Ilibidi niondoke saa 8 kupitia barabara ya Kibiti – Lindi. Kwa kweli nilifurahi kweli maana nilipofika kuanzia Nangurukuru mpaka Mandawa ni barabara ya lami (*Tarmac Road)*. Nimefika Mchinga, nakuta kuna lami pale mpaka Mnazi Mmoja, Kilomita karibu 60.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, jana ndugu yangu Mheshimiwa Susan Lyimo alipokuwa anasema Serikali haifanyi lolote, nikasema hivi jamaa hafanyi utafiti wa kutosha! Kwa hiyo, nataka niipongeze Serikali kwa juhudi zinazofanywa. Lakini, pia nataka niiombe Serikali hiyo hiyo. Juzi tumeambiwa hapa jana kulikuwa na *opening* ya *tender*. Basi, mshindi wa kwanza na wa pili wale wagawane kwenye ile kilomita 60 ya Ndundu – Somanga ili ifanywe haraka. Unajua, hata Mheshimiwa Susana alikuwa anasema vile kwa sababu tu, kama kuna tatizo mahali na pale alipigwa ndugu yangu

Mheshimiwa Jecha, nilimwona jicho limevimba, jekundu kutokana na eneo lile. Sasa, akiona pale anadhani na sehemu zingine ziko hivyo hivyo. Kwa hiyo, mimi ninaomba Serikali sasa ijinusuru kwa makusudi, watu hao walioomba wapewe watu wawili pale wafanye haraka, angalau mwaka kesho kutwa barabara yote iweze kupitika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili hili la Barabara, Mkoa wa Mtwara una matatizo makubwa. Hauunganiki kwa barabara ya lami hata moja. Mkoa wa Mtwara unaunganika kutoka Mtwara, Mtwara Vijijini, Tandahimba, Newala na Masasi. Lakini, barabara hiyo inayounganisha Mkoa mzima haina lami na hali ni mbaya kweli kweli. Mimi naiomba Serikali ijinusuru kwa makusudi, Bajeti hii tumechelewa, lakini mwakani tuanze sasa ili kuunganisha Mkoa. Kwa sababu sehemu ile ya lami ni kilomita 40 tu kutoka pale Mtwara mpaka pale inapokutana na Lindi. Sehemu nyingine yote haina lami na ni vigumu kweli hata unapokuwa kwenye ziara ya viongozi wakubwa, ukishaingia kwenye maeneo hayo ni dhiki na matatizo makubwa. Naiomba sana Serikali itambue barabara ile ya kutoka Mtwara – Tandahimba – Newala – Masasi, kilomita 200 tu siyo nyingi, ziweze kupitika kwa lami ndugu zangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu mwingine ni kuhusu suala la *Export Credit Guarantee Scheme*. Kama kumbukumbu zangu ziko sahihi, maana mwaka 2003 nilikuwa bado sijawa Mbunge, lakini nilikuwa nafuatilia fuatilia kidogo. Lakini, kama kumbukumbu zangu zilikuwa sahihi, Bunge hili lilipitisha hii *Export Credit Guarantee Scheme* na nia ilikuwa ku-*promote trade* ya nchi yetu.

Lakini mimi naona Benki Kuu wana urasimu kweli kweli na naamini waliopata hii ni wachache. Labda ndugu yangu Mrema pale kwa sababu rafiki yangu tuko kwenye Kamati moja aliwahi kunidokeza kidogo kwamba kwenye maua kule aliwahi kupata kidogo, lakini jamani kuna wazalishaji wa mazao ya Kitanzania na kama inavyofahamika kwamba mchango mkubwa wa uchumi nchi hii unategemea mazao ya kilimo. Sasa mwaka jana hapa tulikuwa tunapiga kelele hapa, korosho watu hawanunui, Wahindi hivi na hivi. Hivi kwa nini wale wenye viwanda vilivyoko kule Kusini vya korosho wasipewe hii *Guarantee Scheme* wakanunua korosho zile tukaepukana na hii? (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwamba Serikali imeanza mkakati wa kuhakikisha kuwa vyama vyetu vya Ushirika vinaweza kununua korosho na hata jana niliongea na rafiki yangu na kaka yangu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, amenihakikishia hilo linaenda kwa *speed* kubwa. Lakini pia nilikuwa naomba hii *Export Credit Guarantee Scheme* tuwasaidie wale wenye viwanda. Kwanza walionunua viwanda wenyewe wale wazalendo watupu, kwa nini wasipewe hii tukamaliza haya matatizo na isiwe kwa korosho tu hata kwa pamba, kwa tumbaku na kadhalika, na kadhalika, na kadhalika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine mwaka jana tulipitisha hapa suala la *Export Levy* tukasema Serikali ipewe tatu na nusu na Halmashauri sita na nusu. Sasa mimi hii sioni Serikali inapeleka ile sita na nusu kule kwenye Halmashauri na korosho zile hela zile zimetokana na korosho zao. Sasa kuna ugumu gani wa kuwapelekea kule, tuamue kuwapeleka na ningeshauri *TRA* waweke kwenye *deposit account* muda

unapoisha wapeleke *straight* kwenye Halmashauri kule na zile za Serikali ziende Serikalini, tusizue matatizo *un necessarily. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni la watendaji wetu wa Kata na Madiwani. Ndugu zangu watu hawa wana mchango mkubwa sana wa utendaji bora kule vijijini tuliko. Lakini wana matatizo, hawana usafiri, posho za kubabaisha na mambo ya aina hii mengi. Mimi nadhani wakati umefika sasa tuwatambue watendaji wetu wa Kata na Madiwani tuwape posho ya kutosha tuwakopeshe hata usafiri ambao watakuwa wanalipa pole pole. *(Makofi)*

Kule ukimpata Mtendaji Kata mzuri, *DC* anapunguziwa kazi. Ukimpata Diwani mzuri hata wewe unapogombea Ubunge, ukimwambia tu bwana tushirikiane katika hili, umeshapata kura za Kata zile. Sasa kwa nini tusiwasaidie hawa, tuondoe matatizo yasiyo ya lazima ya kukutana na ugumu wa utendaji wa kazi zao na maisha usio na lazima? Lazima tujibane na kama kweli tunataka utawala bora kwa maana halisi ya utawala bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo jambo lingine la Chuo cha Mipango na hii nia yangu kabisa kwa mtani wangu Mheshimiwa Ngasongwa, Chuo kile hujakipa stahili inayotakiwa. Mimi ninavyoamini tukitengeneza watu wazuri wenye uwezo pale, watatufanyia mambo mazuri kweli ya kubuni uchumi ulio bora wa nchi yetu na uchumi utapanda. Maana hawa tunawategemea waende kule wilayani na vijijini wakaibue mipango ya maendeleo. Lakini siku moja nilitembelea pale, nimekuta watu wako nje, wamekaa nje, madirishani, ni nini? Eti wanafuatilia *lecture* anayotoa mwalimu kule kwamba wanafunzi wako wengi ndani, wengine wako nje, wanasikiliza *lecture* wakiwa nje, katika hali hii hatuwezi kwenda. Lazima tuwatengenezee *seminar rooms* pale, *theatres* na mambo mengine. Walimu wale wapewe nyumba na tuwa-*promote* uwape motisha wa aina fulani ili wazalishe watu walio na uwezo watusaidie kujenga uchumi imara wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo dogo lingine ningependa nishauri, lenyewe ni Mkoa wa Dar es Salaam. Mimi namhurumia kweli Mkuu wa Wilaya ya Temeke na Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni. Unakuwa Mkuu wa Wilaya katika eneo kubwa hili lenye watu wengi namna ile hivi unaongozaje? Utawala bora huo unakufikiaje? Mimi nadhani wakati umefika sasa Wilaya hizi tuzigawanye, Temeke tuipe Mbagala Wilaya nyingine, Kinondoni tuwape Kawe kule Wilaya nyingine, tuwapunguzie ugumu wa kuwaongoza Watanzania wanaoishi Dar es Salaam. *(Makofi)*

Katika hali ya kawaida huwezi kuwa Mkuu wa Wilaya ya Temeke na *population density* ya namna ile ukasema utawatumikia vilivyo wananchi wale, siyo rahisi. Hali kadhalika Kinondoni *population density* iliyoko Kinondoni ile mimi sielewi. Tena mimi nawapongeza hawa watu, maana hata sijui wanafanyafanyaje kwa kweli kufanya *administration* iliyo sahihi. Lakini najua wana wakati mgumu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ambalo ningependa kuchangia ni kuhusu yale mambo yaliyojitokeza katika bajeti mwaka jana. Mambo mengi ya afya, maji.

Tuliahidiwa mambo mengi sana hapa. Hatuku-*impliment* kama inavyotakiwa. Kuna mahali tumewaambia wananchi na labda niseme hapa tu kwa mfano, ingawaje mimi ni Mwenyekiti wa Bodi ya Maji ya Makonde isingekuwa vizuri niseme hapa. Lakini siyo vibaya nadhani nikisema, kwanza, katika Bunge hili tulisema tunapitisha milioni 800 kwa ajili ya Mradi wa Maji wa Makonde na amekuja Rais kule amesema Tandahimba, amesema Newala, amesema Masasi. Leo hadi sasa milioni 800 zile hazijafika kule, nilikuwa nanong'ona na Waziri wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Lakini kuna tatizo moja pia kwamba kuna bandari ya kutoa mizigo kutoka nje kwa maana *main key,* na *light key* pale *Malindi Wharf,* kuna bandari ambayo huwa inapakia mizigo kutoka Zanzibar. Kule Zanzibar pia kuna wafanya biashara ambao masoko yao makubwa yako huku Tanzania Bara. Kama tunavyojua Zanzibar ni Kisiwa kwa hiyo shughuli zake zote inachotegemea ni uchumi wa biashara tu, na siku labda utalii, hatuna madini, ardhi hakuna ya kutosha, ya kututosheleza sisi wenyewe zaidi ya kwamba sisi kwa kiasi kikubwa sana kule Zanzibar tunategemea bidhaa kutoka Bara. Kwa mfano, aina ya mboga mboga zetu zote kuanzia nyanya, vitunguu na kila kitu kinatoka huku.

Kwa hiyo, ili mtu wa Zanzibar apate hela ya kununulia vitu hivyo ni lazima afanye biashara na biashara yenyewe ni *importation* waagize, watoe wapeleke na hivi. Bahari nzuri *TRA* hii hii ndiyo iliyokuwepo Zanzibar, Zanzibar na yenyewe pia kuna *TRA* ambao mfumo wa kulipa kodi ni kama unaotumika Bara. Tatizo linakuwa sasa bidhaa na suala hili tumelizungumza kila mara. Nakumbuka mwaka jana pia nilizungumzia suala hili. Lakini bado tatizo lipo.

Tunapata shida sana, wanapata shida sana wafanyabiashara wa Zanzibar wanapoleta mizigo yao kupitia bandari ya Dar es Salaam kufika Dar es Salaam pale *Malindi Wharf* au *Baggage Room,* mzigo ambao tayari umeshalipiwa ushuru Zanzibar kwa mtandao huu unaoitwa *Esquda Plaus Plus* ambao umekubalika kabisa na *TRA* Tanzania nzima. Ukifika Dar es Salaam bado anaambiwa mtu yule weka mzigo! Wiki mbili, wiki tatu, eti kwa ajili ya uchunguzi zaidi! wakati ana nyaraka zote zilizokamilika ambazo zina kila kitu na ushahidi upo. Hiki kitu kwa kweli kinatuvunja moyo sana kule Zanzibar, bila ya biashara Zanzibar hakuna shughuli.

Kwa sababu umefikia wakati sasa hivi bidhaa za Zanzibar hazinunuliki, kwa vile ni ghali zaidi kuliko Dar es Salaam, matokeo yake vijana pale Zanzibar wanakuwa hawana kazi. Wanakaa chini ya miti tu na kuzungumza kutwa nzima mambo ya siasa tu, hawana kazi yoyote na ndiyo mtaona kwamba sasa hivi Zanzibar vijana wengi sana wanajishughulisha na mambo ya siasa kwa kuwa hawana kitu cha kufanya.

Muda wote wako kwenye miti tu. Bila ya kufanya biashara hakuna jinsi na njia ya kuweza kufanya biashara soko la Zanzibar haliko. Zanzibar kutelemsha kontena moja tu la kibiriti litakaa miaka 10 halijamalizika. Lakini pale ni njia ya kuweza kuvitoa

kuvileta huku na huku njia ya kupitisha ni Dar es Salaam bandarini na bandarini wanatumia *document* zote halali, wanalipa ushuru halali, kila kitu kinakwenda sawa sawa.

Hiki kitu kinashangaza kwamba kuifikisha mizigo bandarini Dar es Salaam wanapata shida sana. Sasa ikiwa kuna mpangilio mzuri wa kutoa bandarini mizigo ambayo inatoka nje, kwa njia rahisi basi waliangalie na bidhaa zinazotoka Zanzibar ili kuinusuru au kuwanusuru watu wa Zanzibar waweze kuhimili maisha yao. *(Makofi)*

Hilo nafikiri nimelizungumza vya kutosha. Sasa nakuja kwenye suala hili la mafuta. Mimi nafikiri suala la kupandisha kodi ya mafuta kwa maoni yangu, mimi sioni kama ni tatizo. Tatizo letu sisi Tanzania si mafuta, tatizo ni barabara. Tatizo linalowakabili Watanzania kuingia gharama zaidi ni barabara. Nitatoa mfano mmoja , pale Dar es Salaam wakati wa *rush hours* kutoka Kariakoo kwenda Magomeni hasa kuanzia saa 10 - 12 *Taxi Driver* anaweza akakataa au akakuchaji bei ambayo wewe mwenyewe utakataa kwenda nayo. Si kwa sababu ya masafa, ni kwa sababu ya barabara. Lakini kama kungekuwa na barabara nzuri na watu wanaweza kwenda *free* na gari zikaenda zaidi, basi bei yenyewe ya usafiri itapungua kwa sababu kila mmoja atakwenda kwa njia iliyo nafuu.

Sasa hivi Tanzania mtu anaweza akapandisha bei ya nauli ya mabasi kwa kufika mji fulani au mkoa fulani ni tabu kwa ajili ya barabara si kwa ajili ya mafuta kwa ajili ya barabara, kwa sababu akiwa na barabara mbovu atatatumia mafuta mengi, atatumia na vipuri vingi vya kuripea gari. *(Makofi)*

Lakini kama kutakuwa na njia nzuri basi magari yatafika kwa wingi na kwa kuwa magari yatafika kwa wingi, hao madereva na wenye vyombo vya magari wataweza ku-*balance* faida kwa sababu watajua mimi nikikataa nikiweka bei ghali, kuna mwenzangu atafanya hivyo. Mimi nitakupeni mfano mmoja kule Zanzibar kuna usafiri wa boti kutoka Zanzibar kuja Dar es Salaam, kuna boti ambazo zinaondoka moja kila baada ya saa nne, wanatoza shilingi 14,500/= lakini kuna boti mbili zinaondoka wakati mmoja saa 10 wao wanatoza shilingi 10,000/=, masafa ni yale yale. Sababu ni kwamba wanakwenda pamoja.

Sasa hapa tatizo ni kwamba ikiwa kuna uwezekano wa kuwa na barabara nzuri, magari yanakwenda kwa wingi, basi usumbufu huu, nauli kupanda utapungua tu, kwa sababu magari yatakwenda moja kwa moja na kuna urahisi wa kwenda. Kwa hiyo, tatizo letu Tanzania sisi ni barabara na kama Serikali imezidisha pesa hizi, kodi hii kwa ajili ya kutengeneza barabara zetu ni vizuri sana. Lakini tu cha msingi ni kwamba ihakikishe kwamba hela zote zinazopatikana katika kodi ya mafuta zinatengeneza barabara. Tatizo letu Tanzania ni barabara, tukiweza hilo na katika bajeti ijayo Mheshimiwa Waziri hapa akija kutueleza kajenga kilomita ngapi kusitokee tena mabishano ya jana, Serikali haikujenga kilomita moja wala hivi! Nafikiri akitoa maelezo itakuwa ni vizuri zaidi. *(Fedha)*

Mheshimiwa Spika, fedha hizi zote zisimamiwe vizuri, na zijenge barabara zetu, magari yafike kila Mkoa kwa urahisi, basi kwa kufanya hivyo, kila mkulima ataweza

kusafirisha bidhaa zake kwa urahisi zaidi na kutakuwa na msongamano wa magari kwenda kila mahali. Utaratibu huu utakuwa mzuri zaidi kuliko kulilia suala ambalo halitatusaidia. Kwa kweli mimi nina kitu kimoja ambacho nilitaka kuwafahamisha, nina mfano mmoja mzuri sana. Kwa kawaida binadamu yeyote kama akitaka kutengeneza au kujenga kitu fulani, ni lazima kuna mambo fulani ajinyime ili aweze kufanikisha kusudio lake.

Hivyo, sisi au Serikali ilivyofanya hivi kubana kidogo huku ili kutengeneza barabara ni jambo zuri sana. Mimi nitakupeni mfano mmoja kule kwetu Zanzibar. Kule Awamu ya Kwanza mwaka 1965 baada tu ya Mapinduzi, Rais wetu wa Kwanza, Mheshimiwa Karume alisema tunataka kujenga nchi yetu na kama tunataka kujenga nchi yetu nchi hii haitajengwa na mtu mwingine ni sisi wenyewe. Kwa hiyo, fedha yetu tuliyokuwa nayo itabidi tujinyime kile kilichokuwa si cha muhimu, vitu vyote vya anasa tutakata hatuagizi nje, pesa zetu tutaagiza zana za kujengea.

Kwa kipindi cha miaka minane mnavyoiona ile Zanzibar kuna majumba ya maendeleo yamejengwa kila mahali nchi ile. Kuna barabara zimejengwa pale toka miaka hiyo mpaka leo hazijajaa, kama Michenzani ukishafika Zanzibar, ni kwa sababu mtu kajinyima huku lakini anakusudia kufanya kitu. Kwa hiyo, Serikali kuanza kujinyima au kuanza kujibana kwenye suala la mafuta siyo jambo baya kwa sababu nia yao nzuri, ni kwamba wanataka kujenga barabara kwa ajili ya kutengeneza miundombinu yetu ya Tanzania kuwe na fursa ya kuweza kufika kila mkoa kila wakati, iwe mvua iwe jua wakulima wetu mikoani waweze kusafirisha bidhaa zao kwa wakati unaohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba tena kuunga mkono hoja hii. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Bajeti hii ya Serikali na nimpongeze Waziri wa Mipango na Waziri wa Fedha kwa bajeti nzuri ambayo imewasilishwa mbele yetu. Lakini kabla sijaanza kuchangia, basi nichukue nafasi hii kuwapa pole wale wenzetu wa Singida ambao wamepatwa na matatizo ya ajali ya basi la *Mohamed Trans* na ni jana tu wale wahanga walizikwa na nawapa pole sana jamaa zao ambao wamepotelewa na ndugu zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na Serikali kwamba kutokana na mapato madogo ya ndani ya nchi yetu ni vizuri sasa kuweka kipaumbele na kuangalia vipaumbele kwa makini sana katika sekta mbalimbali zinazohusu wananchi walio wengi. Niendelee kuipongeza Serikali kwa kuangalia kwa kupanga bajeti kwa asilimia 18 kwa Wizara ya Elimu. Wizara ya Elimu kwa mwaka jana sisi kama Viongozi wa wananchi tulifanya kazi kubwa sana kuwahamasisha wananchi wajenge shule za sekondari katika maeneo ya Kata na wananchi waliitikia wito huo na shule zimejengwa nyingi lakini kuna matatizo makubwa katika shule hizo zilizojengwa. Walimu hawatoshi, vifaa hakuna, watoto wa kike wanatembea mwendo mrefu na hakuna *Hostel* na maeneo mengine ukipita wananchi wanasema kwamba, tunaamini kwamba watoto wetu wa kike wamepata nafasi ya kuingia kidato cha kwanza lakini idadi ya watakaomaliza kidato cha nne

kutokana na umbali wa kufuata shule mbali, itakuwa ndogo mno. Kwa sababu wengi wanadanganyika njiani, wengi wanapata mimba, wengi wanapata matatizo mbalimbali. Kwa namna hiyo wanashindwa kumaliza kidato cha nne.

Kwa hiyo, naipongeza sana Serikali kwamba wameiona hiyo hali na wakaipa Wizara ya Elimu asilimia 18. Ninaamini Wabunge wenzangu tutakapokwenda katika majimbo yetu tutakuwa na la kusema kwamba sasa shida katika Wizara ya Elimu itapungua kwa mwaka ujao wa fedha.

Naomba sasa nichangie katika hotuba ya Waziri wa Mipango katika Jedwali Na. 1(b) ambalo nimeona pato la Taifa katika Sekta ya Kilimo ilivyopungua kutoka asilimia 5.1 hadi asilimia 4.1. Maelezo wanasema imetokana na kiangazi. Lakini pamoja na kukubaliana na hilo bado naamini kabisa kwamba sekta ya kilimo haijatiliwa mkazo inavyotakiwa. Sisi kama Wabunge tunatoka maeneo ya vijijini, sijui ni mikoa mingapi ambayo wanalima kufuata kilimo cha kisasa cha kufuata kabisa utaalamu na ni mikoa mingapi wataalamu wale wa ugani wanatembelea kila shamba la mwanakijiji.

Mimi nimelima mwaka huu eka 10 lakini hata siku moja sikuwahi kutembelewa na Afisa Ugani, hata siku moja na wala simjui sura. Lakini kilimo asilimia 80 ya Watanzania ni wakulima na sisi Dodoma tumehamasishwa sana na Mkuu wa Mkoa kwamba tulime zabibu na eka 1,000 zimetengwa kwa ajili ya kilimo cha zabibu, lakini Maafisa Ugani wako wapi? Inawezekana kweli hawatoshi? Inawezekana hawajui wajibu wao? Mimi sielewi. Lakini naiomba Serikali kwamba waangalie sasa namna ya kuwasaidia wakulima, pamoja na kwamba tunalima zabibu, tuna *varieties* tatu tu. Hatuna *variety* zingine na tuna soko kubwa sana la mizabibu. Lakini Maofisa Ugani tulionao hawana uwezo wa kutupa *variety* za aina zingine, hawana uwezo wa kuwashauri wakulima. Wakulima tangu waanze kulima zabibu katika Mkoa wa Dodoma wanalima hivyo hivyo miaka nenda rudi, wana-*prone* zabibu kama walivyo-*prone* wazazi wa miaka 47 iliyopita. Hawana wataalam!

Maafisa Ugani tulionao inawezekana hawana utalaamu pia wa kujua kwamba mabadiliko ya hali ya hewa yanapotokea wawashauri nini wakulima wa zabibu. Nampongeza tena Mkuu wetu wa Mkoa kwa sababu Maafisa Ugani wa Dodoma amewapeleka shule. Jana alikuwa ananiambia kwamba ametoa shilingi milioni nne kuwafundisha Maafisa Ugani wa Mkoa wa Dodoma. Lakini ni Mikoa mingapi ambayo imefanya hivyo? Niiombe Serikali sasa kama ni kweli tunataka kusogea katika sekta ya kilimo basi tuangalie namna ya kuwasaidia wananchi na hasa Maafisa Ugani.

Niliposoma kwenye bajeti pia nimeona kwamba kilimo cha umwagiliaji kimeongezeka kwa hekta 14 tu. Nchi hii ni kubwa mno na tuna mito mingi inayofaa sana kwa kilimo cha umwagiliaji. Na tumebarikiwa kuwa na maeneo mazuri ya kuweza kulima kilimo cha umwagiliaji, lakini kama kweli kwa mwaka mzima miezi 12 kilimo cha umwagiliaji kinaongezeka kwa hekta 14 tu ina maana kwamba hatujatilia maanani kilimo cha umwagiliaji. Katika bajeti haikuonyesha kwamba mwaka huu Serikali inategemea kuongeza kilimo cha umwagiliaji kwa hekta ngapi. Sisi Kondoa hapa tuna mto mzuri tu ambao unaweza ukafanya kazi nzuri sana ya kilimo cha umwagiliaji.

Lakini katika bajeti sikuona kama kuna pesa yoyote iliyotengwa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji katika maeneo mbalimbali. Tukumbuke katika Mto Rufiji zamani hizo kulianzishwa kilimo cha umwagiliaji katika Mto Rufiji na ukapewa jina la RUBADA. Sasa sijui kilimo kile kinaendelea, sijui ndiyo kimeishia, lakini kuna haja kubwa ya Serikali kuangalia hali ya kilimo cha umwagiliaji. Nafikiri kitatukomboa kwa namna nyingine na kitatusaidia kwa namna nyingine pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee tena kuhusu *fast trucking* katika bandari. Mimi nimechanganyikiwa. Wabunge tunapoingia tumedhaminiwa sana na wananchi na tumeaminiwa sana na wananchi. Lakini tunapoingia Bungeni hapa tunapekuliwa, mikoba yetu inapita kwenye mashine, na sisi wenyewe tunapita kuangaliwa kama tumeingia na silaha. Lakini mfanyabiashara anaaminiwa kwa mizigo anayoingiza nchini moja kwa moja bila kukaguliwa ( *fast trucking),* kuna nini katika *fast trucking*? Sisemi kuna rushwa, lakini naomba kuitahadharisha Serikali kuwa anayeingiza mizigo hiyo ni binadamu asiaminike kiasi hicho! Tutaruhusu rushwa! Kwa sababu kila mmoja atapenda mizigo yake isikaguliwe na naamini kabisa kabisa bidhaa itakayoletwa mwanzo watafanya vizuri, lakini mbele ya safari huko mtu anaweza akachanganya bidhaa katika kontena lake na kwenye *documents* zisionyeshe kwamba kuna bidhaa tofauti katika kontena. Naomba hili kwa kweli Mheshimiwa Waziri wa Fedha uliangalie kwa jicho lingine. Tunaweza tukaingiziwa silaha pasipo kujua, kwa sababu mizigo haitakaguliwa, sasa atakayejua kwamba silaha imebebwa kwenye kontena ni nani? *(Makofi)*

Muda unanishangaza unavyokwenda.Nichangie kuhusu barabara ya Iringa-Dodoma-Babati. Mwaka jana tuliahidiwa kwamba barabara hii ingekuwa katika mchakato wa kujengwa. Lakini mwaka huu Serikali imenyamaza kimya kuhusu barabara ya Babati-Dodoma-Iringa. Tungeomba maelezo wananchi wa Dodoma kwa sababu tulishakuwa na imani kwamba Serikali itajenga barabara hiyo.Nizungumzie pia kuhusu uwanja wa ndege wa Dodoma. Wananchi wa Dodoma wanaoishi katika eneo la Msalato walishaambiwa kwamba eneo lao litajengwa uwanja wa ndege. Sasa hivi ni kama miaka minne, mitano imepita, hawafanyi maendeleo ya aina yoyote, wanasubiri kulipwa fidia. Lakini hiyo fidia ya milioni tangu waahidiwe mpaka leo hawajalipwa, hawafanyi maendeleo yoyote, mtu hawezi kujenga nyumba, mtu hawezi kufanya kitu cha maendeleo, kwa sababu anajua mahali pale siyo pake, patajengwa uwanja wa ndege. Lakini watu hawa hawajalipwa. Naomba Serikali iwalipe wale watu na watafute pa kuishi ili wakafanye maendeleo katika maeneo hayo wanayokwenda kuishi.

Nizungumzie sasa kuhusu udhibiti wa fedha za Serikali. Mimi nipo katika Kamati ya *PAC,* ninaona jinsi pesa za Serikali zinavyotumika. Sasa tumeombwa kufunga mkanda, na mimi nakubali kufunga mkanda na nakubali kuwashawishi wananchi wangu kufunga mkanda. Lakini je, watumishi wa Serikali wameandaliwaje kufunga mkanda. Matumizi katika manunuzi ni makubwa mno na pesa nyingi zinapotea katika manunuzi ya Serikali na zaidi ya hapo wataalamu wengi wanakimbia kutokana na mshahara mdogo ambao Serikali inatoa kwa Wakaguzi wa Mahesabu na Wahasibu pia. Kwa hiyo, wanasomeshwa, mwisho wanakimbia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Serikali ionyeshe namna itakavyoweza kukaa na kuhakikisha kwamba wahasibu na wakaguzi wa mahesabu hawaachi kazi katika Serikali.

Wengi wanaacha kazi, wengi wanaiba, wengine kesi zinakwenda Mahakamani wanashinda kesi na kesi nyingi za Serikali zinazopelekwa Mahakamani nyingi wanaokwenda kule wanashinda.

Sasa ni wakati mzuri kwa wananchi pamoja na kwamba tunafunga mkanda tufunge sote na tuhakikishe kwamba bajeti hiyo ndogo kwa hicho kidogo tulichonacho tunakitumia vizuri kwa wote na kinatumika vizuri kwa faida ya wote. Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee sasa kuhusu mafuta ya taa. Jamani asilimia kubwa ya wananchi wanatumia mafuta ya taa na hata sisi tunapokwenda vijijini kule taa na vibatari tunavyotumia kule vinatumia mafuta ya taa hata katika ziara wengine tunalala vijijini huko huko ni mafuta ya taa ndiyo yanayotumika. Ninaomba kama kuna uwezekano basi ushuru ulioongezwa katika mafuta ya taa Serikali iangalie namna ya kuwasaidia hawa watu, wanawake wanahangaika na safari hii wengi watauawa kwa ajili ya macho mekundu kwa sababu moto ndiyo utakuwa taa, usiku ni moto na mchana ni moto. Sasa basi, tuangalie namna ya kuwasaidia wananchi kwamba je, kuna ulazima wa kupandisha bei ya mafuta ya taa? Tuangalie mahali pengine ambapo tunaweza tukapunguza na tukaongeza ushuru huo na wananchi wakapunguziwa ushuru katika mafuta ya taa. Mafuta ya taa yanawahusu watu wengi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nichangie kuhusu...!

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, sasa namwita Mheshimiwa James Mnamka Wanyancha na kisha Mheshimiwa Pindi Hazara Chana na Mheshimiwa Balozi Hamis Sued Kagasheki awe tayari.

**MHE. DR. JAMES MNANKA WANYANCHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijasema lolote napenda sana kuwapongeza Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Zakia Hamdani Meghji na Manaibu wake kwa hotuba nzuri waliyoitoa hapa Bungeni. Napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Dr. Juma Alifa Ngasongwa , Waziri wa Mipango na Naibu wake na wafanyakazi wote wa Wizara yake kwa hotuba nzuri waliyoitoa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nichukue nafasi hii ya kipekee kuipongeza Serikali ya Awamu ya Nne. Serikali ya Awamu ya Nne imeingia wakati ilipokumbana na matatizo mengi, kwanza, kulikuwa na ukame, njaa na mataizo ya umeme, homa ya bonde la ufa pia.

Lakini limeweza kuhakikisha kwamba uchumi umekuwa kwa 6.2%, siyo nchi nyingi zimeweza kufikia hapo lakini mvua ingenyesha na umeme usingekuwa na matatizo mimi naona kama ingeweza kufikia 10. Kwa hiyo, jamani hicho ni kigezo cha kuifanya Serikali hii tuipongeze.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kwa kuhamasisha wananchi kwa michango na kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa sekondari, sekondari zaidi ya 1000 zimejengwa. Hii ni rekodi ambayo haijawahi kutokea, ni lazima tuipongeze hii Serikali hiki si kitu kidogo na watoto wetu sasa wanakwenda shule na elimu ndiyo itakayotukomboa Watanzania, hata huko Japan na kwingineko kilichowafanya waendelee ni elimu, kwa kweli mimi nawapongeza sana Serikali ya Awamu ya Nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile makusanyo ya ndani yamevuka kiwango na hicho ndicho kigezo ambacho tunataka kuona ili kuipima Serikali siyo mambo tu ya kuandika magazeti bali tunatumia vigezo, utalaam na sayansi katika kuipima Serikali. Sasa Serikali imefanya kazi kubwa namna hiyo ni vizuri tukaipongeza jamani.

Vilevile hata deni la ndani lilipungua kutoka *USD billion* 9.4 kwenda *billion* 7.3, kwa hiyo, hayo ni mafanikio makubwa kwa taifa kwa sababu unapopunguza deni ndivyo unavyozidi kuimarisha uchumi wako.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu hizo mimi napenda kuunga mkono hoja hii mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo napenda kusema machache, kwanza, napenda Watanzania watambue kwamba uamuzi wa Serikali kupandisha ushuru wa petroli na dizeli ni uamuzi ambao ulichukuliwa baada ya kutafakari sana. Mwaka huu tumekuwa na mvua za *Elnino,* barabara zimeharibika ,sasa ndugu zetu tusipozitengeneza si ndiyo tumejimaliza?

Kwa hiyo, hizi pesa za ushuru ni kwamba Serikali itengeneze hizo barabara na ziweze kupitika. Hivyo, ndugu zangu wananchi wa Tanzania tunaomba sana tuipe

ushirikiano Serikali yetu kwa hili, tusiambiwe kwamba tunataka kuandamana eti kupinga bei, sasa tutoe wapi hela na nani atupe hela ya kutengeneza barabara zetu? Ni lazima tujifunge mkanda sisi wenyewe hakuna mtu yuko pale atujengee barabara sisi na kutupa pesa wakati sisi tunakataa kuchangia na kujifunga mkanda?

Kuhusu ada ya leseni nina ushauri ufuatao, kwamba ada ya leseni, magari mengi yanayotumika kama *taxi,* mengi yanaanzia *CC* 1500 – 2000 na dereva wa *taxi* anachomletea mwenye gari ni shilingi 10,000/=. Ukiwauliza *Tax Drivers* wengi kwamba unampelekea nini bosi wako atakwambia ni shilingi 10,000/= na ile gari inafanya kazi kwa siku sita. Kwa hiyo, kwa mwezi anapata kama shilingi 210,000/= kama gari haikuharibika.

Sasa tukichukua tukaupiga ule ushuru mpaka 230,000/= tutakuwa tumechukua pato la mwezi mzima la huyu mwenye gari ambaye ni mwananchi. Kwa hiyo, madhara yatakuwa ni magumu sana kwake.

Vilevile ukichukulia kwamba hizi gari zinatumika na wafanyakazi wa kawaida ambao mshahara wao ni kama 200,000/= kwa hiyo ukiangalia tukipiga ada ya shilingi 230,000/= tutakuwa tumemchukulia huyu mfanyakazi mshahara wa mwezi mzima.

Mimi nasema kwamba magari ya *CC* 1500-2000 ushuru uwe ni shilingi 80,000/=, naomba Serikali iwafikirie hao watu ili waweze kufika kazini mapema na wengine wenye mifugo waweze kuchukulia majani hizo gari zao, ndiyo hivyo tunavyoishi.

Kuhusu kudhibiti matumizi ya fedha, ndugu yangu hata ukiwa tajiri kiasi gani kama unatumia hela yako kiasi gani huwezi kuendelea utaona tu mtu anafilisika. Kama ulikuwa unajua kudhibiti hela ukabadilika sasa ukaanza kuzitumia vibaya utakuta tu mtu huyu anafilisika. Jamani kuonywa kumetosha, watu wanaonywa kila siku kwamba usitumie hela vibaya na mtu anaiba hela unamuonya kwamba usitumie hela vibaya? Sheria ifuate mkondo wake na kwamba mtu yeyote akiiba basi achukuliwe hatua ili tuweze kukomesha hili. Taifa haliwezi kwenda kwa kuonya watu, kila siku mtu anaonywa, leo kesho anakwenda kuiba hela halafu ukaguzi usiwe miaka miwili msituletee mahesabu ya miaka miwili huyu mtu si ajabu alishahama au alishakufa na hela ziliibiwa, tunataka miezi sita. Sasa hivi kuna kompyuta, kwa nini miaka miwili itumike? Miezi sita utampata huyu mtu na atachukuliwa hatua, atakuwa mfano kwa wengine.

Sasa naomba tuangalie kitabu hiki cha hotuba ya Waziri wa Mipango ukurasa wa 96 kielelezo Na. 1. Ukiangalia sasa hivi mapato yetu na mauzo ya nje yanatokana na dhahabu, dhahabu ni kitu ambacho huja kwisha. Ukienda kwenye migodi mimi nilikuwa kwenye Kamati ya Uwekezaji tuliitembelea anakwambia miaka 15 au 12, sasa hali hii ni lazima tuijue kwamba ipo na tutafute vyanzo vingine vya kuziba pengo hili ama sivyo tutakuja kujikuta katika hali mbaya sana siku zijazo na vyanzo hivi mimi ninavyoona kwanza kabisa kilimo ni chanzo namba moja .

Utalii umepanda njoo uone ndege za *KLM* zilivyojaa, hata *Air Ways* watu wanashuka, *Emirates, British Airways* na kadhalika. Tukiweka hoteli nzuri kwenye hifadhi zetu na mijini watalii watakuja sana na uzuri tuna amani ya kutosha nayo hiyo inaweza kutusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ni bandari. Bandari ya Tanzania kwa kweli Mungu ametusaidia sana, wewe fikiria mtu aliyepo Zambia, mimi nilijaribu kuagiza wakati huo nafanya kazi Zambia nilete kitu mpaka kule Lusaka kilikuwa kinagharimu zaidi ya dola za Marekani 1000 na ilikuwa ni *deep freezer* tu kubwa sikulinunua, ndipo nilipogundua umuhimu. Sasa bandari hii ya kwetu inaweza kutupatia faida, tuitumie vizuri mizigo tuhakikishe inatoka haraka lakini ndivyo hivyo kwamba kutoka haraka siyo kwamba sasa kuwe na *fast truck*.

Mfanyabiashara akitaka kutajirika, njia mojawapo ya kutajirika ni kutolipa kodi. Kwa hiyo, kila mtu yupo pale kukwepa kodi ! "Kama ukitaka kuwa tajiri usilipe kodi", ndiyo maana nchi zilizoendelea ukikwepa ushuru tu kodi hakuna msamaha, ni lazima ufungwe. Kwa hiyo, tunaomba tukazanie bandari yetu.

Uvuvi nao ni kitu ambacho kinaweza kutupatia pesa nyingi pamoja na misitu na viwanda, hii dhahabu ndiyo tunayo sasa lakini hata hivyo dhahabu hii ikiuzwa hivi hela kweli inakuja nyumbani? Si tunalipwa *tax* na inaishia Ulaya? Ndiyo maana ina-*contribute* 3.8%. Kwa nini uuze kitu ambacho kina-*contribute* 47.8 halafu kwenye *party you contribute* 3.8? Kwa hiyo, tunaomba sana tujikite katika hii dhahabu tuiangalie sana isije ikatuletea matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo nafikiri kimechangiwa na mwenzangu lakini naomba tu nisisitize kwamba kuna haja ya kuwa na mpango maalumu *martial plan* kuhusu kilimo kinavyokwenda ni kwamba hatujakidhibiti.

Hiki kilimo kinachangia 44.7% katika pato la Taifa na wananchi 80% wanategemea kilimo Tanzania. Kwa hiyo, ninachoomba ni kwamba nchi igawanywe kikanda tujue nini kinakuwa wapi. Aidha, utafiti ufanywe wa mbegu nzuri ili mbegu nzuri ziweze kutumika wakati wa kupata mbolea tuwe na matrekta ya kutosha, madawa na masoko. Kama tunaweza kuinua kilimo Watanzania wote tumetajirika.

Kuhusu *budget defitic* nendeni Zimbabwe mkaione, mimi nilitembelea mwaka jana, hali ni mbaya sana kule! Baada ya wale wahisani waliokuwa wanawasaidia na Mheshimiwa Mugabe akasema nataka ardhi yangu, wakakimbia wakasema kwamba anawaonea. Wazungu wachache wamemnyima misaada na sasa hivi Zimbabwe hali ni mbaya sana. Sasa hii *budget deficit* tujiwekee mkakati kwamba miaka 10 ijayo tutakuwa tunajitosheleza, hapo tutakuwa tunalinda uhuru wa Taifa letu.

Sasa nataka nizungumzie Serengeti. Jimbo la Seringeti ni tajiri sana kwani lina hoteli nyingi na watalii wengi huja huko lakini huja kwa ndege ama magari kutoka Arusha na kurudi. Tunaomba barabara za Wilaya ile zitengenezwe kwani hatuna barabara

hata moja ya changarawe, ili na sisi tuweze kupata watalii hao. Vilevile barabara ya lami ambayo inatarajiwa kutengenezwa kutoka Makutano kupitia Mgumu kuelekea Loliondo, tunaomba nayo ianze mara moja.

Tunazo shule nyingi za sekondari lakini hatuna walimu, kwa hiyo, tunaomba Serikali itupatie walimu, tumejenga shule lakini watoto wanakwenda pale wanafeli mitihani.

Kuhusu maji napenda kuishukuru sana Serikali kwa kutupatia fedha za kujenga bwawa la Manchira, sasa linakamilika lakini tunaomba hela za kuweka mabomba ili maji yaweze kufika mjini.

Vilevile tunazo hoteli nyingi lakini zile hoteli watalii wanalala sisi hatupati kitu chochote, tunaomba angalau tungepewa dola 2 za kitanda yaani kila mtalii akilala tupewe hata dola mbili tutaendelea. Lakini kwa sasa hizo hoteli zipo lakini faida yake kwa wananchi hatuioni.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo narudia tena kusema kwamba naunga mkono hoja hii.

Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dr. James M. Wanyacha na sasa namwita Mheshimiwa Pindi Hazara Chana na Mheshimiwa Balozi Sued Kagasheki na Mheshimiwa Felix Christopher Mrema atafutia.

**MHE. PINDI HAZARA CHANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nichukue nafasi hii kukushukuru kupata nafasi hii ya kuchangia hotuba hizi mbili yaani ya Mipango na Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nami niungane na Watanzania wengine wote kutoa pole kwa familia za marehemu waliopata ajali kwenye basi la Singida, nasema pole na Mwenyezi Mungu aziweke Roho za Marehemu Mahali Pema Peponi, Amin!

Mheshimiwa Naibu Spika, ninazungumza kwa niaba ya wananchi wa Iringa mimi ni Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Iringa. Wananchi wa Iringa kwanza kabisa wanaishukuru Serikali kwa bajeti iliyopita ya mwaka jana ambayo iliweka vipaumbele mbalimbali na kimsingi vipaumbele vile vimesimamiwa na kutekelezwa ipasavyo. Ni matumaini ya wananchi wa Iringa pia kwamba bajeti hii tutakayopitisha pia vipaumbele ambavyo tutakuwa tumeviweka vitasimamiwa na kuzingatiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wameshukuru sana Sekta ya Elimu kwa mambo makubwa ambayo tumeyafanya katika nchi yetu, wameshukuru pia uwezeshaji wa *Local Government Authorities* pamoja na masuala ya biashara kwa kuondoa leseni ambazo tulisema kwamba mtu atalipa mara moja na hatalipa tena. Kwa hiyo, watu wengi wamewekeza mtaji mkubwa katika masuala ya biashara na vilevile ikapelekea kuongeza

ajira kwa tafsiri ya ajira ya nchi ya Tanzania katika Sekta Rasmi na Sekta isiyo Rasmi. Kwa hiyo, wananchi wanashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile wanashukuru sana kwa hotuba ya Wizara ya Mipango pamoja na Fedha ambayo imeonyesha vyanzo mbalimbali vya mapato na wametoa ushauri ufuatao ambao naomba niulete mbele ya Bunge lako Tukufu.

Wananchi wa Iringa baada ya kuisikia hotuba ya Wizara ya Mipango wameona rasilimali kubwa katika nchi yetu ambayo ipo Iringa Wilaya ya Ludewa inayoitwa Mchuchuma na Liganga, chanzo kikubwa ndani ya nchi na ndani ya Afrika Mashariki na duniani kote hakikutajwa kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, chanzo hiki ni rasilimali kubwa sana, chanzo hiki ni muda mrefu sana tumekuwa tukikisemea lakini bado *project* hii haija *take off* kwa muda mrefu. Sasa suala hili nalileta tena mbele ya Bunge lako Tukufu na nitashukuru sana tutakapopata maelezo juu ya hatma ya Mchuchuma na Liganga. Yamkini watu wengi watakuwa hawajafika maeneo haya na hawaelewi labda Mchuchuma ni nini na Liganga ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, Liganga ni Jiwe la Chuma na Mchuchuma ni Makaa ya Mawe. Chuma hiki ambapo kipo zaidi ya mita 30 kwenda juu kutoka usawa wa ardhi wakati Madini mengine yanatafutwa mita kadhaa kwenda chini lakini Liganga iko mita kadhaa kwenda juu. Kwa hiyo, hata gharama zake za kuendeleza ni ndogo ukilinganisha na Madini mengine ambayo yanazungumzwa nchini Tanzania. Tunaweza baada ya kuzalisha chuma, na uzuri ni kwamba unahitaji makaa ya mawe ambayo nayo yako Wilaya ya Ludewa kuyeyushia chuma hiki, sasa hapo Mungu atupe nini? Unahitaji Makaa ya Mawe kuyeyusha chuma na vitu vyote viko Ludewa, ni suala tu la sisi nchi yetu kuamua kwamba sasa ni wakati wa Mchuchuma na Liganga ku *-take off*.

Tunaweza tuka-*produce* chuma, katika hotuba ya mipango imeeleza kwamba katika vitu ambavyo tumekuwa tuki- *import* ni pamoja na chuma, nchi ya China wameweza sana kuleta mapinduzi ya Viwanda kwa kuwa wana- *produce* chuma na kuuza nje hata Tanzania. Tunaagiza chuma na vyuma vya aina mbalimbali kutoka China lakini sisi wenyewe tunayo haya Madini ya chuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni imani yangu kwamba wakati umefika sasa suala la Mchuchuma na Liganga likaanza kufanya kazi, muda mrefu sana tunaambiwa kwamba jambo hili lipo katika hatua za *study,* ni zaidi ya miaka 30.

Lakini wananchi wa Iringa wamenituma kwamba katika harakati hata za hizo *study they are ready to volunteer* washirikishwe basi, washirikishwe wawepo kwenye hizo tafiti ili waone ni nini kinaweza kikafanyika pale. Lakini tunaposema tafiti zinaendelea na kiwango kinachoendeleza huo utafiti ni katika kiwango cha kitaifa. Hali hii inafanya iwe vigumu sana kwa wananchi waliopo kwenye Halmashauri za Wilaya kuelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara ya mwisho nilipokuwa nimefika pale nilisomewa hotuba pamoja nyimbo mbalimbali wananchi wanalia wanasema Mchuchuma na Liganga vimekuwa kama ni kituo cha utalii, watu wanakuja wanaangalia basi! *Mchuchuma is there and Liganga is there* kisha wanarudi na kesho wanakuja wageni wengine, sawa tumeona wanarudi. Inakuwa ni kama Mbuga za Wanyama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani wakati umefika sasa na nitumie nafasi hii baada ya Mkutano huu wa Bajeti ninaomba sana Waziri wa Nishati na Madini, Waziri wa Viwanda pamoja na wewe mwenyewe Naibu Spika unayetokea Wilaya ya Njombe, tuongozane na mimi twende tukaone malighafi hii adimu Afrika na duniani kote ambayo tumekaa miaka yote tunaiangalia…..

**NAIBU SPIKA:** Nafikiri wamekubali.

**MHE. PINDI HAZARA CHANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala lingine muhimu sana katika kuwezesha kiuchumi, ni suala la kuongeza *job opportunities*. Nafasi za kazi katika uchumi wowote ni muhimu sana zinaongezwa, hii itasaidia pia kuleta mzunguko mkubwa wa fedha lakini pia itasaidia wananchi wenye uwezo wa kufanya kazi wafanye kazi. *(Makofi)*

Takwimu zinanionyesha kwamba nchini Tanzania watu wenye uwezo wa kufanya kazi ni milioni 20 na wanaofanya kazi katika sekta rasmi na zisizo rasmi ni milioni 18.3 ambapo wanawake ni milioni 9.3 na wanaume ni milioni 9.3. Kwa hiyo, bado ni imani ya wananchi walio wengi kwamba Mchuchuma na Liganga itakapofanya kazi itaongeza ile idadi ya milioni 20 kwenda hata milioni 25, ajira zikaongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana suala hili lizingatiwe lakini maswali madogo madogo ya mafuta ya taa, leseni za magari *CC 1500* ziingie Mchuchuma na Liganga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nizungumzie kuhusu suala la kilimo. Kutokana na Wilaya zetu ambazo ziko pembezoni kama Ludewa, Makete na Wilaya nyingine Mkoani Iringa na kupelekea kwamba nafasi za ajira zikawa hafifu kutokana na huu Mchuchuma na Liganga kutokufanya kazi basi imebidi tuwekeze katika Kilimo. Tumewekeza katika kilimo lakini kilimo chetu bado kina changamoto kama ifuatavyo:-

Changamoto ya kwanza katika kilimo ni kwamba tunategemea sana mvua bado hatujaweza kutumia kilimo cha umwagiliaji maji ipasavyo. Mwaka jana tulikuwa na uhaba wa chakula na mwaka huu mvua zimenyesha nyingi sana na hatujafanya vizuri sana katika maeneo yetu kubuni miradi yaani *projects* za *irrigation*. Juzi naambiwa Mtera maji yameanza kupungua ingawa walituahidi kwamba tutafika lakini yameanza kupungua. Kwa hiyo, haya ndiyo mambo ambayo tunapaswa kuzingatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba tupate wawekezaji wa kutosha katika suala zima la kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la soko huria kwa wananchi wa maeneo ya Ludewa, Makete na Njombe, soko huria bado ni jambo gumu sana kwa sababu miundombinu yetu ni hafifu. Wafanyabiashara hawafiki kule kwa hiyo tunaomba sana Serikali iongeze vituo vya *SGR,* Hifadhi ya Serikali wajenge kule maeneo ya Ludewa.

Sasa hivi tunatumia kituo cha *SGR* Makambako ambacho hakinunui sana mazao kutoka kule kwa sababu palepale Makambako wanazalisha sana na niitumie nafasi hii kuwaomba wananchi wafanyabiashara wote nchini Tanzania wanaotaka kununua mahindi tunayo mahindi mengi sana Mkoa wa Iringa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa pembejeo tunashukuru Serikali imefanya kazi vizuri sana kwani mwaka jana tulikuwa na wakala katika kila kata lakini kulikuwa na utaratibu kwamba vibali vya pembejeo vinapatikana Makao Makuu ya Wilaya, Kata nyingine zilikuwa mbali kwa mfano Kata ya Manga na vijiji vya Madilu, Kitulo na hata Kilolo vilikuwa mbali. Kwa hiyo, kwenda kuchukua kila kibali Makao Makuu ya Wilaya tuangalie jinsi ya ku-*decentralise,* vile vibali vya pembejeo vipatikane ngazi ya Kata kulekule waliko wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naona nimegongewa kengele ya kwanza sasa nimalizie harakaharaka, nitakuwa mnyimi wa fadhila nisipozungumzia suala la wanawake. Katika nchi yetu wanawake wapo zaidi ya 50%, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais ametukumbuka sana wanawake ametuweka kwenye vyombo nyeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unapotumia kada hii ya wanawake utafiti umeonyesha kwamba ni wachapakazi wazuri sana. Wanawake ni wafanyakazi bora, wako makini hata *graph* ya rushwa ukiangalia maeneo ambapo wapo wanawake hakuna *corruption*.

Kwa kuwa katika Ilani imesema kwamba itaangalia jinsi ya kuendelea kuwatumia wanawake kutoka 30% kuongezeka, niitumie nafasi hii kushukuru sana kwamba lipo kwenye Ilani na sasa kwa kuwa tunajadili suala la bajeti basi niweke msisitizo ili liwepo katika mipango na hatimaye kwenye bajeti kuangalia jinsi ya kuwatumia wanawake maana yake mchango wao ni mkubwa hivyo wanapokuwepo kwenye vyombo mbalimbali ikiwa ni nafasi za Bunge, nafasi ya Udiwani na *Local Government* kwenye vyombo vya kufanya maamuzi *(decision making bodies)* hata ile bajeti inakuwa ni *gender sensitive* maana yake wanabeba mzigo mkubwa sana nchini. Wana mzigo mkubwa wa yatima, mzigo mkubwa wa kuzalisha mazao ya kilimo na kadhalika. Lakini wakati wa kupanga bei za mazao hata katika *interview,* hata katika bodi wakati mwingine wanawake hatuwaoni. Watu wanapohojiwa juu ya *interview* wanawake hatuwaoni, tunaomba sana Serikali yetu kwa jitihada ambazo wameshaonyesha juu ya utashi wa kisiasa, kuwatumia wanawake iendelee kuwatumia wanawake hawa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia na niitumie nafasi hii pia kusema naunga mkono hoja hii, nisingependa kengele inigongee. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. BALOZI HAMIS SUED KAGASHEKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu asubuhi hii ya leo.

Kwanza naomba kwa niaba ya Wanajimbo wa Jimbo la Bukoba Mjini kutoa mkono wa tanzia kwa watu wa Singida kwa msiba mkubwa uliowafikia siku hizi za karibuni, tunasema pole sana.

Baada ya hapo naomba kwa niaba ya wapiga kura wa Jimbo la Bukoba Mjini ambao siku zote ninasema ni waajiri wangu, niseme kwamba nawashukuru sana kwa imani ambayo waliiweka kwangu mimi na wananipa nafasi hata ya kuwa hapa Bungeni kuwasemea hayo ambayo nitayasema sasa hivi kwa mujibu wa Bajeti ya Serikali ya mwaka 2007/2008.

Ningependa nimpongeze Spika wetu ambaye hayupo lakini naomba unifikishie salamu zake kutoka kwa wapiga kura wangu wanasema kwamba juhudi zake za kuongoza Bunge zetu zinakwenda vizuri sana. *(Makofi)*

Ningependa hapo hapo nimpongeze Waziri Mkuu na isiwashangaze kwa nini nasema nataka nimpongeze Waziri Mkuu. Waziri Mkuu alifanya ziara ya kuja katika MKoa wa Kagera na alikuja katika Jimbo la Bukoba Mjini mwezi MAchi mwaka huu katika vitu vikubwa ambavyo alikumbana navyo hapo kulikuwa na suala la kilimo katika Mkoa wa Kagera na kuliwa na suala la Halmashauri ya Jimbo langu.

Kuhusu kilimo aliacha maagizo na aliona kabisa kwamba kilimo cha Kagera kimeshuka sana na alisikitishwa kabisa kuona kwa mfano, mbolea ambayo ilikuwa pale haijatumika na sababu zikazungumzwa kwa nini haikutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kubwa zaidi ambalo nataka niliseme ni kwamba Waziri Mkuu alikuta kulikuwa na Afisa wa Kilimo wa Mkoa ambaye alikuwa amekaa pale kwa miaka 13 na taarifa aliyoitoa mimi naweza kusema kwamba Waziri Mkuu yeye mwenyewe kabisa katika majumuisho alionekana alikuwa *shocked* kabisa.

Kwa sababu kwanza alikuwa haelewi nini kinaendelea katika Mkoa, alikuwa haelewi kilimo kinakwenda vipi na kadhalika na nakumbuka Mheshimiwa Waziri Mkuu alimuuliza aelezwe sababu kwa nini baada ya miaka 13 (na ripoti hii ambayo unatoa) tuendelee kuwa na yeye kama Afisa wa Kilimo wa Mkoa? Kwa hiyo, mimi nasema kwamba baada ya kutoa maagizo kulikuwa na mikutano ambayo ilifuatia, nasema kwamba tutampa taarifa. Matatizo mengine siyo ya Serikali Kuu lakini yanakuwa ni ya huku chini katika utendaji. Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye Halmashauri pia alikuta kuna matatizo na hayo bado tunajaribu kuyatazama.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, naomba niwapongeze Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, wote wawili kwa taarifa zao.

Waziri wa Fedha kwa kutupa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka 2007/2008 na Waziri wa Mipango, Mheshimiwa Juma Ngasongwa kwa taarifa ya Hali ya Uchumi ya mwaka 2006 na mipangilio ya uchumi katika miaka mitatu ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naweza kusema tu kwamba baada ya kusikiliza bajeti hii, nimeona kuwa si nyepesi na mtu akisema kwamba ni bajeti nyepesi nadhani si kweli, kwa sababu tumeona jinsi Watanzania wote kwa ujumla walivyoipokea. Lakini hiyo ni kawaida kwa sababu hata kule Uingereza ambapo uchumi wao umekua na huwa napenda siku zote kulinganisha na mataifa mengine kwa sababu Uingereza uchumi wao ulikuwa mbovu, licha ya Waziri wao wa Fedha kujitahidi sana, pamoja na *sterling pound* kuwa na nguvu, lakini bado Kambi ya Upinzani walikataa hata bajeti yao ambayo walipitisha mwaka huu mwezi Machi. Lakini hiyo ni kawaida kwa sababu unapokuwa na Upinzani lazima wapinge kitu ambacho wanaona wanaweza wakakipinga. Kwa hiyo, kwa kweli mimi hainishangazi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, isipokuwa nataka kusema tu kwamba wapiga kura wangu ambao ni waajiri wangu wa Bukoba Mjini, wamenitumia barua pepe na hii naona niiseme kwa sababu kwa utaratibu tulionao sasa hivi wananiona hata katika televisheni na watashuhudia kwamba ninakubali kwamba nilipata barua pepe zao. Kwa mfano, kuna vikundi vya pale Bukoba Mjini vilivyonitumia barua pepe, kuna kikundi cha Twenyambe, kuna kikundi cha Owebanze, kuna kikundi cha Katanyukwile, kuna kikundi cha Mwataniwabaki, kuna kikundi cha Seneti na hawa wameleta mawazo yao jinsi walivyoipokea bajeti ya Serikali. Lakini pia nimepata *SMS* kutoka kwa wafanyabiashara wa pale Bukoba Mjini akiwemo Ndugu Mlindwa, ndugu Wejazibar, Yakubu Kabaka, Salum Mawingu, Ndugu Njau, Ndugu Rutinwa na wote hao kwa kweli wamenituma, haya ndiyo nataka niyaseme.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanasema kwamba wamemsikiliza Waziri wa Fedha na wamemsikiliza Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji. Wanasema kwamba katika kusikia kwao wamemsikia Waziri wa Fedha akisema kwamba mfumuko wa bei katika mwaka huu ni asilimia 7.3 na wamemsikia Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Uchumi wa Uwezeshaji akisema kwamba ukuaji wa ongezeko la kipato cha mtanzania katika mwaka huu 2006 umekua kwa asilimia 10.8. Lakini wao wanasema kipimo cha mfumuko wa bei na kipimo cha uongezekaji wa pato lao kama Watanzania wanakipima kwa yafuatayo, nayo ndiyo nataka niyawasilishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanasema kwamba mwaka 2005 kilo moja ya mchele walikuwa wanainunua kwa shilingi 300 pale Bukoba Mjini, wanasema sasa hivi mwaka 2007 kilo ya mchele wanainunua shilingi 600. Wanasema mafuta ya taa mwaka 2005 walikuwa wanayanunua lita moja shilingi 800, wanasema sasa wananunua lita moja ya mafuta shilingi 1200. Wanasema sukari imetoka shilingi 700, sasa hivi kilo moja wanainunua kwa shilingi 1200.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanasema mfuko wa semeti umetoka shilingi 14,000, sasa hivi wanaununua kwa shilingi 17,500. Wanasema petroli na dizeli kwa Bukoba bei ni moja hiyo hiyo lita moja inauzwa kwa bei ya shilingi 1600 na wasema

hiyo ikilinganishwa na Dar es Salaam ambako dizeli lita moja inauzwa kwa shilingi 1240. Wanasema kwa hali hiyo wao wanaamini kabisa kwamba bajeti ni kali na ina makali; na kwa maana hiyo wanasema kwamba iko haja kwa Serikali kuwatazama watu wa Kagera na hasa watu wa Bukoba kwa sababu ni Mkoa wa pembezoni. Aidha, wanasema usafiri una matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, usafiri wa majini wao wamenituma na ni wajibu wangu niseme hapa Bungeni. Wanasema kwamba MV Bukoba ambayo ilikuwa ndiyo ikiwasaidia katika kusafirisha abiria kutoka Bukoba kwenda Mwanza wamesema kwamba ilizama miaka 10 iliyopita na Serikali haikufanya jitihada za kuwaletea chombo mbadala. Lakini hata hivyo, chombo ambacho kimekuwa kinatumika sasa hivi ni Meli ya MV Victoria ambayo karibu ni mwezi mmoja haifanyi kazi na meli inayotumika sasa hivi ni MV Serengeti ambayo si ya abiria kwa sababu utengenezwaji wake ilikuwa ni meli ya kubeba mizigo. Kwa hiyo, wanasema kwamba kwa kweli ipo haja Serikali ilitazame suala la usafiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa sasa mafuta yamepanda bei; na kwa kuwa wako pembezoni, wanasema ina maana kwamba kila kitu kitapanda bei na kwa hiyo, mfumuko wa bei kuhusu wao itakuwa ni tabu. Wanasema usafiri wa ndege, kiwanja cha ndege cha Bukoba Mjini pale hakijafanyiwa ukarabati. Katika taarifa yake Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji alisema kwamba tayari katika 2006 kazi imeanza kufanyika na uzio umewekwa, lakini ukweli ni kwamba kazi haijaanza kufanyika na uzio haupo na hii ukitazama katika hotuba yake ukurasa wa 48 ndivyo anavyosema, lakini hiyo si kweli! Kwa hiyo, tunaomba Serikali ijaribu kuzingatia na kutazama matatizo ambayo yanakabili mikoa ya pembezoni na Mkoa Kagera ukiwa ni mmojawapo ambao kwa kweli kiusafiri una matatizo na watu wa Kagera wanaomba hata upande wa barabara kipande ambacho kinatoka Biharamulo kwenda Mwanza kitengenezwa haraka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, mimi nasema kwamba yapo mengine muhimu ambayo tunaweza tukayatazama ambayo yanaweza yakatusaidia katika Serikali wakati tukiwa tunatengeneza bajeti yetu kama hivi ilivyotengenezwa. Kwa mfano, Tanzania ina vitu viwili muhimu ambavyo tujaribu kuvitumia kwa nguvu sana. Kwanza, upande wa Maliasili, tunazo nyingi karibu kuliko hata nchi nyingine katika Bara la Afrika. Pili, tuna amani ya kisiasa ambayo nchi nyingi katika Afrika hawana na hiyo tukiweza kuitumia ingeweza kutusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa uwekezaji wa kutoka nje kuwekeza Tanzania, ukitazama kwa kweli ni kidogo sana ingawaje taarifa ya Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Uchumi, Mipango na Uwezeshaji inaonyesha kwamba kumekuwa na ongezeko, lakini ongezeko hilo unaona kabisa limejikita katika maeneo matatu. Eneo moja ni la madini, eneo la utalii, na eneo la viwanda vidogo vidogo, lakini maeneo mengine makubwa ambayo yangeweza yakatusaidia inaonekana Serikali bado haijayafanyia kazi lakini iko haja ya kutazama hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna utafiti ambao umefanywa na Umoja wa Mataifa Kitengo cha *UNCTAD* ambao umetoka mwaka jana ambao unaonyesha kwamba upande wa uwekezaji katika Afrika Tanzania imechukua nafasi ya pili pamoja na Angola, baada ya *South Africa*. Lakini wanasema kwamba bado hatujatumia utaalamu na ujuzi wa kuweza kuvutia uwezekaji katika njia ambazo zinastahili.

Jana Mheshimiwa Michael Laizer hapa alizungumzia juu ya suala la mifugo. Utafiti ambao wamefanya watu wa *UNIDO* unasema kwamba upande wa mifugo Tanzania ni ya tatu katika Afrika na utafiti huo u naonyesha kabisa kwamba hatujafanya uwekezaji wa kutosha ama hatujafanya utaratibu wa kutosha wa kutumia hiyo mifugo kama kiwanda kikaweza kuwaajiri watu wengi ambao wanaweza wakafanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini baada ya kutazama yote hayo naomba niseme kwamba ipo pia haja ya kusema kwamba utaratibu wa kufanya biashara hapa Tanzania kweli tunajaribu kuwavutia wawekezaji, lakini pia urasimu ni mwingi na kufanya biashara hapa Tanzania ni ghali ukilinganisha na nchi za jirani ambazo zimepunguza mambo mengi ambayo yanawasaidia kuwafanya watu wengi waweze kuja kuwekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania kwa ardhi ni nchi kubwa kwa sababu ukilinganisha ardhi ya Tanzania ukalinganisha na nchi ya Ujerumani na Ufaransa, ukiziweka pamoja nchi zote mbili hizo bado Tanzania ni kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia naweza nikasema ukubwa wa Tanzania ukiweka Kenya na Uganda ukaziunganisha pamoja bado hujafikia eneo la Tanzania. Ina maana kusema kwamba Tanzania ni nchi kubwa, kwa hiyo, ina mabonde mengi, ina mito mingi, ina maziwa ya kutosha na kadhalika na ni kiasi cha kutazama tunaweza tukavitumia namna gani *(Makofi).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa kilimo ambapo Waheshimiwa Wabunge wengi wamekizungumzia, kwa kweli hatujafanya kazi ya kutosha. Kwa sababu ukitazama takwimu tulizonazo unakuta katika maeneo ambayo tunaweza tukayatumia katika kutengeneza kilimo, hekta milioni 99 zinaweza kuwa za umwagiliaji, lakini katika hizo ni chini ya milioni moja ambayo inatumika katika kilimo cha umwagiliaji. Sasa hapa yako majibu ambayo yanaweza yakatusaidia kama tukiweza kuweka nguvu katika kilimo. Ukitazama upande wa thamani ya shilingi yetu utakuta kwamba imekuwa ikiporomoka, majibu ambayo tunayapata nasikitika kusema kwamba hayaridhishi. Kwa sababu Serikali inajaribu kusema kwamba shilingi inaporomoka kwa sababu mazao ambayo tunauza nje ni mazao machache na kwa sababu ya suala la soko huria huwezi ukaliingilia, kwa hiyo, hilo ndilo linafanya thamani ya shilingi ikateremka chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukweli wa mambo ni kwamba tukitazama huko ambako soko huria limeanzia wao wakati mambo yanakuwa mabaya wanaliingilia hilo soko huria, Wamerikani hawako *exceptional* wamekuwa wanaingilia soko hilo, Wajapan wamekuwa wanaingilia soko hilo, Waingereza wamekuwa wanaliingilia soko hilo. Sasa

mimi ninachosema *Bank of Tanzania* hapa kusema kweli ni chombo cha umma na ni chombo cha kulinda maslahi ya umma. Yamefunguliwa mabenki mengi, lakini hakuna mwongozo wa kutosha kwa wananchi jinsi ya kuyatumia mabenki hayo, hakuna utaratibu wa mabenki wa hayo, na ni wajibu wa *Bank of Tanzania* kutazama suala la riba. Kwa sababu unaposema kwamba riba ni suala la soko huria hiyo si kweli! Kwa sababu sasa hivi ukitazama na Benki Kuu wanajua, Wamerakani na wengine katika *G8* wamekuwa wanawapigia kelele Wachina kusema kwamba wanataka wapunguze thamani ya fedha yao kwa kuwa ipo juu. Wachina wao wakasema kufuatana na hali ya soko fedha yao ndivyo ilivyo. Kwa hiyo, hali ya biashara kati ya China na nchi nyingine ipo namna hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini unaona kabisa kwamba iko dhamira ya Serikali za Mataifa makubwa kujaribu kuingilia soko kwa shabaha ya kujaribu kudhibiti fedha ya Kichina, na hii natoa tu kama mfano.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

*(Hapa Kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, ahsante sana. Sasa nitamwita Mheshimiwa Felix Mrema. Mheshimiwa Castor Ligallama na Mheshimiwa Halima Mdee wajiandae.

**MHE. FELIX C. MREMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie. Kwanza, nitumie nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote wawili, Naibu Mawaziri wao, Makatibu Wakuu na wataalamu wao waliofuatana nao kwa hotuba nzuri zilizowasilishwa hapa Bungeni na hao Mawaziri wao. Niwatoe wasiwasi kuwa naunga mkono hoja zote zilizowasilishwa na Mawaziri hao wawili mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilichonifurahisha zaidi ni kwamba bajeti hii imetushirikisha sisi kwa kiwango ambacho nafikiri hakijapata kutokea katika historia ya Bunge hili. Tulishirikishwa kwenye semina tukatoa mawazo mengi na mazuri tu yakazingatiwa na Serikali kwa kiwango kikubwa sana.

Hata kwenye Kamati zetu za Bunge tuliwarudisha Mawaziri waende wakayarekebishe maeneo ambayo tuliona yana kasoro, wakatusikia na wakafanya hivyo. Nawapongeza sana kwa ujasiri huo mkubwa waliotuonyesha wa kutusikia sisi Waheshimiwa Wabunge na kwenda kurekebisha bajeti hiyo ioane na matashi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naelewa kabisa kwamba yamekuwepo machungu mengi kwenye bajeti hii na mimi pia nilipigiwa simu na wapiga kura wangu wa Arusha wengi tu na wengine walinitumia ujumbe na nitawataja wawili. Mmoja alikuwa Alhaj Msangi mzee wa pale Sibetini namheshimu na mwingine alikuwa mama Bichu bila mfanyabiashara mzuri tu pale Arusha, wote hao walikuwa wanalalamika wakisema Mheshimiwa Mbunge tutakufa kwa mtazamo huo.

Kodi hizo zimepandishwa zitatumaliza, nikawambia tulieni. Wakasema piga kelele huko zipunguzwe, nikawambia hilo kwa heshima siwezi, kwa sababu mimi nilishiriki kikamilifu katika kuishinikiza Serikali iongeze hiyo kodi. Sasa leo siwezi kurudi nikaiambia Serikali hiyo hiyo hapana, turudi nyuma, hapana mzee, wakasema tutaendelee kubana mikanda yetu kwa ajili ya kufanya kazi hiyo muhimu ambayo tumeamua kuifanya ya miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka ndugu yangu Kabwe Zitto kwenye semina ile alisema kipaumbele ni miundombinu, sasa Serikali imeenda imeifanyia kazi haikuona mahali pengine isipokuwa kwa kupandisha kodi, sasa itakuwaje sisi tukiwa wa kwanza kusema hapana, mrudi nyuma! La hasha!

Lazima turudi kwa wananchi wetu tuambie kwamba hii kulikuwa hakuna namna lazima kodi hiyo iongezwe ili dunia nzima ijue *we are serious* katika kupambana na hili tatizo la miundombinu katika nchi yetu na tuko tayari *serious* katika kubana mikanda yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini akaniambia Mzee huyo kusema kwamba kwa mtazamo huo mnatuondoa katika *radar* ya kuwa na magari lilinisumbua kweli. Lakini nikakaa nikafikiri tatizo la huyo mzee wangu ni nini siyo hii kodi ni mfumo mzima wa jinsi alivyopata hiyo gari yake. Huyo mzee kama ninavyoelewa ilimbidi ajibane, ilimbidi ajifunge mkanda yeye na familia yake aweze kupata shilingi milioni kumi na kitu anunue gari, ndilo tatizo la nchi hii.

Mfumo huo wa mtu kutafuta fedha kupata malighafi au pembejeo muhimu kama hiyo ambayo anaitumia, tungelimwezesha huyo mzee kama ilivyo mahali pengine popote kupata mkopo wa miaka mitatu wa kununua gari yake ile alipe taratibu huku anafurahia matunda gari yake, asingesita kulipa kodi hii ambayo tunaongeza hapa huku akijua kwamba kodi hii hatimaye yake ni kurefusha uhai wa maisha ya gari yake kwa miundombinu kuwa mizuri, asingesita hata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tatizo letu ni mfumo huo wa watu wetu kuwafikisha hapo wanatafuta fedha kununua vitu kama magari. Sasa Waziri wa Fedha alitwambia nini kwenye hilo? Kwenye ukurasa wa 21 wa hotuba yake, "Serikali karibu itakamilisha Muswada wa Sheria utakaoweka mazingira ya kuwezesha upatikanaji wa mikopo kwa njia ya ukodishaji vifaa, mitambo na rasilimali nyingine." Ndiyo majibu rahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, na yote hii tunaambiwa iko kwenye Awamu ya pili ya Maboresha na mageuzi katika Sekta ya Kilimo. Mimi najiuliza kuna nini kwenye hii Awamu ya Pili. Nimeisikia hadithi yake kwa zaidi ya miaka minane iliyopita. Awamu ya Pili ya Maboresha na Mageuzi, tunafanya nini huko. *Rocket Science* au ni mambo ya kawaida ambayo dunia nzima na majirani zetu wana utaratibu kama huo ambao tunasema yapo ndani ya Awamu ya Pili ya Maboresha na Mageuzi katika Sekta ya Kilimo.

Sasa kwa nini tuchukue miaka zaidi ya 8 kukamilisha hiyo mpaka sasa hivi miaka yote hiyo minane ni Miswada miwili tu ambayo tumeletewa hapa Benki Kuu na *Financial Institutions* ya mwaka jana.

Hayo mengine yote tunaambiwa bado, karibu kukamilika na watu wetu wanazidi kuendelea kudhoofika na kuumia. Mimi sasa ndiyo nasema nafikiri kinachohitajika ni sisi tuilazimishe Serikali ikamilishe awamu hiyo ya pili kwa kasi na nguvu inayohitajika kupambana na tatizo hili la kutokuwa na mfumo mzuri wa fedha katika nchi hii. Ndiyo msingi wa hoja yangu ambayo nilikuwa nataka niilete.

Serikali ikiniambia kwamba wako tayari, sina haja ya kuwa na hoja hiyo, waonekana kwamba wanaishughulikia hii kwa nguvu na kasi inayostahili; na wangetuletea hata katika bajeti iliyopita ingemwezesha Mzee wangu Alhaj Msangi angepata mkopo wa gari.

Niliambiwa toka mwaka jana ilikuwa iko tayari ingeweza kuletwa, sasa sijui inazunguka zunguka namna gani huko Serikalini mpaka bajeti nyingine inakuja tunaambiwa bado iko karibu itakamilika, hapana!

Lazima tuonyesha *seriousness* na njia ya kuonyesha *seriousness* ni sisi hapa nawashawishi Waheshimiwa Wabunge wenzangu tuiagize Serikali kama inaweza kuleta mwisho wa bajeti hii sheria ile watuletee tutengue taratibu tupitishe sheria hiyo halisi tuondoe aibu hii katika nchi yetu na tuwe na mfumo wa watu kuweza kukopa na kupata hiyo malighafi kwa njia ambayo ni rahisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka kulizungumzia ni lile ambalo nalipigia makelele kila siku hapa, *mortagage finance*. Naambiwa na hii nayo iko kwenye hiyo Awamu ya Pili ambayo inachukua zaidi ya miaka minane kukamilika.

Kwenye Kamati Waziri alitwambia kwa maandishi Jumuiya ya Vyombo vya Fedha imewasilisha Serikalini mapendekezo ya vipengele mbalimbali vya sheria vinavyohitajika kurekebishwa ili vyombo hivyo viweze kutoa mikopo ya nyumba. Serikali inatafakari mapendekezo hayo.

Kwenye hotuba yake ukurasa wa 22 ametumia maneno kama hayo hayo, lakini kaongeza mengine kidogo mazuri amesema kwamba: “Ili kuboresha mazingira ya upatikanaji wa mikopo ya nyumba (*mortagage finance*) Serikali inaanda Muswada wa marekebisho ya vipengele kadhaa vya Sheria ya Ardhi na sheria nyingine.”

Sasa hapa ndiyo inanipa wasiwasi. Kuna nini la zaidi tena linalotakiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, nimejaribu kufanya utafiti, nimegundua kwamba Tanzania *Bankers Association* imeleta mapendekezo mengine zaidi ya kufanyiwa marekebisho katika ile sheria ya Ardhi. Sasa mimi ninavyoelewa tulipokea

mapendekezo yao mwaka 2002, tukabadilisha Sheria ya Ardhi, *(the Land Act*), tukaibadilisha sura nzima ya kumi ili ioane na matashi ya *Tanzania Bankers Association*.

Nilitegemea kwamba baada ya mabadiliko yale ya mwaka 2004 kwnye *Land Act*, Tanzania *Bankers Association* ingezama sasa kwenye soko na kuanza kutoa mikopo ya muda mrefu kwa ajili ya kutuwezesha sisi kujenga nyumba za kuishi. Hiyo ni siyo mikopo ya miaka mitano, ni mikopo ya miaka ishirini na zaidi ndiyo *mortagage finance* hiyo.

Sasa hawakufanya hivyo mpaka leo wanakuja na mapendekezo mengine, naona hao watu wanatuchenga bila msukumo wa makusudi wenye nguvu ya kisheria, hao watu hawatawekeza kwenye hiyo *mortagage finance*. Kwa nini hawataweza nitoe tu mfano. Katika miezi mitatu ya kwanza ya mwaka 2007, Taasisi za Fedha nchini zilikuwa tayari kununua *Government paper* yaani hizo dhamana na hati fungani za Serikali *(treasury bills)* na *treasury bonds* zenye thamani sawa na dola za Marekani milioni 979.

Wana pesa kwa kipindi cha miezi mitatu tu yaani ni shilingi trilioni 1.2 wakati bajeti yetu ni trilioni 6, kwenye miezi mitatu wako tayari kununua *government paper* trilioni 1.2. Serikali ikawauzia ngapi? *USD 622 milion dollars* yaani trilioni 791.

Hapa ndipo wanapopata faida yao kwa urahisi kabisa, wanakula kuku kwa mrija na mtu anayekula kuku kwa mrija hawezi kwenda kufanya kazi ile ya kutoa jasho ile *mortagage finance*. *Mortagage finance* ni kazi ya kutoa jasho pale kwa nini aende huko. Sasa hatua za makusudi zinahitajika kumlazimisha yeye aende huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefurahia sana kwamba Serikali sasa imeamua kujiondoa kwenye hilo soko. Tuipongeze Serikali kwa hatua hiyo nzuri na muhimu ya kujiondoa kwenye hilo soko la hati fungani na dhamana za Serikali.

Sasa changamoto ni kwamba watafanya namna gani wale sasa watumie fedha zao ziende kwenye sekta muhimu zitakazochochea ukuaji wa uchumi wetu. Nasema bila mapendekezo hayo kufanyiwa kazi na Waziri wa Fedha na Gavana wa Benki Kuu kutumia mamlaka waliyonayo chini ya sheria hizo tulizozipitisha mwaka jana za kutunga sheria ndogo za kuwalazimisha wao kutumia sehemu fulani ya mtaji wao katika sekta hii kwa utaratibu kwamba wanatoa mikopo kwa miaka ishirini na zaidi hao watu hawatafanya hivyo bila kuwa na sheria hiyo.

Pili, hatutakiwi kuwalazimisha waende wakakopeshe kama hawataki, kama hawataki wawekeze tu kiasi kinacholingana *(equivalent amount)* Benki Kuu huku wakijua kwamba hawatapata riba kwenye hizo fedha watakazopeleka Benki Kuu ili Benki Kuu izitumie fedha hizo kuzipa zile Taasisi ambazo zitaweza kufanya kazi hiyo ya kutoa *mortagage finance*.

Hiyo ndiyo dhana ya hoja ambayo nataka kuisaidia Serikali iweze kuzishinikiza hizo *Financial Institutions* ziwekeze katika yale maeneo ambayo yanaweza yakatoa mchango mkubwa katika kukuza ajira katika nchi yetu mpaka kila nyumba inayojengwa ikatoa ajira zaidi ya 10.

Tuna upungufu wa nyumba zaidi kati ya milioni 1. 2 na milioni 2 katika nchi hii na kila mwaka nyumba zinazohitajika 200,0000. Nyumba 120 Mijini na nyumba 80 vijijini ndiyo tathmini ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kazi hiyo tu ya ujenzi wa hizo nyumba itakuza kabisa uchumi wa nchi yetu, tutafika mahali ambapo hiyo ajira ya milioni moja iliyopo kwenye Ilani yetu ya uchaguzi itafikiwa bila matatizo yoyote.

Wale vijana wangu wa *Oysterbay* kule *Ongeremitedi* watapata ajira, wale vijana wangu Daraja mbili pale relini nikiteremka kwa mama yangu kule Limara watapata ajira badala ya kukaa kucheza *pool* siku nzima. Miji yetu yote pia itakua na vijiji vyetu vitakua kama hatua za makusudi zitachukuliwa na Serikali.

Naiomba Serikali hii ichukue hatua za makusudi ili Sekta hii itoe mchango wake katika kukuza uchumi wetu tufikie yale malengo ya asilimia 8 na 9 ya kukua kwa uchumi wetu kama kila mmoja wetu atatoa mchango wake. Sasa ninachokiomba Serikali izingatie hilo. Serikali ikifanya hivyo sina haja ya hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja zote mbili. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Awali ya yote napenda niwapongeza Mawaziri wote wawili, Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji na Mheshimiwa Zakia Meghji, Waziri wa Fedha, kwa hotuba ambazo kwa kiasi kikubwa zimezingatia maoni yetu ya mwezi Aprili, 2007. Aidha, napenda kuipongeza Serikali kwa kutupa kivuko cha Kilombero, tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mengi yameongelewa na wenzangu hasa kuhusu maeneo ya kurekebisha na nina uhakika Serikali ni sikivu, itafanya hivyo hata katika eneo la mafuta ya petroli na mafuta ya taa.

Wakati tulipokuwa tunaongea mwezi Aprili, 2007 Waheshimiwa Wabunge wengi waliguswa na hali ya barabara zetu na ndiyo maana walikubali eneo hilo kwamba wako tayari kuchangia zaidi ili barabara zetu ziwe nzuri. Waziri wa Miundombinu atambue kwamba fedha hizo zitakusanywa na zitawagusa wananchi wengi kwa maana kuwa watakuwa wanaumia.

Kwa hiyo, namwomba zitumiwe kwa uangalifu ili barabara zijengwe na ikiwezekana maoni yetu ya mwezi Aprili, 2007 tulisema turudishe kambi zile za barabara yazingatiwe. *PWD* zilikuwepo kambi kilomita 30, 50 kunakuwepo na kambi, weka *tipper* moja pale, siku hizi zipo *tipper* za tani tatu na nusu, weka *tipper* ile moja, wape wale vijana *spider*, sululu, waweke wafanyakazi hata watano tu, barabara inapoanza shimo wao tayari wameishaitengeneza, wakoloni walifanya hivyo na barabara zilikuwa zinapitika mwaka mzima.

Kwa hiyo, na sisi turudi huko, tulifanya makosa na hayo makosa na kwa bahati nzuri mimi nilifanya kazi Serikalini, makosa hayo yalianza miaka 1970 na kitu.

Watu wakasema, tuache kufanya Kambi badala yake wakaanza kutengeneza *Master Rolling,* zile *Master Rolling* za uongo. Wafanyakazi wa barabara ni uongo mtupu! Hawapo waliofanya kazi kwenye barabara hiyo. Lakini waliona kwamba tukiweka zile Kambi tutaibaje. Kwa hiyo, tuondoe Kambi ili mtu aorodheshe tu majina mia moja wamefanya kazi barabarani. Hamna! Turudishe Kambi na barabara zetu zitadumu.

Mimi mzee mmoja aliniambia kwamba enzi ya ukoloni walikuwa wanatoka Masasi kuja Dar es Salaam kuangalia mpira halafu wanarudi. Leo hii tunahangaika Mingoyo, lakini mimi sijafika huko. Lakini wanasema barabara ni mbaya. Wale waliokuwa wanatoka wakati ule miaka ya 1950 au 1960 kuja kuangalia mpira Dar es Salaam na kurudi Masasi sio hao hao waliokuwa wanatumia kambi kilomita 50, kambi! Hilo moja. Kwa hiyo, tunaomba hizi fedha zitakazoongezwa zitumike kwa uangalifu mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ningependa sana niongelee kilimo. Lakini kabla sijaongelea kilimo tunakubali kwamba uchumi wetu unakua kwa kasi ndogo sana na mahitaji ni mengi. Watanzania tunaongezeka kwa asilimia tatu, kila mwaka ni kiasi kikubwa sana. Huku tuko 37,000,000 huku *resources* ni ndogo na uchumi unakua kwa kusuasua, hatuwezi kuwa na sera ya kuua watu ili tufaidike na *resources* tu-*balance*. Kitu cha kufanya ni huko kwenye *resources* tufanye nini? Watu wabaki vile vile 37, Mwenyezi Mungu ametujalia wamezaliwa, basi.

Labda nianze kwa mfano mwaka 1988 Benki niliyokuwa naifanyia kazi, mimi *CRDB* ilinipeleka Mauritius kufanya kazi pale kwenye *Development Bank of* Mauritius kwa miezi minne, walikuwa watu 1,100,000 mwaka 1988. Sisi Watanzania tulikuwa 23,000,000 *by then.* Bahati nzuri wiki tatu, nne zilizopita mimi nilikwa Mauritius tena kwenye Mkutano wa Bodi ya Sukari kama Mwenyekiti wa Bodi ya Sukari wale watu wako 1,200,000 wameongezeka laki moja kwa miaka 19. Sisi tuko 37,000,000 tumeongezeka 14,000,000. Sasa ndio mtu mwingine anaweza kusema kisiwa kidogo. Hapana! Hata kwa kwenda *ratio* kwa kisiwa kile tuzidishe mara 20 ongezeko lao la laki moja ingekuwa milioni ngapi tumeongezeka sisi ni 2,000,000.

Sasa tufike mahali wataalamu wa idadi ya watu watuambie ukweli, tusifiche. Wataalamu wa Idadi ya watu takwimu tumepewa. Mimi nimesoma kile kitabu cha idadi ya watu tuna *project* tunasema kwamba sasa hivi tuko 37,000,000 halatu tunasema baada ya miaka 2025 tutakuwa watu 63,000,000. Sasa kama kwa tafsiri hiyo mwananchi wa kijijini anasema tufanye bidii tufike 63,000,000, tuseme. Kwani ukimwambia mtu ni vizuri Mtanzania ukiwa na watoto wanne kwani tumekataza watu kuzaa. Hivi tunaangalia uchumi wetu unavyokwenda kwa *rate* ya kupanda ni ndogo kwani tukiwaambia watu ni vizuri Watanzania sasa hivi tupunguze uzazi, tuzae watoto angalau watatu, kwani tunawazuia watu kuzaa.

Mimi nawasifu vijana wa siku hizi hawazai sana, yaani hawaoi mapema, lakini kutokana na mambo yao. Halafu zile sababu za kuzaa watoto wengi sasa hivi hazipo. Watu wa zamani walikuwa wanazaa sana kwa sababu mbili. Moja nipate watoto wengi ili niongeze ukoo, hivi ukiongeza ukoo wa kina Ligallama itanisaidia nini mimi?

Sababu ya pili ilikuwa tuzae watoto wengi ili baadaye wakipata kazi wataniletea mahitaji yangu, yaani matumizi. Siku hizi watoto wanaleta matumizi, wangapi wana watoto hapa wanawaletea fedha, hawaleti siku hizi? Sasa zile sababu hazipo. Kwa hiyo, afadhali Serikali iseme tumekuja na kwanza uzazi wa majira, halafu wananchi wa kawaida bwana wazuri sana wanaelewa upesi sana. Uzazi wa majira miaka miwili mtoto, miaka miwili mtoto. Wakaenda bila *limit less* watu watoto kumi au kumi na ngapi. Serikali baadaye kwa kutokuwa wazi wakaanzisha *system* nyingine kwamba nembo ya nyota ya kijani ilikuwa anakuwa baba, mama na watoto wawili, wa kike na wa kiume. Lengo ni kisaikolojia mwananchi akiona vile kwamba watoto wale wana afya, baba na mama yuko pale wanaona wataelewa kwamba angalau tuwe na watoto wawili tu. Twende tuwaambiwe ukweli.

Sasa tukaja na mipango hiyo uzazi wa mpango afadhali kidogo *we are coming close to that reality*, lakini sasa mpango hatujauainisha tuseme mpango wa namna gani. Sasa ndugu zangu wataalamu wa idadi ya watu wangekuja waseme kabisa kwamba watoto watatu. wangapi. Sio vizuri tutumie neno, ni vizuri tuseme usizae zaidi ya watoto watatu au wanne. Tuseme ni vizuri kufuatana na mahesabu yao watakayofanya tuseme ni vizuri kuzaa watoto wanne sasa hivi sisi Tanzania kitu kama hiki ambao huwezi kushtakiwa na dini yoyote.

Lingine la mwisho nilikuwa naongelea kuhusu Mauritius. Nichukue mfano wa Mauritius kidogo nimekaakaa, nimekwenda tena nchi ile. Ni ndogo sana, urefu ni kilomita 65 upana kilomita 45 labda ni Kibaigwa. Lakini nchi nzima imejazwa miwa, mahali hamna miwa kuna nyumba. Lakini wale watu wamekuja kuona kwamba bei ya sukari ilipoanza kuwachezea wakasema tui-*diversify*, wana *jewel industries* kubwa kuliko sisi. *I would expect* kwamba *Tanzanite* Arusha pale tungekuwa na kiwanda kikubwa cha *jewel* lakini kiko Mauritius na hawa wanazaa watoto nilipoangalia familia watoto ni wawili tu ndiyo maana unakuta 100,000 kwa miaka 20.

Nije kwenye kilimo. Ili tuweze kuepukana na mambo haya tu-*balance.* Hatuwezi kuuwa watu lakini tuweke mkazo kwenye kilimo. Kilimo ndio kitatuokoa sisi. Sisi wengine wilaya yetu kwa mfano mimi ya kwangu ina mito 38, ina *flow* mwaka mzima, ardhi nzuri sasa inaibuliwa miradi sijui kwa kutaja tu, miwili jamani ya umwagiliaji maji tutafika kweli? Mimi nimekuwa mwalimu wa kilimo na mimi mwenyewe nimelima. Nawafundisha watu kilimo katika mikutano yangu yote ya siasa jinsi ya kulima mpunga. Mimi nimewaambia hamna ku-*broadcast* na katika miaka mitatu nafikiri nitafanikiwa. Nakwenda na nyenzo kabisa, vipimo sentimita 20 kwa 20 kwani hamna fani ya kilimo kwa miaka 45 nije nifundishe mimi Mbunge.

Kwa hiyo, kama tutagawana kama maeneo fulani kwa mfano mimi nilime mpunga, Kyela alime mpunga, Shinyanga walime mpunga lakini Shinyanga mpaka wapate mvua, wa uhakika ni sisi. Tugawane maeneo kwamba wewe fanya hivi. Kwa mfano hapa Dodoma zabibu zetu hapa Dodoma zina sifa kwamba sababu jua linawaka kutwa nzima, zina uhakika linawaka kwenye lile tunda kumbe ndio sifa ya kuwa na zao la zabibu. Sasa watu wa Dodoma wangejua, wangechangamkia hilo. Lakini tugawane, hatuwezi kulima kila mahali mpunga, huwezi kulima Dodoma mpunga. Nitalima mimi tu na Kyela na Shinyanga mvua ikiwa nzuri na Ulanga watalima mpunga. Tandahimba mnalima mpunga! Sasa kilimo ndio kinavyotakiwa.

Katika kilimo mwaka jana nimeangalia katika matumizi ya Serikali Mfuko wa Pembejeo, fedha zimebaki. Fedha za pembejeo zimebaki. Mimi naomba kuanzia mwaka huu mnijaribu mimi basi. Mimi ni *banker, ex-banker* ni mwaminifu najua upembuzi. Naomba watu wangu wakopeshwe, mimi ndiyo mdhamini, Serikali inanidhamini mimi iniangalie nitakopesha kwa watu ambao watalipa. Ebu tujaribu Wilaya ya Kilombero kidogo. Naomba Waziri wa Fedha, Waziri wa Kilimo mnijaribu mimi niwape watu wangu mikopo tuanzie na matrekta nipeni 10 tu baada ya mwaka mmoja mimi nitawarudishieni fedha. Kwa sababu bila nyenzo huwezi kulima. Mimi nafundisha kilimo bora cha mpunga lakini tunahitaji nyenzo za kulimia sasa. Matrekta, *power tillers* nilishaongelea wakati fulani, tukopesheni. Sasa fedha zinarudi ni shilingi bilioni 3.1, nafikiri tungerudisha shilingi bilioni moja ya mfuko wa pembejeo, watu hawakukopa. Tukopesheni sisi, dhamana mniweke mimi Mbunge. Wapeni watu wangu mikopo, dhamana mimi. *(Makofi/Kicheko)*

Kilimo hasa cha umwagiliaji mito 38 haikauki, wapi? Wilaya gani? Niambieni hapa! Niambieni, ndiyo Wilaya yangu hiyo sasa! Tutakwenda tu, lakini hamna njia ya kusema.

**NAIBU SPIKA:** Naona wamekusikia utapewa tu.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Awali ya yote, naomba nichukue fursa hii kuipongeza kwa dhati kabisa Kambi ya Upinzani kwa hotuba yake nzuri ambayo imeonyesha mjadala wa bajeti unaweza ukawa mzuri. Iwe changamoto tu kwa wenzetu, sio kwamba tunashindana, ila ni katika kusaidiana ili kuweza kusogeza gurudumu la maendeleo mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kuchangia, nataka nitoe angalizo dogo tu. Ninatoa angalizo kwa sababu tunaamini kwamba Bunge ni chombo ambacho kinaheshimika sana. Jana Mheshimiwa Dr. Slaa alisoma taarifa fulani ambayo nadhani wengi wetu tunayo. Inawezekana hiyo taarifa ina ukweli au inawezekana hiyo taarifa sio sahihi. Lakini ina mambo nyeti sana yanayohusiana na nchi yetu. Naamini kama Mbunge badala ya ku-*neutralise,* kutaka kile ambacho kimesemwa kionekane ni uongo ni vizuri Wabunge wakiwa wanachangia waonyeshe nia ya Serikali kufanya uchunguzi

kuhusiana na hilo suala sababu linahusiana na fedha nyingi sana ambazo zimepotea na ni fedha za wapiga kura wetu ambao tunawaongezea kodi hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuchangia kuhusiana na matamko ya viongozi wetu ambao wamekuwa wakiyatoa sasa hivi kwamba wananchi wajifunge mikanda. Lakini nakumbuka kwenye Kampeni za Uchaguzi mwaka jana, wananchi waliambiwa wataletewa maisha bora. Sasa kama tungekuwa tunatumia hizi *statement* za fungeni mikanda halafu mnichague, nadhani picha ingekuwa tofauti. Kwa hiyo, kuna umuhimu sana wa kuwa tunasema kile ambacho tunakuja kukitenda. Sio kule tunaomba picha tofauti mwaka mmoja baadaye tunaanza kuwaambia lugha nyingine za kufunga mikanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze moja kwa moja na kuchangia kuhusiana na ongezeko la kodi ya mafuta. Mimi najaribu kuzungumzia kulingana na kipato cha watu wa chini. Sitazungumzia katika *thinking* ya Mbunge au *thinking* ya mfanyabiashara. Nafahamu kwamba kima cha chini cha Mtanzania kwanza kilikuwa Sh. 60,000/=, naambiwa sasa hivi ni Sh. 75,000/= huyo ni mtumishi wa umma. Kima cha chini cha mfanyakazi ambaye sio mtumishi wa umma nikimaanisha *Private Sector* ni Sh. 48,000 kwa mwezi. Sasa kwa bei ya usafiri tu wa daladala wa sasa hivi mtumishi huyu wa umma anatumia karibu Sh. 40,000/= kwa nauli kabla ya haya mabadiliko ya sasa hivi ambayo tutakuja kuyapitisha.

Sasa tumekuwa tunajiuliza, huyu mtu ambaye karibu mshahara wake mzima anatumia kwa ajili ya usafiri, hapo ondoa hizi shule ambazo wanafukuzwa na mgambo kwa ajili ya kwenda kuchangia, ondoa za ambao sasa hivi tunaambiwa ndiyo hatua inayofuata wananchi kujichangia kutengeneza zahanati. Kwa hiyo, naona kuna umuhimu wa Serikali wakati inafikiria wapi inafanya mipango yake iangalie lile daraja la chini tusije tukawa tuko huku juu tuna-*assume* kila kitu kiko hivyo kumbe kuna watu wengine ambao wako chini, *they cant afford* kabisa kulipa hivyo vitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kuhusiana na suala zima la hizi kodi za magari, ni kweli sisi tunapenda mambo rahisi na kwa kuwa sasa hivi Dar es Salaam kuna foleni sana, imeonekana kwamba kumbe kuna magari mengi. Sasa njia rahisi ya kuongeza kipato ni ya kutoza kodi yale magari zaidi. Lakini wanasahau kwamba kumbe yale magari asilimia 90 ni mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, unakuta mtu amekwenda kuanza kazi amepata mkopo wake ndiyo anajidunduliza kwa mwezi alipie ule mkopo ili aweze kulipa lile deni *in full.* Kwa hiyo, tusiwe tunafikiria tuna *think small* tujaribu ku-*think big*. Ndiyo maana sisi kama Kambi ya pili tunatoa *alternative*. Sisi tulifikiria wenzetu *at least* watupongeze kwa hatua ambayo tumeumiza vichwa vyetu kuambiwa jamani *next time* tumieni (a), (b), (c)( e) (f) (g) ili sasa usije na fedha za ndani trilioni tatu, zije tano na sisi tulifanya kwenye makisio ya chini. Kwa hiyo, tunajua hotuba yetu ya *next time* tunaweza tukaja hata na trillioni 10, *we will be surprised*. Lakini ndiyo hivyo tunafanya kazi, tunataka nchi yetu isonge mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumzia kukusanya kodi, tunazungumzia pia na matumizi. Yaani naamini kabisa kwamba Watanzania watafarijika wakiona kwamba wanakusanyishwa kodi halafu hizo fedha zao zinatumika vizuri. Nimebahatika kupitia ripoti kadhaa za Mkaguzi Mkuu wa Serikali katika miaka michache iliyopita. Katika ripoti ya mwaka 2002/2003 Sh. 65,000,000 zilikwenda chini. Katika ripoti ya mwaka 2003/2004 shilingi bilioni 82 zilikwenda chini.

Nakumbuka majuzi hapa wakati nakuja kuleta Muswada wa Matumizi ya Ziada kulikuwa kuna *difference* katika matumizi ya ziada shilingi bilioni saba. Tumewauliza Mawaziri hapa wakashindwa kutujibu. Tunatarajia sasa hivi wamekuja na majibu, hatujui kama yatakuwa yametengenezwa ama kwa *really,* lakini tunatarajia sasa hivi watakuja kutujibu. *(Makofi)*

Mwaka 2004/2005 shilingi bilioni 203 zinazidi kuongeza. Mwaka 2005/2006 shilingi bilioni 273. Sasa tunajiuliza, hawa Watanzania ambao wanaambiwa watozwe kodi ambao ni *majority* ni masikini wanajipindapinda, wanalipa kodi, zinakuja zinaishia kwenye mchanga. Tumefanya utafiti, inaonyesha kabisa hiki kiasi kilichopotea mwaka 2005/2006 kwa Serikali Kuu peke yake kwa sababu ukijumlisha na Serikali za Mitaa ndiyo inafika shilingi bilioni 273.

Kwa Serikali Kuu peke yake ambayo ni shilingi bilioni 242 inaweza kulipa walimu 160,000 kwa mwaka mshahara. Hizi hizi fedha zinatosha kununua vitabu 1,000,000 na hizi hizi fedha zinatosha kujenga Ofisi za Serikali na maktaba kila kijiji Tanzania. Sasa tunakuwa tunajiuliza kama tunaweza tukafanya mambo makubwa hivi kwa hizi fedha chache kwa nini hawa watu ambao wanafanya hujuma hizi fedha wanaachiwa. Rais amesema kabisa, wale watachukuliwa hatua. Tunatarajia basi tuone nani amechukuliwa hatua au amesema zimetumika kwa vigezo gani, hatuoni mnakuja kutukusanyia kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kwenye hii ripoti ya Mkaguzi kuna hiki kitu ambacho kinaitwa akaunti za Benki zisizotumika. Hii inapatikana ukurasa wa 87 kwa *reference* kama utataka. Ukiangalia unakuta akaunti zimefungwa. Kuna hii iliyofungwa mwaka 1995 ina shilingi bilioni tano ndani. Kuna hii imefungwa mwaka 1997/1998 ina shilingi bilioni 100. Taarifa ambazo mimi ninazo, hawa wezi wanatumia hiyo *advantage* wanafunga akaunti wanasubiri mambo yakiwa kimya wanakuja wanazivuta.

Sasa nataka nijue hizi akaunti ambazo zimeonekana zimefungwa hapo na zenyewe mabilioni zimeingizwaje katika bajeti hii ili hata kama ikienda Miundombinu tujue kwamba fedha zimekwenda wapi. Sio tunaambiwa akaunti zimefungwa halafu zina fedha *then what?* Kwa hiyo, natarajia Mheshimiwa Waziri atanipa majibu. Haiingii akilini kabisa, tunawaambia wananchi wafunge mikanda wa kati sisi huku juu tunafaidi. Nchi yetu sote, lazima sote tufaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija moja kwa moja kwenye hoja yetu kama nilivyosema, sisi tuna *think big* hatu *think small.* Kuna Mheshimiwa Mbunge hapa alikuwa anaongea kuhusiana na miundombinu akafanya *reference* nzito alizosema

miundombinu, miundombinu! Ni kweli kabisa Mheshimiwa Zitto anakubaliana na hiyo hoja ya miundombinu lakini sisi tunasema tuongeze wigo wa kodi ya mapato ili hiyo miundombinu ambayo tunaisema isiwe kwa kuwakaba hawa wananchi ila kwa kutafuta *sources* nyingine za *income.*

Kwa hiyo, watu wasije wakajenga picha kwamba watu tuko *against* miundombinu sio kweli. Tunasema mfikirie kwa mapana, sio mnafikiria kwa ufupi tu. Kama mmefanikiwa kusoma taarifa yetu ya Kiongozi wa Kambi ni nzuri ni *productive.* Mkiitumia *next year* najua mtakuja na *proposal* nzuri sana ambayo itakuwa pana zaidi. Tutafurahi mki- *appreciate.* Tutashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimejaribu kufanya tu utafiti mdogo kwa kuangalia kwa jinsi gani tunapoteza fedha. Nikija kwenye suala zima la uvuvi taarifa zinaonyesha kwamba leseni ya uvuvi, sisi tunatoza dola 20,000. Sasa wakati Somalia nchi ambayo haina hata inatoza dola 300,000. Sasa mimi nadhani kipindi kimefika kujua kwamba inabidi tuanze kufanya kazi tusifikirie kama ambavyo tulivyokuwa tunafikiria miaka 10 iliyopita. Inawezekana labda *age* imekwenda inakuwa ngumu lakini naamini kuna vijana wengi huko wanaweza wakasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwenye suala zima la misitu, kuna taarifa ya asasi ya *Traffic* na taarifa zaidi ataleta Waziri wetu wa Mambo ya Maliasili inaeleza kwamba kwanza mwaka 2004 Serikali ilipata asilimia nne tu ya mapato ya misitu ambayo inatakiwa ipate. Hicho ni kitu cha aibu. Kwa hiyo, kuna umuhimu wa kujijengea utamaduni wa kusoma taarifa na kuzifanyia kazi. Vile vile kuna rekodi mbili tofauti.

Kuna rekodi ambayo inapatikana hapa maliasili Tanzania na kuna rekodi ambayo inapatikana forodha China. Rekodi ya Maliasili Tanzania inaonyesha kwamba *cubic metre* 18,000 ndiyo ziliuzwa na ziliuzwa kwa dola 150. Rekodi za forodha China zinaonyesha kwamba ziliingia *cubic metre* 90,289 na ziliuzwa kwa dola 450. Kwa hiyo, huu ni upotevu mkubwa wa fedha na hapa nimetoa mfano mdogo tu. Ukisoma hiyo ripoti nzima inatisha na inawezekana misitu ikawa inachangia kwa kiasi kikubwa sana cha bajeti. Kwa hiyo, kuna umuhimu sana wa kufikiria kwa mapana kama ambavyo tumesema. Kuna umuhimu pia wa kusoma hotuba zetu na kuzipembua na kuzifanyia kazi, nchi yetu itasonga mbele. Wote tuna nia nzuri, hakuna mwenye nia mbaya na nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia, naona kengele ya kwanza imegonga ni kuhusiana na utegemezi wa kasma ya maendeleo. Sisi tumependekeza kupunguza kwa utegemezi kwa asilimia 42. Nimeona madhara ya huu utegemezi kwanza kwa ripoti yenyewe ya Mkaguzi Mkuu na vile vile kwa ripoti ambazo nimezipata kwenye Kamati. Mimi niko kwenye Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Kuna hiki kitu kinachoitwa *Legal Sector Reform* na ni programu. Sasa imesikitisha kuona kwamba mwaka 2006/2007 imeshindwa kufanyika kitu cha maana kwa sababu asilimia 99 ya fedha tulikuwa tunategemea nje na hazijaja.

Kwa hiyo mwaka jana hiyo *Legal Sector Reform Programme* ni kwamba ilikuwa imeshindwa, sasa hayo ndiyo matatizo yenyewe ya kutegemea vyanzo vya nje kwa ajili ya kufanya shughuli zetu za ndani. Sote tunaona kila mtu analalamika, Mahakimu, sijui Mahakama hivyo ndivyo vitu vilikuwa vinaweza kusaidia. Sasa tunategemea nje madhara yake ndiyo hayo.

Vile vile nikiangalia katika kasma ya maendeleo kwa mujibu wa ripoti ya *CAG* ukurasa wa 74. Inaonyesha kwamba makisio ilikuwa 1.3 trilion. Matumizi ilikuwa shilingi bilioni 800 pungufu ilikuwa shilingi bilioni 500 pungufu kwa maana hazikuja. Kwa hiyo, asilimia 37 ya fedha ambazo zilikuwa kwa ajili ya maendeleo hazikuja. Kwa hiyo, hii ni hatari kabisa. Sasa mimi ushauri wangu ni kwamba Kambi tumeweza kuonyesha uwezo wa jinsi gani bajeti yetu inaweza ikaongezwa na nashauri kwamba ni muhimu mkayazingatia na kama kuna *consultation* yoyote mnayohitaji kuna vijana wamejaa hapa tutasaidiana ili kusogeza gurudumu letu mbele. Nashukuru sana.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, natumia kifungu cha 55 fasili ndogo ya 3, mchangiaji aliyetoka kuzungumza sasa hivi ametumia maneno ambayo pengine naomba unisaidie kwamba hao wenzetu waliotayarisha bajeti hii hawafikirii sana, *they don't think big.* Sasa yale maneno nafikiri kama vile viongozi wa Chama cha Mapinduzi na Serikali yake waliyotayarisha bajeti hii pengine wana mawazo mafupi kwa maneno yake mwenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ni sahihi kweli! Naomba mwongozo wako.

**NAIBU SPIKA:** Tunapojadili unaweza ukasema neno lolote. Anachokisema kwamba yeye ana hoja ambayo tunaweza kuifikiria. Kwa hiyo, sikuona kwamba ni maneno yenye karaha. *(Makofi)*

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hoja ya hotuba mbili ambazo ziko mbele yetu.

Lakini kabla ya hapo kwanza napenda nitoe shukrani na pongezi za dhati kwa hotuba mbili za Kambi ya Upinzani ambazo kwa kweli zimeleta mambo ambayo Serikali inaweza kuyatumia katika bajeti ijayo. Hii si kitu mbadala lakini kingeongeza. Nafikiria yale mazuri tunaweza kuyafuata na yale mabaya tukayaacha.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hotuba mbili hizi kusomwa wiki iliyopita Watanzania wengi walipata nafasi ya kuzichangia wakiwemo wataalamu mbalimbali wana uchumi, wana siasa Watanzania wa kawaida. Mawazo ya wengi katika hao waliochangia ni kwamba bajeti hii inawakatisha tamaa. Wanasema kwamba ile kauli mbiu ya Serikali ya Awamu ya Nne kwamba maisha bora Tanzania kwa kweli inakuwa ni ndoto, haiwezi kupatikana. Lakini wameleta *criticism* zao hizo kwa kuangalia hasa juu ya upandishwaji wa ushuru wa bidhaa ya mafuta. Yako mambo mengi ambayo wameangalia, lakini hilo lilikuwa ni la msingi kabisa. Wamesema kwamba ukipandisha mafuta maana yake unapandisha bei ya vyakula vyote. Ukipandisha mafuta maana yake unapandisha bei ya usafiri na usafirishaji na vile vile unaharibu mazingira kwa maana

kwamba watu wengi watahama kwenye mafuta wataelekea kwenye kuni. Mazingira yakiharibika maana yake maji yatakosekana, yakikosekana maji maana yake kilimo kitakuwa hakipatikani kwa maana kwamba itakuwa ni ukame wakati huo huo umeme utakuwa haupatikani tutarudia pale pale katika mwaka uliopita kwamba uchumi unaharibika kwa sababu ya umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono mawazo hayo na namwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha aangalie ili ushuru wa kodi ya mafuta auondoe kabisa kwa sababu itakuwa ni vigumu sisi kama Wabunge kuunga mkono bajeti ambayo wananchi wengi wanaiona kwao ni matatizo. Kwa ushahidi tulioupata hapa kwamba kuna baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wameletewa *message* hapa hapa na *e-mail* kuonyesha kwamba hawakuridhika na hali halisi. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha ushuru huu wa mafuta ya taa na petroli, dizeli auondoe atafute njia nyingine za kuongeza mapato.

Mheshimiwa naibu Spika, baada ya Serikali kujiondoa katika shughuli za biashara lakini kazi kubwa iliyobakia ilikuwa ni kukusanya kodi. Lakini suala lilikuwa kodi ikusanywe wapi na wapi na itumike vipi na vipi? Yako maeneo ambayo Serikali ilipashwa kukusanywa kodi lakini inaelekea haikusanyi kabisa au inakusanya kidogo mno.

Mheshimiwa Mongella hapa alitoa takwimu za kwamba wale ambao wanapaswa kukusanya kodi ni wachache mno ambao wanalipa kodi. Hili ndilo tatizo kwamba Watanzania wengi wale ambao wanapaswa wakusanye kodi hawapaswi, hakuna usimamizi mzuri wa ukusanyaji wa kodi. Lakini vile vile yako maeneo ambayo yangepaswa kusamehewa kodi, lakini hayasamehewi.

Kwa hiyo, la msingi hapa linaloonekana hapa ni kwamba suala zima la usimamizi wa ukusanyaji wa kodi bado linahitaji kuangaliwa upya ili Watanzania wapate mapato ili ile kauli ya lazima tufunge mikanda isije. Kwa sababu inaaminika kwamba angalau robo tu ya wale ambao wanapaswa kulipa kodi wakikusanya kodi, basi uchumi wetu unaweza kuwa mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi yetu ya Upinzani ilitoa maeneo mengi ambayo yanaweza kuangaliwa kama njia ya kuongeza kodi; na Mbunge aliyekaa sasa hivi ameeleza hayo. Kwa mfano, bidhaa za misitu. Tuna misitu mingi sana hapa na tunavuna mbao na nilikuwa najiuliza wakati Mheshimiwa Diallo alipoingia kwenye Wizara, hii alikuwa na mapambano makubwa juu ya kuzuia usafirishaji wa magogo kupeleka nchi za nje.

Sasa hivi tunajua kwamba kumbe kulikuwa na mambo ambayo yanafanyika. Kwa *research* ambazo zimefanyika ni kwamba kuna upotevu mkubwa wa magogo. Nchi ambazo zinanunua magogo ni tatu kubwa. Ukiangalia ni China, India na Japan. Lakini *research* ambayo nimefanya kwa China peke yake tunapoteza kiasi cha dola za Kimarekani 52.8. Sasa kama tutakwenda kwenye nchi nyingine kama Japan au India

sijui hali itakuwaje. Kwa hiyo, mimi nataka hilo suala liangaliwe vizuri na usimamizi uwe mzuri ili rasilimali hii ya misitu tuweze kuihifadhi na itusaidie katika uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, kama alivyozungumza Mheshimiwa Mbunge aliyepita ni kwamba hali ya uvuvi; kuna meli nyingi zinavua na samaki wetu wanaibiwa. Kuna nchi ambazo uchumi wao unategemea samaki tu. Kuna nchi ambazo zinalisha, zinafanya kampeni ili watu wao wale samaki na samaki zinakuwa bei rahisi. Sisi hatuli samaki kwa sababu hatuna vyombo vya kuvulia vya kutosha, lakini hivyo hivyo zile meli ambazo zinatoka nchi za nje zinavua samaki zinaondoka na samaki. Nadhani baada ya kupitisha ile Sheria ya *Deep Sea Fishing* usimamizi sasa utakuwa mzuri zaidi. Lakini suala kubwa la hapa leseni ambazo zinatolewa, kuna meli zisizopungua 193 kama tulivyoambiwa kwenye Bunge hili ambayo yanavua samaki, meli kutoka nchi za nje. Lakini suala kubwa ni kwamba: Je, leseni zinazotolewa pale zinatosheleza? *(Makofi)*

Leseni za sasa ni Dolla za Kimarekani 18,000 tu ambapo nchi jirani hapa kwa mfano Somalia ambapo hata Serikali haina, lakini wao wanatoza Dolla 100,000 kwa meli moja kwa mwaka na kama tuna meli 193 hapa ni fedha kiasi gani ambazo tungeweza kukusanya. Lakini vile vile katika meli hizo kuna mambo ambayo yanaitwa kutoza mrahaba. Wanavua samaki wengi sana na inasemekena meli moja inaweza kuvua samaki tani 1000 hadi 1500 kwa siku. Sasa kiwango hicho cha samaki ni kikubwa sana na tungeweza kutoa mrahaba na sisi tumependekeza angalau *ten percent* ya mrahaba utolewe kwa meli hizo na hesabu ambazo nimefanya haraka haraka hapa tunaweza kukusanya sio chini ya Dolla milioni 75 kwa kazi hii. Hali kadhalika tumependekeza *Fishing poss* kwa sababu hizo zinaweza vilevile tukazitumia kuuza baadhi ya mali zetu, maji au mafuta au chumvi na vilevile kuwapa ajira vijana wetu. Kwa hiyo, haya ni mambo ambayo yako mengi ambayo tumependekeza lakini haya ni mifano michache ambayo Serikali inaweza kuyatumia katika Bajeti ijayo ili kuongeza mapato ili isije ile kauli ya lazima tufunge mikanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni kuhusu ushuru wa baadhi ya mazao au bidhaa zetu ambazo zimependekezwa. Kuna vitu kama tumbaku na sigara za aina tofauti na vinywaji vikali. Suala la tumbaku nafikiri tunalijua, sote tumefanyiwa semina Bungeni hapa kwamba tumbaku inaathiri afya na kuna kampeni ya kuzuia utumiaji wa tumbaku. Lakini kodi hizi za tumbaku mimi nahisi bado hazijatosheleza. Tunayo nafasi ya kuendelea kuongeza kodi. Moja, kwa ku-*discourage* uvutaji wa sigara.

Kuna rafiki yangu mmoja aliwahi kusafiri katika nchi za Ulaya akakuta pakti moja ya sigara itamgharimu sio chini ya shilingi 15,000. Kwa bei hiyo, yeye mwenyewe akaamua kuachana na sigara. Nafikiri tukiongeza bei ya sigara tutakuwa tumemsaidia sana mvutaji wa sigara kuacha, lakini vile vile tunaongeza mapato katika Bajeti yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile mambo ya vinywaji vikali na bia, Waheshimiwa Wabunge wengi hawatafurahi; lakini ni ukweli usiopingika kwamba ulevi unaharibu afya ya binadamu. Kwa hiyo, tukiongeza kodi katika ulevi wa aina zote iwe

bia iwe vinywaji vikali iwe *wine* na nini kwa kweli tutaongeza kodi na tutawasaidia baadhi ya watu ambao wamezama katika mambo hayo ili kuokoa afya zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningependa kuligusia kwa haraka haraka ni kupitisha bidhaa bila ukaguzi. Waheshimiwa wengi wamelizungumza hilo. Mimi nafikiri huo ni mtego, kwa sababu kila mfanyabiashara kazi yake ni ku-*maximize profit*. Wafanyabiashara ambao leo tunawaona ni wazuri lakini kesho watageuka watakuwa sio wazuri.

Kwa hiyo, kuwaachia tu makontena yapite pale katika milango ya kijani mekundu na nini, sio busara kwa sababu binadamu ni binadamu na anaweza kubadilika wakati wowote kutokana na mazingira. Sasa mimi napendekeza kwamba mizigo yote ichekiwe vizuri ili tuhakikishe kuna nini na kiasi gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, jingine ambalo ningependa kuchangia ni hali ya uchumi na utulivu wa kisiasa. Katika Hoja ya Waziri wa Mipango Uchumi na Uwezeshaji, amesema kwamba nchi za maziwa makuu kwa mfano uchumi wake umeshuka kwa wastani kutoka asilimia 6.2 mpaka asilimia 5.8 na sababu ambazo amezitoa Mheshimiwa Waziri ni ukame, ongezeko la bei ya mafuta, vita na hali mbaya ya kisiasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuzungumza hili in *particular* katika kesi ya Zanzibar. Hali ya kisiasa ya Zanzibar sio nzuri. Ukame tunao, ongezeko la bei ya mafuta upo, hatuna vita, lakini kuna hali mbaya ya kisiasa na hili linajulikana, linaeleweka na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri aliona hilo mwanzo alipokuwa akifungua Bunge hili na akaahidi kwamba atalifanyia kazi ya kutosha lakini kwa bahati mbaya hadi leo mambo tunaona yanakwenda polepole mno. Hatusemi kwamba tumekata tamaa, lakini tunahimiza kwamba suala hili lisifanyiwe mchezo ikiharibika au hali ya siasa kwa sababu imeharibika uchumi wa Zanzibar hauwezi kukua. Zanzibar sasa hivi hakuna *circulation*, mambo sio mazuri katika uchumi. Uchumi wa Zanzibar umeanguka mno.

Kwa hiyo, ili kuisaidia Zanzibar ni lazima kuhakikisha kwamba hali ya kisiasa Zanzibar inatengemaa. Vinginevyo itakuwa ni ndoto Zanzibar kupata maendeleo yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni juu ya hali ya uchumi. Sisi au uchumi wetu kama alivyozungumzia jana ni uchumi wa kijamaa. Lakini tuangalie ziko nchi za kijamaa kuliko sisi ambazo zimepiga hatua kubwa katika uchumi kwa mfano China. China leo inatikisa madola makubwa kwa sababu uchumi wake umekuwa mno. China leo inaongezeko la asilimia 27 ya mauzo ya nje. Inashinda Marekani, Ujerumani na nchi nyingine. Sasa sisi tuna matatizo gani? Kweli Ujamaa tuna u-*practice* lakini mbona hatufanikiwi katika uchumi? Uchumi wetu bado unakwenda polepole mno. Kwa hiyo, napenda hili liangaliwe vizuri, kuna tatizo gani katika uchumi? Wachumi wanatupa maelezo mazuri lakini bado hayatoshelezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningependa kulichangia ni kupeleka madaraka kwa wananchi katika Halmashauri au katika Wilaya au hiyo *(D by D)*. Tunajua

kwamba asilimia 70 ya Bajeti inakwenda katika Halmashauri za Wilaya kwa kupitia mifuko mbalimbali. Tatizo hapa ambalo hata Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi alilieleza kwamba; tatizo za Halmashauri ni kwamba uwezo wa Halmashauri ni mdogo mno na hii imejidhihirisha katika ripoti ya *CAG*. Ikiwa asilimia 70 ya Bajeti inakwenda katika Halmashauri na Halmashauri zenyewe hazina watendaji wazuri na ripoti imeonyesha sasa tunategemea nini? Mimi nafikiri hili ni suala la sera na inabidi Serikali liangalie vizuri kwa sababu yaliyotokea mwaka huu yanaweza kujirudia mwaka ujao.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kwa haraka haraka, nizungumzie hali ya kilimo. Kilimo ndiyo tunasema uti wa mgongo wa nchi hii. Kilimo kinachangia zaidi ya asilimia 40 ya pato la kigeni. Kilimo kinaajiri zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania, lakini kilimo katika Bajeti hii kimepewa asilimia 6.2. Yaani ni chini ya yale makubaliano ya *SADC* kwamba angalau bajeti zetu zi-s*u*pport kilimo kwa asilimia 10. Sasa watu wamechangia hapa wamesema kwa kweli kilimo kimedharauliwa. Zamani kipaumbele cha Serikali kilikuwa kilimo, lakini sasa hivi kimekuwa elimu na miundombinu, afya na maji ni sawasawa lakini je, hiki kilimo tunakiangalia vipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa kwa maelezo niliyotoa siungi mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MAIDA HAMADI ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa na mimi kuchangia hoja hii iliyoko mbele yetu. Hoja ya Waziri wa Mipango Uchumi na Uwezeshaji na Hoja ya Waziri wa Fedha ambayo ni Bajeti ya mwaka huu 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika kwanza nipende kuwapongoza Mawaziri jinsi walivyoweza kuwasilisha vizuri Bajeti hii ya mwaka 2007/2008. Naomba nitoe shukrani za pekee jinsi Serikali ilivyoangalia katika kuandaa Bajeti hii kuangalia mambo makuu yaliyoainishwa katika Ilani ya CCM ya mwaka 2005. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niipongeze Serikali kwa kujipangia mikakati katika Bajeti hii kwa kuzingatia mwongozo na mkakati wa kudhibiti ya nje na kujiwekea utaratibu wa kukopa nafuu na stahimilivu ili kuzidi kuleta maendeleo nchini. Pia niipongeze tena Serikali kwa kuweka utaratibu mpya wa pensheni kwa wastaafu nchi. Lakini napenda kuishauri Serikali kuwa mstari wa mbele zaidi katika kuhakikisha kwamba haki za wastaafu zinasimamiwa vizuri katika kuzipata haki hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niipongeze Serikali kwa kuona umuhimu wa kupitia maboresho na mageuzi ya sekta ya fedha kwa kuona kuwa mikopo inayotolewa na mabenki ya biashara inatolewa kwa gharama kubwa na kuweka mikakati ili kupunguza tofauti ili kuwawezesha wananchi wa kipato cha chini kuweza kukopa mikopo kwa masharti nafuu. Napenda pia Serikali niipongeze Serikali kwa kuweka kipaumbele katika masuala ya ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la ajira, itakukumbuka kuwa katika nchi yetu, mara nyingi huwa tunachukua takwimu za wanafunzi wanaojiunga na shule za awali, sekondari na vyuo na kutoa takwimu mbalimbali katika utendaji wa kazi zetu za Serikali. Lakini pia Serikali haiangalii ni wangapi ambao wamemaliza shule hizo na tumewajiri katika nafasi gani.

Kwa hiyo, naiomba Serikali ingalie katika masuala ya ajira, ni kweli tumelipanga suala hili la ajira, lakini tuangalie ni wangapi wanamaliza shule? Ni wangapi tumewaajiri na wangapi watawekwa katika mpango wa ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika afya kuna vituo mbalimbali vya kujitegemea ambavyo wananchi mbalimbali huwa wanakwenda kujisomea kwa mafunzo mbalimbali katika vyuo hivyo na sasa hivi upo mlolongo mrefu wa Watanzania ambao hawajaajiriwa katika sekta hizi za afya, wapo waliochukua masuala ya Udaktari, Unesi na mengineyo. Kwa hiyo, naiomba Serikali ingalie vyema katika suala hili la ajira kuwapatia ajira wananchi wetu wa Tanzania. Yaani iwe mbele katika kushughulikia masuala haya ili kusiwepo malalamiko katika kutoa ajira hizi za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumzie suala la uwezeshaji wananchi kiuchumi. Ni kweli kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hotuba yake ya Bajeti iliyopita ya mwaka 2006/2007 alihutubia Bunge na kusema kuwa kila Mkoa utawezeshwa shilingi bilioni moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuipongeze Serikali jinsi ilivyojitahidi ili kuwawezesha wananchi kujiendesha kiuchumi, yaani hayo ndiyo maisha bora kwa kila Mtanzania na kweli yanawezekana. Lakini sasa jinsi ya kuzipata fedha hizo kwanini kumekuwa na ugumu katika kupata mikopo hiyo?

Wananchi wengi wanalalamika jinsi ya kuzipata fedha hizo. Kwa hiyo, naishauri Serikali katika awamu hii ya pili iangalie vizuri jinsi ya kuwezesha wananchi hao. Kwa sababu malalmiko ya Watanzania ni mengi na malalamiko wanailalamikia Serikali kwamba Serikali yao haiwajali, kwa hiyo, watendaji wachache wasiweze kutuwekea kasoro ndani ya Serikali yetu hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa uwezeshaji wananchi kiuchumi kwa upande wa Zanzibar Mheshimiwa Rais alitamka katika Sherehe za Mapinduzi kuwa kwa upande wa Zanzibar tutawezeshwa shilingi milioni 100.

Lakini nataka nieleweshwe au nipewe ufafanuzi kwa upande wa Zanzibar ni lini au juzi Mheshimiwa Naibu Waziri alipokuwa akijibu swali Bungeni alisema kuwa Zanzibar itajumuishwa katika mtiririko wa pili, yaani awamu ya pili ya mikopo hiyo ndiyo ambapo watawezeshwa hawa wananchi wa Zanzibar kwenye mjumuisho huo.

Kwa hiyo, nauliza hivi; jinsi ya kuwekwa utaratibu huu utakaotumika ni utaratibu gani ambao utatumika jinsi ya kuwawezesha kupata mikopo wananchi hawa wa Zanzibar? Kwa sababu utaratibu tulioelezwa ni kuwa mikopo hii itapitia *NMB* na *CRDB*,

kwa upande wa Zanzibar hatuna Benki ya *NMB* wala *CRDB*. Benki ya *NMB* iko Pemba tu, kwa maana hiyo mikopo hii tujulishwe itapitia *SMZ* Benki au itapitia *NMB* iliyoko Pemba na kwa upande wa Unguja watafanyiwa namna gani kwa sababu *NMB* ipo Pemba tu.

Kwa hiyo napenda kumjulisha Mheshimiwa Waziri wa Fedha kuwa aangalie huu utaratibu wa mara ya pili wa kuipa mikopo kila Mkoa. Utaratibu wa Zanzibar uangaliwe kwa makini kwa sababu sasa hivi wanawake na vikundi mbalimbali vya wananchi mbalimbali wamejitolea wameanzisha *SACCOS* na vikundi mbalimbali vya ujasiliamali visivyopungua 200 kwa maana ya kuwa wanasubiri mikopo itakayopelekwa katika Mikoa yao ili waweze kujikwamua kiuchumi. Kwa hiyo, wananchi wa Zanzibar wako katika hali ngumu sana. Naomba mikopo hiyo iingizwe mapema kusiwe na ubabaishaji. Kwa hiyo, naomba Serikali itufikirie Zanzibar ni lini tutaingiziwa mikopo hiyo, huo utaratibu wa awamu ya pili utaanza lini na kwa utaratibu gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nizungumzie ingawa suala hili halikuzungumzwa katika Bajeti yetu, lakini nataka nigusie kidogo suala la rushwa. Suala la Rushwa limekithiri sana katika nchi yetu na itakumbukwa kuwa tulipokaa katika Bunge hili kwenye Kikao cha Saba tulipitisha Muswada wa Kudhibiti Vitendo vya Rushwa.

Nataka niulize hivi, tokea tupitishe Muswada huo, ni wananchi wangapi wamekamatwa au wamepelekwa Mahakamani kutokana na suala hili? Kwa sababu rushwa bado inaendelea katika nchi yetu na bado inaendelea kuitia dosari nchi yetu na imetawala katika vyombo mbalimbali na katika sekta mbalimbali na hasa katika Mahakama. Wananchi ambao hawana uwezo wanakwenda pale ili kupata haki zao. Lakini leo wanatakiwa watoe kwanza ndiyo ambapo washukuliwe. Kwa hiyo, naiomba Serikali ishughulikie sana suala la rushwa, yaani iundwe timu ambayo itapitia kila Wizara hasa Mahakama na Bandari na kupelekwa katika vyombo vya Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Sheria na Katiba alipokuwa akijibu swali Bungeni alisema kuwa huenda Sheria inapopitishwa inawezekana pia sheria yenyewe ikawa na mapungufu au watendaji kuivunja au kuona adhabu yake ni ndogo au pengine labda Serikali pindi itakapokuwa, yaani Serikali haijajiweka tayari kuisimamia sheria hiyo. Kwa hiyo, naiomba Serikali ishughulikie suala hili la rushwa katika nchi yetu, limekithiri na linaendelea kutia doa katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika naomba nizungumzie suala la kupanda kwa bei ya mafuta. Kwa kweli suala la bei ya mafuta liko katika njia panda kwa kweli.

Naiomba Serikali ilifikirie sana suala hili la bei ya mafuta ili kumwangalia mkulima wa kipato cha chini kwa sababu mkulima huyo atakapopata mazao yake hatayapeleka mjini ikiwa hajatumia usafiri na usafiri huo utakuwa na bei kubwa katika kuyapeleka mazao hayo na chakula kitapanda bei na usafiri pia utapanda kwa bei kubwa na matumizi ya nyumbani yatakuwa ni magumu kwa upande wa mwananchi. Kwa hiyo, naiomba Serikali kodi au ushuru ulioongezwa katika masuala ya mafuta hasa ya taa.

Ukipunguza mafuta ya taa ukaacha *diesel* kwa maana usafiri utakuwa upo pale pale. Kwa hiyo, naomba suala la kodi za mafuta lipelekwe katika masuala mengine ili mafuta yawe katika mtiririko wa chini.

Naiomba Serikali kuwa na udhibiti mzuri kwa wafanyabiashara kwa sababu hivi leo wameshasikia bei ya mafuta imepanda hata kabla hawajakwenda kuchukua yale mafuta ambayo yamepandishwa kodi iliyotajwa hapa wao tayari mafuta yaliyomo ndani ya visima vyao wao wanauza kwa bei ya juu. Kwa hiyo, Serikali iwaangalie vizuri na iendelee kuwadhibiti wale ambao wanakwenda kinyume na maadili ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kasi ya upandaji bei ilitakiwa isizidi zaidi ya asilimia nne hadi ifikapo Juni 30, mwaka huu. Lakini kutokana na hili hali na mafuta hii ilivyo, basi upandaji wa bei utazidi hata asilimia saba. Kwa kweli Serikali itufikirie sana suala la upandaji wa bei ya mafuta, yaani iweze kupunguza na iweke katika viwango vya chini.

Pia napenda kusisitiza kuhusu kubadirisha utaratibu wa kupitisha bidhaa bila ubaguzi bandarini. Naiomba Serikali ilifikirie sana suala hili kwa sababu kuna wafanyabiashara ambao sisi tunawaamini na tunawaona ni wazuri, lakini baada ya kupitishwa utaratibu huu, wao wataweza kupitisha zile bidhaa ambazo hazistahili katika nchi yetu na zinatuletea madhara katika nchi yetu na kupitisha kwa utaratibu huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA.** Waheshimiwa Wabunge, kwa mchana huu nadhani tumetosha, lakini tutaendelea baadaye saa kumi na moja. Watakaoendelea wafahamu kusudi wasikosekane. Mheshimiwa Juma Killimbah, atafuatia Mheshimiwa Sevelina Mwijage, Mheshimiwa Vita Kawawa, Mheshimiwa Mohammed Mnyaa, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa na wengine kadri itakavyobandikwa kwenye sehemu ya taarifa. Sasa kama nilivyosema, Hotuba ya Waziri wa Fedha na ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji tunazungumza siku tano na hatuna swala la kupitisha vifungu. Kwa hiyo, wakimaliza kutoa maelezo au ufafanuzi ,basi tunaingia kupiga kura.

Hotuba ya Waziri Mkuu tutatumia siku tano, kwa sababu anaanza TAMISEMI, ndani yake lakini haziwi siku tano zote za kuzungumza tu kwa sababu tunapitisha vifungu. Ndiyo maana nawashawishi wengi wenu msingojee ile hotuba ya Waziri Mkuu, mtakuwa wengi mno kiasi kwamba mtakosa nafasi. Hii ina nafasi zaidi kuliko ile. Kwa hiyo, nawashawishi kwa sababu mazungumzo ni ya aina hiyo hiyo na kama unajua kujipanga vizuri, basi kama utataka ufafanuzi zaidi utaingia kwenye vifungu wakati unapopasa. Lakini mazungumzo, ni vizuri ukazungumza katika hotuba hii kwa sababu hakuna tofauti ya namna ya kujadili.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hivyo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 6.55 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mheshimiwa Jenista J. Mhagama) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea na kadri ya orodha iliyoko hapa Mezani, tutaanza na Mheshimiwa Juma Killimbah, atafuatiwa na Mheshimiwa Savelina S. Mwijage na baadaye Mheshimiwa Vita Kawawa ajiandae. Lakini, naona Mheshimiwa Killimbah hayupo, hivyo namwita Mheshimiwa Savelina Mwijage.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nguvu na kuniwezesha kuweza kusimama hapa kuweza kuchangia katika bajeti hii. Mengi yameshachangiwa na mengi yamechangiwa sana sana na Kambi ya Upinzani. Lakini, nina machache na mimi ya kuchangia kuongeza hasa katika Mkoa wangu wa Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasikitika sana kuhusu jambo hili la kufunga mkanda. Mkanda tuliufunga kuanzia kwenye Vita vya Idd Amin, hasa Mkoa wa Kagera. Sasa nasikitika sana mkanda huo sijui tutafunga mpaka lini!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika sana nimesoma kitabu cha Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, kasema kwamba Mwaka 2006/2007 kabahatika kuweka uzio wa Uwanja wa Ndege. Nasikitika sana uzio mimi sijauona. Sijui wamejenga sehemu gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina masikitiko makubwa sana katika Mkoa huo huo wa Kagera kuhusu usafiri. Usafiri wa majini na barabara, nashukuru sana Wizara ya Miundombinu, fedha walizozipata naomba wajaribu kutusaidia hii barabara ya kutoka Muleba – Lusahunga. Kwa kuwa meli sasa hivi kwenye bajeti ya Serikali, labda hawakuandaa, lakini, angalau watengeneze hiyo barabara, watu wawe wanapitia Geita kwenda Mwanza, inakuwa ni rahisi kuliko kupanda ile meli imezeeka, inaangusha watu kila siku kwenye maji, wakati mwingine inazimika, watu wanabaki kutapatapa. Huko kote ni kufunga mkanda. Mwalimu Nyerere alitueleza tufunge mkanda, tumefunga mpaka akaondoka, hatujaufungua na tumeongeza mkanda mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kagera, Mheshimiwa Waziri Mkuu atakuwa shahidi wangu kwa sababu vijana walijitahidi kujiundia uchumi wao wa kuweza angalau wakiwa wanasema kuchangia shule, inakuwa rahisi, wanapata uchumi kidogo kwenye baiskeli na pikipiki, wanapata pesa kidogo ya kuweza kuchangia. Lakini, mpaka sasa hivi ukifika Mkoa wa Kagera huwezi ukajua kama kuna vijana au kuna mtu yeyote anayeishi pale kwa sababu vijana walikuwa wamechangamka wanafanya hiyo kazi. Lakini, kwa kusikia Mheshimiwa Waziri Mkuu akisema kwamba hiyo sheria itapitishwa.

Nampigia, magoti Mheshimiwa Waziri Mkuu atusaidie hilo jambo, angalau namwomba kwa sababu yeye mabango yanamkuta kila siku kila akiingia Mkoa wa Kagera, mabango anayakuta kwenye ukumbi. Ni kwa sababu ya shida ya uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wamechangia Sekondari na leo hii wanasema kila Kata itakuwa inajenga Zahanati. Sasa wamefunga mkanda, Zahanati hiyo pesa wataitoa wapi katika mkanda huo mkubwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, badala ya kukamata wale kwenye Wizara zinazotengewa pesa wanakula wakubwa, badala ya wao kufunga mikanda, wanakuja kuwafunga wananchi wenye kipato kidogo. Ukiangalia kama Mkoa wa Kagera, sana sana unakuta hakuna umeme. Ukienda kama Kyaka, Karagwe, Muleba, hawana umeme. Leo hii unawaeleza mafuta, watafanya nini? Watatoa wapi pesa ya kununua mafuta. Naomba Serikali iangalie wale wananchi tunaokwenda kuwaomba kura, kuwapigia magoti, leo hii unawapandishia mafuta na unawaambia fungeni mkanda, wafe!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iangalie kilio cha wananchi wenye kipato kidogo hasa Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia kuhusu hali halisi ya kilimo. Mimi nimesoma kutokana na kilimo cha kahawa. Lakini, tangu nimeingia hapa, hii ni bajeti ya pili katika Bunge, sijasikia mtu anagusia kuhusu kilimo cha kahawa Mkoa wa Kagera. Sasa, naomba, nalia mbele ya Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, waangalie wenye kilimo cha kahawa Kagera waweze kusaidiwa. Hata bajeti ikiwa kidogo, angalau wawe wanawatengea kidogo. Hata kama siyo bajeti hii, bajeti inayokuja watukumbuke, siyo kutusahau kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yasije yakaingilia mambo ya siasa. Ukisimama kuongea kutetea Mkoa wako, kutetea nini unakuta inaingilia mambo ya siasa. Mtu anafika mahali akisimama anasema hivi, nyie Wapinzani ndio mnapanga foleni kwa kuchukua posho na wote hatukuomba kura kuja hapa kuchukua posho. Tuliomba kura kuja hapa kutetea maslahi ya wananchi wote, sio Kagera, sio Mwanza na kadhalika. Sisi tunatoka huko kuja kutetea maslahi ya wananchi, siyo maslahi yetu binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Wizara hii kuhusu uwanja huo niliokuwa nimesema mara ya kwanza, angalau kidogo wapanue na kutuwekea lami. Sisi Bukoba, mafuriko ni kila siku. Unakuta uwanja umejaa maji, unakwenda kumpokea Kiongozi wako, Waziri Mkuu, Rais, unashindwa hata mahali pa kukanyaga kwenda kumpokea. Ni aibu kubwa sana. Kwa sababu tuliitwa ushomile na ushomile ulikwisha kwa sababu tumesahaulika na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo sehemu nyingi ndizo nilitaka kuchangia kwa sababu mambo mengi wameshachangia. Narudi kwa Madiwani. Madiwani wetu wanatufanyia kazi sana. Wakati sisi tuko hapa Bungeni wanaofanya kazi sana ni Madiwani. Lakini, ninachoomba, ni kwamba Madiwani angalau na wenyewe wakumbukwe. Angalau wapewe posho au usafiri kwa sababu kuna Mbunge mwingine nimemsikia ameshasema, wawafikirie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naongelea kuhusu afya. Bukoba tuna Hospitali nzuri tu na hii ni safari ya pili naiongelea. Nimeingia kwenye bajeti ya mwaka jana nimeongelea

kuhusu Hospitali ya Bukoba.  Hospitali tunayo nzuri tu, lakini Madaktari hatuna. Naomba kwa kweli Serikali ituangalie. Wasitusahau barabara za Muleba, Karagwe, kupita Kimisi kwenda mpaka Lusumo, ni pori na kuna majambazi.  Ndio maana tunatekwa mara kwa mara kwa ajili ya barabara mbaya. Kutoka Bukoba kwenda mpaka Biharamulo, kati kati ya Kasindaga na Biharamulo, hakuna mawasiliano!  Unakuta maaskari kipindi hicho wanakama na majambazi, hana sehemu yoyote ya kupiga mawasiliano kwa sababu hilo pori lote halina mawasiliano, mara kwa mara wanapata shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kagera maaskari wamefanya kazi kubwa sana kipindi hiki cha majambazi. Naomba Serikali angalau iwaangalie kwa mawasiliano ya kati kati porini hapo angalau wawe na mawasiliano ya kuweza kuwasaidia kuwasiliana kule Biharamulo na Muleba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi tulipotoka hapa Bunge lilopita, nilipita barabara hii ya Biharamulo, tukakuta majambazi wamemteka askari akiwa anasindikiza gari lina maiti. Lakini, alitekwa mle katikati akiwa na simu mkononi, lakini hamna mawasiliano. Naomba Serikali sana sana, huo Mkoa usisahaulike, angalau kipindi kijacho bajeti inayokuja mtukumbuke katika maskari hao wa Kagera kuhusu mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengi yameishaongelewa na Wapinzani tayari na ninachoomba sana, mimi mwenyewe Kambi ya Upinzani na wananchi wa Mkoa wa Kagera hatuiungi mkono kwa sababu haitutetei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishia hapo.  *(Makofi)*

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia bajeti ya Serikali ya Mwaka 2007/2008 ya Wizara ya Fedha na Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza kabisa nianze kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri, Waziri wa Fedha - Mheshimiwa Mama Zakia H. Meghji, Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji - Mzee wangu Mheshimiwa Juma H. Ngasongwa na Manaibu Waziri.  Kaka Yangu Mheshimiwa Mustapha Mkulo, Mheshimiwa Abdisalam Issa Khatib na Mheshimiwa Gaudence Kayombo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Spika na Kamati ya Uongozi wa Bunge kwa mara ya kwanza kabisa Bunge kuwa na *Vote* yake ya bajeti inayojitegemea. Pia, naomba nitumie nafasi hii kuipongeza Serikali na Wabunge wote kwa kukubali Elimu iwe kipaumbele katika bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitaka kumsaidia maskini kwa kumfikia kutoka katika mapato ya Serikali elimisha watoto wake. Hata Mwalimu Nyerere alisema, naomba kumnukuu: *"If you want to rich a poor family, educate  their children."*  Hivyo na Serikali ya CCM inafahamu umuhimu huo na ndio maana inatekeleza hayo. Nami naiunga mkono bajeti hii ya Serikali ya 2007/2008. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nipongeze Taasisi za Fedha, hasa ikiwapo *NMB*. Tumekuwa tukiona kwenye vyombo vya habari vikichangia fedha kwa ajili ya maendeleo ya ujenzi wa shule zetu za Sekondari na *CRDB* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niipongeze *NMB* kwa kuwa tumeona kila mara kwenye magazeti ikitoa michango hiyo kwa ajiili ya kuendeleza dhamira ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nitoe ushauri mdogo katika bajeti hii tuliyoiongeza na tuliyoipa kipaumbele kwa Wizara ya Elimu, basi ifikirie kuongeza idadi ya watoto wanaolipiwa na Serikali, wale yatima. Naomba sana Serikali ifikirie hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudie, sasa nizungumzie Kilimo. Kwa mujibu wa Taarifa ya Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, ni kwamba kiwango cha mchango wa Sekta ya Kilimo kilishuka kwa asilimia 0.9 ukilinganisha na mwaka 2005. Lakini, Sekta hii hata kwa kushuka kwake, imechangia kwa kiwango cha asilimia 44.7 ukijumuisha Sekta zote zilizochangia Pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta hii ya Kilimo ina nafasi kubwa ya kuendelea kuchangia mchango wa Pato la Serikali. Lakini, katika hotuba ya Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, Mheshimiwa Alhaj Dr. Juma Ngasongwa, *bullet* ya 50, uk. 37, naomba kunukuu; Amesema: “Katika mipango ya mwaka 2007/2008, malengo ya kukuza Sekta ya Kilimo yatakuwa kama yafuatavyo:-

§ Kuendelea na mpango wa kuandaa mkakati wa matumizi bora ya ardhi;

§ Kuimarisha mikakati ya kuongeza idadi ya wawekezaji binafsi katika Sekta ya Kilimo;

§ Kuongeza kilimo cha umwagiliaji ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara;

§ Kuwafundisha wakulima matumizi ya vifaa mbali mbali vya umwagiliaji katika sehemu mbali mbali ambako kilimo cha umwagiliaji kinafanyika; na

§ Kuviwezesha vyama vya Wazalishaji kuzalisha mazao ambayo yanakidhi matakwa ya soko la ndani na nje” Mwisho wa kunukuu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hakuna mipango ya kuboresha masoko ya mazao ya mkulima kule vijijini na uboreshaji wa mapato yake kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaomba tutazame mapato yatokanayo na wazalishaji wadogo, wazalishaji wakulima, kwani wakulima kwa mfano, kule Namtumbo wanazalisha lakini pato lao ni dogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu tumefikia mahali kwa kukosa masoko ya uhakika, mahindi yameuzwa kilo Sh. 25/= kwa maana ya kwamba Sh. 2,500/= kwa gunia. Mkulima kwa heka moja ya mahindi anagharamia shilingi 87 na *average* ya mapato yake ni gunia kati ya 10 na 15. Hivyo, ukizidisha mara hizo 2500 kwa 15 ni sawa na Sh. 32,500/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, masoko ni suala kubwa sana ukitaka kumwendelea mwananchi mkulima wa kawaida. Serikali inatoa huduma nyingi za fedha kuboresha kilimo kupitia miradi mbalimbali, ruzuku ili wakulima waweze kuongeza vipato vyao na kupata maisha bora. Naomba tuangalie uboreshaji wa mauzo yao ili wapate faida tuliyodhamiria waweze kupata. Ukuzaji wa kilimo hauna budi kwenda sambamba na uenezaji wa masoko sahihi ambayo yatanunua mazao ya mkulima kwa bei na vipimo sahihi kule vijijini. Hivyo, naomba mtusaidie kutupa uwezo wa kuboresha masoko ambayo yatatusaidia kuuza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna miradi ya *AMSDP*, tuliahidiwa katika Mpango wa *Ware House Receipt System*, lakini bado kwetu haujafika kule ndio maana walanguzi wanapata *loophole* ya kuingia na kutukandamiza.

Kwa hiyo, tunaomba sana Serikali itusaidie mradi huu uweze kuanza mapema. Naamini kabisa utatusaidia katika masoko hayo. Naomba tusiwaache wakulima peke yao wakibabaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nije katika Mazao ya *Traditional Cash Crops*. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, alizungumzia katika changamoto, *bullet* ya 28, ukurasa wa 30 (iv), alisema "Mahitaji ya fedha za kigeni katika uchumi wetu ni makubwa kuliko uwezo wetu wa kuuza bidhaa na huduma nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu sana kuweka kipaumbele katika kukuza mauzo nje kama njia muhimu ya kujenga uwezo wa kujitegemea". Mwisho wa kunukuu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mauzo haya ya mazao ambayo tunauza nje, *Traditional Cash Crops*; Kahawa, Pamba, Mkonge, Chai, Tumbaku, Korosho na kadhalika. Kati ya Mwaka 2006 na mwaka huu, mapato ya fedha za kigeni, kuna tofauti ya dola milioni 95.7 ambazo mauzo ya nje yamepungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa nini yameshuka? Lazima tusiangalie kwa upande mmoja wa hali ya hewa tu, pia tuangalie kwa wakulima. Je, wakulima wana moyo wa kuendelea kulima mazao haya? Kwa sababu kwa mwaka jana kwa mfano, pamba ilikuwa ya kwanza kwa kuuzwa nje dola milioni 111.5. Lakini, mwaka huu imeshuka na imeuza nje dola milioni 37.6.

Tofauti kubwa sana, uzalishaji wake umepungua kwa asilimia 65.46. Sasa lazima tuangalie hapa wakulima. Vile vile tumbaku imeendelea kuwa ya pili kwa kuuza mwaka jana dola milioni 80.8, lakini mwaka huu imeshuka, imeuzwa kwa dola milioni 53.4. Kwa hiyo, naomba sana tuangalie.

Mimi ninachotaka kusema hapa ni kwamba, tunayo mifuko ya dhamana inayodhaminiwa na Serikali kupitia *BoT*. Kwa mujibu wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Uwezeshaji wa wananchi, *bullet* ya 21(iv); Uwezeshaji wananchi kiuchumi. Sasa mifuko hii naomba pia ituangalie sisi wakulima.

Sisi ndio tunaozalisha na yale mazao tunayozalisha, ndiyo na hao wafanyabishara wananunua kwetu, halafu wanauza nje. Lakini Mifuko hii ya dhamana inaonyesha inadhamini sana wafanyabiashara, inatusahau sisi wakulima. Kwa hiyo, naomba sana Serikali iangalie hii Mifuko ya dhamana itudhamini sisi wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mkulima wa tumbaku anapata taabu sana kugharamia gharama zake za uzalishaji wa tumbaku. Anakopeshwa na mnunuzi ambaye leo hajui *interest rate* yake yule mkulima. Kwa hiyo, mwisho wake anakwenda na anaishia kwenye gharama kubwa ambazo haziepukiki. Lakini, naomba sana Serikali katika Mifuko hii ya dhamana ikiweza kuwadhamini wakulima kwa kupitia *Primary Co-operative Society* zao, itatusaidia sana kunyanyua na kuwapa moyo wakulima, watazalisha kwa wingi na tutasaidia sana kukuza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine naomba nizungumzie kuhusu *Fast Tracking* ambayo imezungumziwa na wengine wakizungumzia kuhusu *Compliant Traders*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naiunga mkono hii. Naiunga mkono kwa maana ya kwamba *Fast Tracking* kwa wale *Compliant Traders* ni muhimu sana wasisumbuliwe pale Bandarini. Kwa mfano, kwanza ndio wachangiaji wakubwa sana wa pato letu. Kwa mfano, Tanzania *Cigarette Company*, mwaka 2006 imechangia shilingi bilioni 72.135 peke yake. Sasa hawa wakichelewa pale, wakicheleweshwa kuingia pale Bandarini kuingiza *raw material* zao, ina maana pia *production* inachelewa, kwa hiyo, *production cost* yao inapanda.

Kwa hiyo, ni muhimu sana watu kama hawa tukawaangalia. Mimi naunga mkono hii. Kuna hawa *Breweries, Coca Cola, Tanzania Portland*, S.S. Bakhresa nakadhalika. Tuangalie, lakini muhimu hapa kikubwa *TRA* lazima wawe makini kuangalia na sisi pia viongozi tusiwashinikize *TRA* kuweka kwenye orodha makampuni ambayo hayaja-*qualify* kuingia. Kwa hiyo, *TRA* wawe makini sana katika kuliangalia hili. Mimi naamini kabisa hawa wakipitisha *raw material* zao mapema, wakizalisha mapema, watazalisha kwa wingi na kodi ya mapato itaongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, naomba niiombe Serikali kuhusu mafuta ya taa. Naiomba Serikali ifikirie tena upya kwa sababu mafuta ya taa yanatugusa sisi wote hasa mwananchi wa hali ya chini. Lakini, sina budi kuwasemea wananchi wa Namtumbo,

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kusema, naunga mkono hoja! *(Makofi)*

**MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi nitoe angalau maoni yangu machache kuhusu bajeti hii

iliyowasilishwa na Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango. Lakini, kwanza napenda nimpongeze Kiongozi wa Kambi ya Upinzani kwa kuielekeza na kwa kutuonyesha mpango mzuri na kuielekeza Serikali wapi yapo mapungufu katika hii bajeti ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika wachangiaji jana, Waheshimiwa Wabunge wengi walikuwa wanawaomba Wabunge wa Kambi ya Upinzani waiunge mkono bajeti hii na ikafika wakati kaka yangu Mheshimiwa Mwanri, akasema sentensi moja ndogo katika *DS* yake kubwa, akatamka neno hili ambalo napenda ni-*quote*: "Bunge lifike pahali likubali *our own poverty*". Hayo maneno ya Mheshimiwa Mwanri. Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani si Kambi ya kupinga kila kitu! Hatuko hapa kupinga kila kitu, wala hatuna maana ya kupinga kila kitu. Lakini, tuko hapa kwa maana ya Kambi ya Upinzani tuna kazi mbili kubwa.

Moja, katika kazi ya Kambi ya Upinzani iliyotuleta hapa Bungeni ni kuikosoa Serikali na kuielekeza nini cha kufanya kwa mujibu wa wananchi walitupa mamlaka ya kuwepo hapa kama ilivyo Ibara ya 8 na Sheria Namba 15 ya 1984.

Kwa maana hiyo, sisi tupo kwa ajili ya kuikosoa Serikali pale ambapo inafanya kitu sivyo, kinyume na matakwa ya wananchi. Kwa hili, ndio tukasema hatuwezi kuiunga mkono bajeti hii kwa sababu yapo mambo mengi ambayo wapiga kura walitutuma, wananchi walitupa madaraka ya kufika hapa, hawayakubali! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mafuta, tena siyo mafuta ya taa tu kwa sababu Waheshimiwa Wabunge wengine wanasema mafuta ya taa tu, mafuta ya taa tu. Siyo suala la mafuta ya taa tu, kuongezeka kwa bei kwa mafuta yote ni athari kwa wananchi katika kila sekta. Wabunge wengi wameliongelea hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Serikali iondoe hili ongezeko la kodi waliloongeza katika mafuta ya aina zote. Serikali ikifanya hivyo na yale mambo mengine tuliyo shauri, ikija ile bajeti ambayo ina mwelekeo mzuri, hatuna sababu kwa nini tusiiunge mkono! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda , nielezee neno ambalo nijitahidi Mungu anijalie nisije nikazungumza mwiba ukasababisha na mimi niwekewe kikao. Lakini, nitumie neno alilolitumia Mheshimiwa Spika wakati tunaikaribisha Timu yetu ya Taifa, juzi. Alisema hivi; "tumechoka Tanzania kuwa vichwa vya wendawazimu". Sasa labda hili litakuwa zuri.

Naomba nitoe mfano. Tunasema hivi, tumechoka Watanzania kuwa vichwa vya wendawazimu! Tuchukue mifano mitatu,minne kuwapa upeo wananchi wafahamu.

Mfano, kuna Kampuni hii ya Alex Stuart ambayo imekuja hapa kwa kuangalia mapato yetu na mchakato mzima wa dhahabu. Lakini, sasa Serikali kipato chake katika masuala ya madini kwa mfano haya ya dhahabu, wanapata Mrahaba *(Royalty)* asilimia 3.

Hii kampuni iliyoajiriwa na Serikali kuja kufanya mchakato huo wa mauzo yetu ya dhahabu, kusimamia, leo wao wanapata asilimia 1.9. Katika mrahaba huo, Serikali ibakie na asilimia 1.1. Hivyo, jamani tumeona wapi katika Dunia hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina kampuni, namwajiri mtu aje afanye uhakiki, yule anayefanya uhakiki namlipa kingi zaidi kuliko faida ninayopata mimi! Je, hicho sio kichwa cha wendawazimu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuchukue mfano mwingine hizi meli za uvuvi na hii ndiyo mifano Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani aliyoieleza Serikali nini cha kufanya ili upate mapato mengine zaidi, usiwabebeshe mzigo hawa wananchi kwenye mafuta. Hicho ndicho kilichokusudiwa. Nichukue mfano mwingine, akasema kuna meli zaidi ya 193 zinavua, lakini meli hizi kodi ya mwaka ni dola 18,000. Majirani zetu wanatoza kodi ya mwaka ni dola 100,000. Hivyo kwa nini sisi tuwe tunatoza dola 18,000 kwa mwaka. Hii si sehemu nyingine ya Serikali kupata mapato? Kwa nini tumkwamue mwananchi?

Sehemu nyingine kuna mapungufu yaliyotokea katika ukusanyaji wa mapato yetu wenyewe, kwa mujibu wa ripoti ya Mkaguzi kuna zaidi ya shilingi bilioni 73.8. Je, hii si sehemu nyingine ambayo Serikali itapata mapato? Ingeweza kusimamia makusanyo haya vizuri? Kuna majengo haya ambayo yanalalamikiwa na wengi ya *Twin Towers* ambayo tumeweza kutumia si chini ya shilingi bilioni 340. Kiwango ambacho kila mtu anashangaa ni kikubwa kwamba wenzetu huko Ulaya ambao *per square metre* hawatumii zaidi ya dola 2,000. Sisi kwa kiasi hiki tunatumia zaidi ya dola 8,000 hivyo sisi ni matajiri kuliko Wajapan, Waingereza na Marekani? *(Makofi)*

Eneo lingine la sisi kudhibiti mapato tukapata mapato. Sasa hii mifano ipo mingi, na imeelezwa wazi wazi katika hotuba ya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, sina haja ya mtiririko wote. Lakini tunachosema ni kwamba ikiwa Serikali itaangalia sehemu hizi nyingine zote, basi uwezekano wa sisi Serikali yetu kuwa na mapato ya kutosha upo. Sisi ni kujitahidi kutafuta njia ya kudhibiti mapato yetu.

Mheshimiwa Hezekiah Shellukindo, Mwenyekiti wangu alizungumza juzi, sijui jana ile, alisema kwamba hawa watu ambao hawalipi kodi, wakamatwe, wapelekwe Mahakamani, sawa na mimi namuunga mkono vizuri sana. Lakini hata huyu ambaye hajalipa kodi, kuna hizi pesa ambazo zimeshaingizwa kwenye Halmashauri ambao Mkaguzi Mkuu wa Serikali anatuambia ni zaidi ya shilingi trilioni 1.2 hazionekani na zimekabidhiwa watu hawa. Kwa nini wasikamatwe kwanza hawa wakapelekwa Mahakamani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo ndiyo njia za kudhibiti. Hizo ndiyo njia zote za kupata mapato. Ukweli wa mambo Tanzania si maskini hata kidogo ikiwa tutaweza ku-*manage resource* zetu vizuri, rasilimali zetu vizuri tukizisimamia vizuri. Tukikusanya, tukisimamia mapato yetu vizuri, hatuna umaskini wa namna hiyo, kwa maana hiyo na mimi naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu waliosema kwamba kodi hizi za

mafuta zilizoongezwa ziondolewe. Zitawanufaisha wananchi wetu ambao ndio waliotupa dhamana ya hapa. Hilo ni suala namba moja nililokusudia kusema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha ukusara wa 23 na 24 alizungumzia ile Tume ya pamoja ya Fedha ambayo itatazama kile kiwango cha kugharamia baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Lakini katika Tume hii, katika ripoti hii ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha inaonekana bado itatumika asilimia ile ile ya kigezo cha asilimia 4.5. Mimi kwa kweli napata wasi wasi. Katika Mkutano wa Saba niliuliza swali namba 79 kwa niaba ya Mheshimiwa Fatma Fereji kwamba hiyo Tume iliyoundwa tangu mwaka 2003 tayari ilikuwa imeshawasilisha ripoti zake Serikalini. Kwa jibu alilotupa Naibu Waziri wa Fedha alikiri kwamba ripoti kweli imefika Serikalini tangia mwezi Oktoba, 2006. *(Makofi)*

Sasa basi mpaka kufikia Bajeti hii ikawa kigezo kile kile cha muda kilichowekwa cha asilimia 4.5 kitumike kile kile na hapa Waziri wa Fedha anatajwa ndiye msimamizi mkuu wa Tume hii kulikoni mpaka leo, ambacho kitu hiki ni moja katika kero kubwa ya Muungano. Lakini vile vile katika jibu la Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha ambalo napenda ku-*quote* sehemu ya mwisho, anasema baada ya kupata maoni ya pande zote mbili za Muungano Wizara ya Fedha ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itakamilisha Waraka wa Baraza la Mawaziri kwa lengo la kupata uamuzi rasmi wa Serikali. *(Makofi)*

Hilo lilikuwa katika jibu la Mheshimiwa Naibu Waziri. Lakini katika hotuba hii Waziri wa Fedha yeye anatueleza hivi. Naomba ninukuu; "Mawaziri wa Fedha wa Serikali ya Muungano Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar wamekutana na kukubaliana kwamba kila upande ukamilishe uchambuzi wa mapendekezo ya Tume na kuwasilisha maoni yaoni yao kwa Kamati ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri Kiongozi wa Zanzibar."

Sasa ni mambo mawili, mimi naona yanagongana. Huku viwasilishwe kwa Baraza la Mawaziri, huku iwasilishwe kwa Waziri Kiongozi na Waziri Mkuu. Sasa lipi ni lipi nafikiri Mheshimiwa Waziri ningeomba hapa atufafanulie vizuri. Kwa sababu Waziri Kiongozi na Mheshimiwa Waziri Mkuu tayari wamekutana, wanakutana muda mrefu sana kuhusu matatuzi ya Muungano, zile kero za Muungano na mpaka leo hazijapata ufumbuzi. *(Makofi)*

Lakini hili kwamba Waziri wa Fedha ndiye msimamizi mkuu wa ile Tume na Tume imeshakamilisha taarifa tangu mwezi Oktoba na mpaka tunawasiliwa Bajeti hii hayajarekebishwa kulikoni. Huku ukiambiwa itakwenda kwa Tume ya Waziri Kiongozi na Waziri Mkuu huku ukienda kwa Baraza la Mapinduzi na hili suala lipo miaka 14 nyuma halijapatiwa ufumbuzi. Si inatupatia picha kwamba bado ni dana dana. Tunataka ufumbuzi wa suala hili. Namwomba Mheshimiwa Waziri akija, atupe ufafanuzi wa suala hili.

Jambo la tatu, *fast tracking* ni mpango mzuri kinadharia na unatumika nchi nyingine na ikitekelezwa kihalali na inavyofaa hata mimi nitaunga mkono. Lakini suala

linakuja hapa, makampuni hayo ambayo yamekuwa yanaaminika kiasi hicho. Hayana matatizo, yanaweza kupitisha bidhaa zao halafu baadaye *clearance* ikafanyika huko baada ya kufikisha mizigo katika maeneo yao. Kwa kweli hilo suala kidogo linatupa wasiwasi je, si mwanya mwingine huu wa kupitisha dawa na mambo mengine? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwnyekiti, hayo makampuni mengi yaliyopo bandarini mpaka sasa hivi mbona ufanisi wa kazi hatujaouna na watu wanakimbiza mizigo wanapeleka kwenye bandari zingine za Mombasa na Msumbiji. Nini tatizo? Hivyo vigezo ni vipi? Ningekuomba kwamba kabla ya kupita suala hili hiyo upande wa *read* na g*reen* suala hili liletwe hapa Bungeni vionekane hivyo vigezo vilivyotumika kwa hayo makampuni ambayo yanaonekana yanaaminiwa. Vinginevyo suala hili ni kutoa mwanya kwa wengine.

Bila shaka wananchi wetu tunakubali wanapata taabu, bandarini wanatumia muda mrefu sana kwa shughuli zao, tungependa suala hili lisiendelee. Lakini hiyo *solution* iliyopendekeza Serikali kwenye Bajeti hii inaonekana kidogo ina walakini na vinginevyo tupatiwe ufumbuzi wa kutosha.

Kwa maoni hayo, nashukuru Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kuchangia ningetaka kutoa taarifa tu kwa ndugu zangu Waandishi wa Habari nawaheshimu sana. Gazeti la Mtanzania jana nilipokuwa nikiuliza swali langu walininakili kwamba mimi ni Mbunge wa Jimbo la Bububu, lakini ni wa chama pinga. *(Kicheko/Makofi)*

Sasa kwa taarifa mimi ni Mbunge wa Chama cha Mapinduzi (CCM). Baada ya taarifa hiyo, Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba na mimi nianze kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naiunga hoja hii mkono kwa asilimia zote. Kwa sababu zifuatazo:-

Kwanza, Serikali imezingatia Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005. La pili, mimi mwenyewe nilikuwa mstari wa mbele katika kuinadi Ilani hiyo na ndiyo maana nikachaguliwa baada ya wananchi walipoifahamu. Ndizo sababu zangu hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nianze kutoa mchango wangu kwa upande wa taarifa ya utekelezaji wa yale malengo ambayo Wizara ya Fedha ilikusudia kuyafanya mwaka jana. Mheshimiwa Waziri ameyaeleza vizuri, lakini ni kwamba kuna vitu vingine ambavyo amesahau. Kuna malengo mengine ambayo alikuwa ameyalenga kuyatekeleza. Lakini hajayatolea taarifa.

Kwa mfano, nafahamu kwamba alinunua magari katika Wilaya ambazo zilikuwa hazina magari. Taarifa hii kama ingejitokeza hapa ingekuwa swali. Kwa sasa litakuwa ni swali na huenda watu wangeuliza swali, kama ingekuwa imejitokeza taaria hii ikawa endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mifano mingine, hata vyanzo vya mapato, mwaka jana kulikuwa na vyanzo ambavyo havijatajwa safari hii, kwa mfano adhabu kwa wale watakaokwepa kodi. Alisema watatoa shilingi milioni mbili au mara mbili na kadhalika. Kwa hiyo, ingekuwa endelevu kidogo, mtu akifanya *reference* ya mwaka jana na angejua utekelezaji unakwendaje. Huo ni ushauri wangu kama utafaa basi Mheshimiwa Waziri kipindi kijacho anaweza akaufikiria. Lakini kingine ninashauri tu kwamba angalau kuwe na *executive summary* au kuwe na *annex* ambayo inaonyesha angalau kila Wizara imepata asilimia ngapi ili kupunguza maswali.

Jana kuna Mheshimiwa Mbunge mmoja alitaka kujua, alikuwa na wasi wasi kwamba Waziri ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi hana uhakika kwamba Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia, labda imo humu, lakini kungekuwa na *annex* inayoonyesha kila Wizara ina asilimia ngapi, isingekuwa swali. Kwa hiyo, ningeshauri na hilo pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hilo naomba sasa nielekeze mchango wangu kwa maeneo haya yanayohusu Zanzibar. Kwa sababu natokea huko. Suala la mgao wa fedha wa asilimia 4.5 wenzangu wamelizungumzia na mimi sina budi kulizungumzia tena. Kwa sababu linanihusu kwamba kama taarifa iliyoandikwa kwamba Tume au

Kamati ya Pamoja ya Fedha imewasilisha taarifa hiyo kwa Serikali. Najua ni Serikali mbili kama alivyotaja Mbunge aliyekaa. Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapunduzi Zanzibar. Kwa ajili ya kupata maoni *comments. (Makofi)*

Lakini naomba unilinde Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ikaamua safari hii SMZ itapewa 4.5%, Sasa nikajiuliza Serikali hizi zimeletewa mapendekezo ilikuwaje sasa mmoja aamue 4.5%. Kwa kweli nikaona labda kuna Serikali moja haijawajibika, kama haiwajibiki basi tuambiwe kuna matatizo gani. Kwa hiyo, tungependa kwa kweli suala hili limalizike ni la siku nyingi kama walivyosema wenzangu na linasaidia sana katika utekelezaji wa Ilani yetu kwa upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana ile 4.5% ilikuwa imeelezwa na kiwango. Ilikuwa ni shilingi bilioni 21.192 kama sikosei. Sasa na hii basi angalau ingeelezwa hii 4.5% ni kiasi gani cha pesa. Lakini pia endapo uamuzi umeshafikiwa kwa mfano mwezi Agosti, Septemba, je, asilimia ambayo itakubaliwa ndiyo itaanza kulipwa? Lakini pesa hizo zitatoka wapi, kwa sababu kwenye Bajeti hamna! Nilitaka tu ufafanuzi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu vitambulisho vya Taifa vya uraia, Zanzibar tayari kuna vitambulisho hivyo kwa upande wa wakazi wa Zanzibar, mimi ninacho. Lakini sasa hivi vitambulisho vya Taifa vya uraia nafikiri ni kwa Tanzania nzima. Kwa kuwa Wizara ina mikakati tayari na matayarisho ya maandalizi je, kwa Tanzania Zanzibar, kuna mikakati gani au hao ndiyo wataendelea na vitambulisho hivyo. Lakini haitakuwa sawa kwa sababu ni Watanzania. Nilitaka ufafanuzi pia juu ya jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu pensheni, linafanana sana na lile la vitambulisho kwa sababu Zanzibar pia kuna wafanyakazi ambao ni wastaafu ambao wamefanya kwenye Taasisi za Muungano, wakishastaafu, wanapata shida ya ufuatiliaji wa pesa, je, kule mmezungumza na Serikali ya Mapunduzi kuhusu kwamba wao watalipwa sasa kupitia *Zanzibar Social Security Fund (ZSSF)* au kuna taasisi au kutafungua Ofisi Zanzibar moja ya ofisi hizo kwa upande wa Unguja na Pemba? Pia nilitaka kufahamu hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo nataka kuzungumzia kuhusu sheria ya Ushuru wa Barabara, *sorry* kabla ya barabara bidhaa za Zanzibar kwamba kwanza niipongeze Serikali kwa kuliona hilo kwamba bidhaa zote zinazouzwa Zanzibar ambazo zinatoka hapa au kutumika kule kutoka Bara. Kwa kweli ni uamuzi mzuri, utaiwezesha Serikali ya Zanzibar na yenyewe kupata mapato kama walivyozungumza wenzangu asubuhi au jana ile. Itasaidia kwa kweli kwa kiwango kikubwa. Lakini wasi wasi tu ni jinsi gani ya kuweza kuyadhibiti hayo mapato. Je, Serikali hizi mbili zimekaa na kuona namna gani hizi bidhaa zinaweka mapato ya kweli kwa upande wa Zanzibar au vyombo vinavyohusu fedha, Wizara ya Fedha Zanzibar watakuwa na Ofisi zao hapa ili kukusanya mapato hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi niipongeze *TRA* kwa kazi nzuri wanaoifanya kwa kweli na-*appreciate.* Pamoja na hivyo lakini kizuri hakikosi kasoro, bado kuna matatizo labda niseme hii *Escuder Plas Plas* haijafahamika kwa upande wa wafanyakazi

wetu au sijui vipi. Kwa sababu mimi yamenikuta nilipokuwa Dar es Salaam. Nilisafirisha gari yangu, lakini sikutaka kujionyesha kwamba ni Mbunge, nilitaka nijue kweli mambo yamerekebishwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale pana matatizo, tena makubwa. Hii *difference* ya magari kutoka Zanzibar wametozwa ushuru mkubwa na ukweli ukiangalia Zanzibar sasa hivi ushuru wa magari ni mkubwa kwa kweli na unalingana na hapa na tuliambiwa na Waziri kwamba suala hilo limekwisha. Kwa hiyo, ukitoka Zanzibar na gari lako ukija hapa wewe utalipia gharama nyingine ambazo ulikuwa hujalipia. Lakini bado mimi nimelipa zaidi ya shilingi milioni 1.2 kwa hilo gari, halafu unaambiwa kuna uchakavu. *(Makofi)*

Jamani gari kubwa kuna uchakavu, sheria haisemi gari kubwa kuna uchakavu. Sasa ushuru wa uchakavu umetoka wapi? Mimi nikaona hapa labda sheria ya hawa watu hawajaelimishwa au wanazikwepa au kuna harufu ya rushwa na kweli harufu ya rushwa ipo. Naomba Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri alifuatilie hilo ni kero kwa wafanyabiashara wa Zanzibar na wa Tanzania Bara kwa sababu na wao wananunua magari kule. Sababu wanayotoa ni kwamba gari ikiletwa Zanzibar linakuwa na bidhaa ndani. Kunakuwa na ma-*frige* sasa hayo yanawahusu nini? Gari imefika pale halina vitu hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hilo alifuatilie na lingine ni suala la kuweka wanasema *one stop centre TRA*. Kwa sasa mtu unapotaka kulipa kodi ya mapato kuna ofisi yaani utazunguka uende sijui *long room* sijui halafu uende wapi, halafu uende Ilala, wengine hata hawafahamu. Kwa hiyo pale, unakuta ile *element* ya rushwa ipo. Unamkuta *Ultimate Security Group* yaani askari ameajiriwa pale, anazijua bei zote za magari na anakushawishi kwamba usiende kufungua *file* kwa sababu ukifungua *file* utachukua siku nyingi. Hapa kila kitu utapata. Hii inaonesha dhahiri ni rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya hayaonekani? Sasa nataka kuzungumzia Sheria ya Ushuru wa Barabara. Kwa kweli ushuru wa barabara ni lazima iwekewe kipaumbele, kwa sababu barabara zetu ni mbaya na zinahitaji matengenezo na hatuna *fund sources* nyingine kwa sasa pamoja na Serikali inajitahidi kutafuta hizi na Wabunge wenzangu ningewashauri kwa kweli tukubali tu kwamba lazima ongezeko fulani litatuathiri, lakini athari yake si kubwa kama ukilinganisha kama barabara zitakuwa mbovu zote, gharama itakuwa ni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachonishangaza hapa mimi ni ile ada ya magari (leseni), yale magari yanayoharibu barabara ndiyo bei nafuu, yale magari ambayo hayaharibu barabara ndiyo bei kubwa. Sasa hii inatokana na nini? Mimi sijajua ni kigezo gani kilichotokea hapa. Kwa kweli mimi naona haya magari makubwa yalistahiki yalipe hizo shilingi 230,000. Kwa sababu ndiyo yanayoharibu barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo yaliyowekewa mizani, hiyo mizani huwezi bwana ukapita na *Land Cruiser* yako ukapima. Nani aliyepita pale kwenye mizani

hakuna. Lakini ni haya mabasi *why?* Kwa sababu yana-*damage* barabara. Sasa mtu ana-*damage* barabara bado unampa ushuru wa chini, mimi nitakuwa na wasiwasi, labda kuna wakubwa pale wameingia, wana vitu vyao hapo, wanataka ku-*defend. (Makofi)*

Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri a-*review* tena hiki kitu, sikatai kwamba watu tusipewe leseni, lakini lazima tulipie leseni ili kuzitengeneza barabara zetu, lakini pia pikipiki, kigezo kisiwe ujazo wa *cc,* kwa sababu mwenye pikipiki jamani tutakuwa tunamwonea. Basi nashauri waweke kwenye vyombo vya moto vyenye miguu miwili, mitatu, walipe shilingi 20,000. Sasa hata unapofanya *design* ya barabara ni hazina. Unahesabu ile *traffic count* yako unaanza na tani tatu au 2.5. Zile ndiyo zina-*impact* kwenye barabara zinazoharibika. Lakini magari kuanzia tani moja mpaka mbili na nusu kuwe na *category* nyingine, gharama yao iwe nyingine. Itakuwa *unfair* kwa kweli, alipe shilingi 230,000 kwa gari ambayo ina tani mbili. Sasa kigezo kiwe ni tani ngapi, kuanzia tani ngapi, mpaka tani ngapi, kiasi fulani, haya magari makubwa yalipe zaidi ndiyo yanayoharibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki nigongewe kengele, lakini sasa ninaomba nizungumzie suala la *TASAF.* Nafahamu *TASAF* ilivyofanya, *TASAF* namba moja, *TASAF* namba mbili. Nasikitika kwenye jimbo langu sijapata hata mradi mmoja. Nafahamu kwamba *TASAF* iko Zanzibar, iko chini ya Waziri Kiongozi, lakini sitaki kusikia nikiambiwa niende huko. Naomba kwa sababu huku ndiyo makao makuu ya *TASAF.* Wananchi wangu wameomba miradi ya maji katika Sheria 4, Sheria ya Sharifu Mussa, Kibweni, Mwanyanya na Bububu yenyewe mpaka leo hatujapata. Sasa tunaomba wananchi wapewe huduma ya maji, wanapata shida sana. Nasema kwamba sitataka kusikia nikamwone Waziri Kiongozi hapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara husika itakaa na wenyewe kule Zanzibar, ili mradi ule ufanyike na bado miaka miwili tu *TASAF II* kumaliza miradi mingine huko tunasikia *TASAF* inakwenda vizuri. Sisi kule hakuna, inakuwaje? Kwa hiyo, nitafurahi sana Mheshimiwa Waziri asinipe majukumu mimi nikamwone Waziri Kiongozi, ofisini kwake ili inishughulikie, hapana. Isipokuwa atajuana na ofisi ya huku ambayo ni makao makuu ya *TASAF* nasisitiza hilo, ahsante. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa mara nyingine. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijampa nafasi Mheshimiwa Ibrahim Sanya aendelee, nimepokea taarifa kutoka kwenye Meza ya Katibu kwamba Waheshimiwa Wabunge mmekuwa mkiendelea kuomba nafasi ya kuchangia hoja hizi mbili. Sasa kwa taarifa ya Meza ya Katibu hoja hizi mbili zimeshapata wachangiaji wa kutosha ambao watatufikisha mpaka muda ule ambao tumekubaliana wa kuhitimisha hoja hizi. Kwa hiyo, tunafunga sasa upokeaji wa maombi ya kuchangia hoja hizi mbili na tusubiri sasa hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu itakapokuwa imewasilishwa Mezani ili tuendelee kuomba. Baada ya Taarifa hiyo naomba sasa nimwite Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Sanya na Mheshimiwa Clemence Lyamba, ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. IBRAHIM MOHAMED SANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie kidogo baada ya kupigwa *pause* juzi na Mheshimiwa Spika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyombo vya habari vilitoa taarifa kwamba nimepigwa *stop* sikupigwa *stop* nilikuwa *paused* tu, sasa naendelea. *(Makofi)*

Waziri wa Fedha ametuletea Bajeti hapa Bungeni, sisi wajibu wetu kuipitia, kuijadili, kuona mapungufu, kujaza nyama na yeye kazi yake kubwa ni kupokea na wataalamu wake kuangalia uwezekano wa yale ambayo tunayazungumza na yale ambayo yataleta maslahi kwa nchi kama kuna uwezekano aweze ku-*review* na kuwapa unafuu wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusimlaumu sana wakati bado hajamaliza kazi, aweze akarekebisha. Mimi naelewa Mama Zakia Meghji ni mama yetu, wengine ni dada yetu, ni Waziri wetu, vile vile ni mzazi katika nchi hii ya Tanzania. Anaelewa matatizo fika ya wazazi wenzake na watoto wa Taifa hili la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mafuta si suala la kusherehekea au kupata nafasi ya kugonga katika Bunge bila ya kuangalia hasa nini athari zake katika nchi changa na nchi zinazoinukia kiuchumi kama nchi yetu ya Tanzania. Siyo petroli tu, wala dizeli au mafuta ya taa, tuangalie nani anataabika, nani anahenyeka na maisha ya kila siku, tunaona daladala zinavyowasumbua wanafunzi wetu nchi hii. Leo tunawapandishia petroli, watafanya nini wanafunzi wetu ndani ya daladala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi vijijini hawana kinachowasaidia zaidi ya mafuta ya taa, hata kama tunalinda mazingira kwa ajili ya kuunusuru msitu wetu na kutumia mkaa, lakini tuangalie athari za mkaa. Mkaa siyo tu kwamba unaathari ya kumaliza mazingira ya nchi yetu, hapana. Unapowasha mkaa kwa ajili ya kupikia, mara ukimaliza mkaa unakwenda, ina maana huutumii tena siku ya pili. Lakini unapompa unafuu wa mafuta ya taa akaweka kwenye jiko la Kichina, atawasha kwa muda ambao atatumia kupikia chakula chake akimaliza analizima jiko la Kichina kulifunga mpaka wakati mwingine atakapohitaji kulitumia.

Kwa hivyo, Mama Zakia Meghji, namwomba sana Waziri, muda bado upo akakae na wataalamu wake, tuweze kuji-*squeze* katika sehemu ya Bajeti hii, twende na *cash budget* lakini suala la mafuta na hasa mafuta ya taa yanayomgusa mnyonge kijijini, yasiguswe wala yasizungumziwe na yawekewe bei ile ile tuliyotokanayo mwaka jana mpaka mwaka huu. *(Makofi)*

Kuna nchi kama Burundi, Bujumbura juzi wamefanya nini? Wameipa kampuni fulani kutoKa Rwanda ya kuchukua taka za Mji wa Bujumbura kuzipeleka kwenye kiwanda zinakaushwa, zinatengenezwa, wakati huo huo wanasafisha mji, wakati huo huo taka zile zinatoa kuni na wanasema kwamba zinatumia nusu ya matumizi ya mkaa wa kawaida. Unapokata kuni zinatumia nusu ya matumizi ya mkaa wa kawaida, unapokata kuni kilo 10 kwa kutengeneza mkaa unapata kilo moja ya mkaa. Kwa hiyo, Mama Zakia

Meghji, tunamwomba sana azingatie Watanzania wanalia kwa uchungu kuona kwamba sasa hawatamiliki hata vibatari vya kusomesha watoto wao vijijini. *(Makofi)*

Hizi sekondari tunazojenga bila ya kuwapa mafuta ya taa watoto wao wakafanya *revision* na umeme haujafika na hata kama ukifika utapita juu ya paa lake hawezi akatia umeme katika nyumba yake ya tembe, atafanya nini Mtanzania huyu? Hilo la kwanza.

La pili ni elimu, Bajeti nzuri sana ya elimu naipongeza lakini tumechelewa tu kwa sababu elimu ndiyo msingi wa maendeleo ya mahali popote duniani, kaulizeni India walipopata uhuru Mahatma Gandhi alifanya nini?

Kwanza elimu halafu wakajenga *dams and schemes* ku-*control floods* wakatumia *scheme irrigations* katika maeneo yao wakazalisha chakula wakawa na *surplus*, leo tunaagiza mchele kutoka India tunanunua kilo shilingi 1200 na tunaagizia mchele kutoka Kyela tunanunua kilo moja kwa shilingi 1200, *what is the difference?* Tunafanya nini hapa?

Elimu lakini ni *quality?* Tunaambiwa tu hapa kata, vijiji na kadhalika kumejaa shule zina walimu *qualified?* Tume-*determine* kwamba wasome katika njia za kisasa wana *laboratories?* Wana *libraries?* Tuki-*determine* kitu ku-*determine* kwa maana ya kwamba kesho kutatokea nini katika nchi yetu. Hilo la pili.

La tatu ni suala la kilimo. *Punjab* maana yake ni *The Land of Five Rivers* katika *river Hindus* ambayo ina *flow* maji yake kutoka India na kuingia katika *Arabia Sea* na *those five tributaries* ni Ravi, Chelam, Chenab, Bayas and Jelam na hizi zinaweza kutumiwa vizuri na India ndiyo *Brass Bread Basket* ya India leo katika *Indus Basin* kama ilivyokuwa Zimbabwe mwaka 1986 ilikuwa ndiyo *Bread Basket* ya nchi za Kusini mwa Afrika. India wanasafirisha chakula, wana *surplus* leo wame-*control floods* lakini tatizo lao ni *population* kama sisi na sisi tuna tatizo la kutokubali ukweli wa mambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapomnunulia mwanao kiatu *size number 6* atavaa kiatu katika ukuaji wake wa kawaida ipo siku atakwambia baba kiatu hakinifai kimekuwa kidogo, na huo ndiyo udhaifu wa binadamu. Baba yake atakubali atamwambia kweli mwanangu kiatu kimekuwa kidogo, hatamwambia kwamba mwanangu kiatu nambari ndiyo ile ile sita uliokuwa ni mguu wako. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa ndiyo sisi Watanzania, tunatupia lawama kwamba nchi yetu ni maskini wakati ina *resources* za kutosha, tunasema kuna matatizo haya na yale lakini hatulinganishi na *population* ya nchi kwamba na sisi tunakuwa wakatu tulipopata uhuru haikuwa na idadi na leo tuna idadi gani na tunaambiwa 2015 tutakuwa na watu milioni 65 tutawaweka wapi? Tutawalisha nini? Mafuta ya taa yatakuwa bei gani? Dhahabu wakati huo itakuwa imekwisha, wazungu walishatokomea, samaki *Lake Victoria* wameshakufa tutafanya nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni lazima tujenga misingi hata hawa wawekezaji wawekeze kwa njia ambayo tutanufaika, kesho wajukuu zetu watakuja kuuliza wataambiwa hapa ni Geita, Simanjiro na kadhalika palitolewa dhahabu, dhahabu hii ilifanyiwa nini na

imekwisha na watu walishatoweka. Samaki, kuna njia gani za kurejesha tena samaki? Za ku-*control* mazalia yao, tuna Serengeti, Kilimanjaro, magofu ya Bagamoyo lakini watalii wako wapi? Singapore leo nimeona kwenye *internet* ambayo inakataliwa na baadhi ya viongozi, Singapore mwaka jana imepokea watalii 9,500,000 hiyo ni mwaka jana na wanasema mpaka mwaka 2015 watahakikisha wanapokea watalii 115,000,000,000 *it is a small country* lakini *with a….* Wanafikiria wafanye nini?

Sasa sisi hapa tusikae tukailaumu Serikali tu bali tuiongoze na tuielekeze ifanye nini kwa sababu Serikali iliyopo kama sisi ni Wapinzani sisi hatupingi kila kitu sisi tunaielekeza ili mfanye kwa ajili ya kuwanafuu Watanzania wenzetu na sisi ni Watanzania hivyo hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kama Mama Zakia Meghji ataondoa ushuru wa mafuta hata hayo ya taa ushindi si wa Wapinzani tu, ushindi ni wa Wabunge wote kwa sababu hata CCM mtaathirika na hili katika Majimbo yetu na katika vijiji vyetu na itajenga heshima kubwa nchini kwamba leo viongozi kweli wanakaa na kujadili na kupanga na mwisho wanatoka na *solution* ya pamoja kwa ajili ya maslahi ya nchi yetu. Ondoa kodi ya mafuta Mheshimiwa Zakia Meghji na tutakupongeza kwa hilo haidhuru kama hatutaunga mkono lakini kukupongeza japo nje, tutakupongeza kwamba *now you have mastered.(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Watanzania tuzalishe kwa maana ya kusafirisha, leo kuna *AGOA, EPA* lakini viwango vyetu havijafikiwa kusafirisha, kwa nini tusisafirishe? Mimi najiuliza, parachichi kaiulize Toronto ni bei gani moja, embe moja bei gani, chungwa bei gani, kaulize maji ya dafu yaliyotengenezwa Indonesia na Philipines ni bei gani. Sisi tunazalisha hatuna viwango. *(Makofi/Kicheko)*

*(Hapa kengele ya kwanza ililia)*

**MHE. IBRAHIM MOHAMED SANYA:** Ah! leo ilikuwa nipate nusu saa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Morogoro wanazalisha machungwa lakini hayana viwango, nenda Zimbabwe kuna eneo moja linaitwa Maikelweni. Maikelweni wanazalisha machungwa yanaitwa *Mazoe Orange* wakati ule walikuwa wakisafirisha dunia nzima pia walisafirisha *strawberries*, leo korosho mh!

Mimi juzi nilibahatika kwenda na Mheshimiwa Rais nchini Uingereza, nikaingia hotelini kule Uingereza nikaona kifriji nikafungua nikaona chupa moja ina korosho zinatoka Japan! Japan wanazalisha korosho? *Salted cashewnuts* bei yake mimi mwenyewe hata kuizungumza hapa naona aibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ina maana kwamba sisi hatupo katika njia ya *processing*, tuchukue korosho tuzifanye ziwe za *salted* kama *salted* au hata kama za masala tusafirishe na soko lipo. Leo dunia nzima bidhaa zao wanazipeleka Dubai kama ni

*centre of business*. Ndiyo pale unapata mchele wa *basmati* unapata *cashewnuts* na mambo mengine chungu mzima kwa nini sisi tunashindwa? *(Makofi)*

Tuna *coffee* kula Mbinga imekaa tu kwa nini isisafirishwe? Kuna *spices* ambazo tunaweza tukazi-*process* tukasafirisha leo soko kubwa la Dubai la *spices they are from Bangladesh, Iran, Indonesia* na hata India, *Why?* Basi *spice Ireland* jina kubwa tu, watalii jina kubwa. Tuandaeni mipango na watu wapo na hawa viongozi wetu wawatumie Mabalozi katika nyanja kama hizi watangaze utalii Mlima Kilimanjaro, leo tunapiga kelele kwamba Kenya katupiku Kilimanjaro iko Tanzania na kama kuiondoa angekuwa ameshaiondoa lakini bahati mbaya tu ni maumbile, anaitangaza ni yake.

Sisi tunashindwa kutangaza Kilimajaro, tunashindwa kutangaza *culture* ya Mmasai, tunashindwa kutangaza magofu ya Bagamoyo, unakwenda katika Mabalozi ya nchi za nje hakuna *brochures* hata za kuitangaza nchi yetu halafu tupige kelele kwamba uchumi mbaya. Watoeni watu wakafanye kazi nje, tumieni pesa kidogo wengi wafanye kazi na warejee, wewe nenda kauze kahawa huku, wewe kauze *prawns,* wewe kauze samaki watu wanauza mpaka mawe, chokaa na udongo. *(Makofi)*

Alikuwepo Mjerumani pale Zanzibar katika eneo la Magomeni, watu wa Magomeni kama mnakumbuka alikuwa akisafirisha mawe, maganda ya machungwa, maganda ya malimao akiyapeleka Ujerumani, *yes!* Sisi tuamkeni kibiashara. Haya mambo ya dhahabu na samaki yatakwisha tu, mikataba lazima isimamiwe vizuri hakuna njia. *(Makofi)*

Tuliingia ubia na *ATC* mwaka 2003/2004 tukala hasara ya shilingi 8.7 bilioni, mwaka 2004/2005 shilingi 8.3 bilioni na mwaka 2005/2006 tuka *expect 5 point something* ilikuwa tumekula hasara ya shilingi bilioni 24. Leo ndege zinakuja hapa Tanzania haifanyi kazi, zinakuja *Qatar Airlines* kila siku ndege moja, *Emirates* kila siku ndege moja zinajaza Watanzania kwenda nje kwa nini katika Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, asielezee kuna mpango gani wa kuanzisha upya na kulijenga shirika letu likajulikana na likazalisha na likaweza kuchukua Watanzania kuwapeleka nchi za nje? *Ethiopian Airlines* inachukua 25% ya mapato ya nchi kwa ajili ya uwanja tu wa Addis Ababa pamoja na ndege zake sisi tunangojea tusafirishwe *first class* tukatembee turudi basi. Wengi wetu tumegeuka Ma-Vasco Dagama na Ma-Christopher Gulumbas. *(Makofi)*

Twende nje tuka *explore markets* kwamba Tanzania kuna hiki na kile ili watu waje wa *invest* kwenye *agriculture, sea fishing* na tusiwangojee wakaja waka-*grab* dhahabu zetu tu. Kwa nini hawa ambao *termination of contract* hazipo katika mikataba unapoona kwamba mwaka umemaliza *Air Tanzania* imekula hasara *more than 5 billion,* simamisha mkataba mwambie hapana hili ni shirika la watu na watu wenyewe ni raia wa nchi hii siyo viongozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kwa niaba yao ndiyo tumetia saini hii mikataba ambayo inachukua hii *Air Tanzania* tukapaka rangi ikawa inakwenda Afrika Kusini inalala Uganda na abiria wanne au watano inarudi Tanzania na matokeo yake ni hasara.

Lakini *source* ya *inflection* kwa wakati huu na itatu-*cost* sana Watanzania wanaweza wakachukua bidhaa za nje zikawa ni rahisi sana kuliko tunazozalisha hapa kwa kupandisha haya mafuta hatuyaoni leo baadaye tutayaone.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi namwomba kwa kumnyenyekea na kwa kumheshimu na atakuwa jasiri atapata heshima na hiyo ari mpya ndiyo itakapoonekana kwamba kweli Watanzania wamepeleka kijiji cha Bunge kwenda kuwatetea Watanzania wao. Ondoeni tunawaomba hiyo kodi ya mafuta na tuji *squeze* hivyo hivyo kidogo kidogo tuzuie Bajeti yetu katika mambo ya semina. Kwa nini tusifanye hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wetu *Taifa Stars* walikuja hapa tukawachangia mara moja na wakapata pesa nyingi tu nchi hii, tuna mipango gani ya kuwaelimisha kuzitumia pesa zile angalau wakanunua hisa katika *NMB?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana nakushukuru na sasa naomba nimwite Mheshimiwa Clemence Beatus Lyamba na Mheshimiwa Fuya Godwin Kimbita, ajiandae.

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia machache niliyonayo. *(Makofi)*

Kwanza napenda kutoa pongezi za dhati kabisa kwa Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa na Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Zakia Meghji, kwa ujasiri na umahiri walioutumia kuiandaa bajeti hii.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti zote na hotuba zote ni nzuri lakini ni muhimu tusidanganyike, Bajeti hii ni ngumu na nzito. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kibinadamu ni rahisi kusema na ku-*criticise* ya mwenzio kuliko kutenda, kwa hiyo, niombe radhi nami toka mwanzo nitaingia katika mkumbo wa kusema kwa kushauri kwa lengo la kuwaletea au kujumuika kuwaletea Watanzania maisha bora kama Ilani ya Chama cha Mapinduzi ilivyoahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema Bajeti hii ni nzuri kwa sababu mipango yake na maandalizi ya Bajeti yamelenga kuelekeza dira itakayotufikisha kuwaletea Watanzania maisha bora na kupunguza umaskini. Lakini pamoja na hayo ni ngumu na ugumu wake unatokana na baadhi ya mambo kama yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama za matumizi zinazotakiwa kwa ajili ya kutekeleza Bajeti hii itakuwa ni ndogo kuliko mapato yatakayokusanywa. Nasema hivyo kwa sababu moja kwamba ukirudi nyuma miaka mitatu au minne na zaidi pengine ukaangalia taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali utakuta kwamba kila mwaka kwa Bajeti iliyopangwa hatma yake atakapotoa taarifa yake utakuta kwamba kulikuwa na upotevu mkubwa wa fedha, kulikuwa na fedha zilizotumika pasipo idhini,

palikuwa na fedha ambazo zimetumika bila maelezo na *actually* inamaanisha matumizi yalikuwa ni makubwa kuliko mapato na Bajeti hii siamini kama itakuwa ni tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kubwa zaidi na ambalo ni zito zaidi na gumu ni njia zilizopendekezwa za kukusanya mapato kuweza kutekeleza azma ya kuwaletea maisha Watanzania kwa sababu njia hizi karibu zote zitamuathiri Mtanzania wa kipato cha chini na hata kipato cha katikati moja kwa moja kwa kuongeza gharama zake za maisha na kwa maana hiyo ile dhana kwamba tunawaletea Watanzania maisha bora kidogo itakuwa na sura ya kufifia kwa sababu ya ukali wa maisha kama Serikali haitachukua hatua ya kulegeza au kubadilisha mapato mbadala kwa kodi mbalimbali ambazo zimepangwa katika mtiririko ulivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia hayo kwa kifupi naomba sana Serikali iangalie na ifanye kila jitihada inayowezekana kupunguza kwa kiasi kikubwa kodi zote ilizozipendekeza zinazomgusa mwananchi moja kwa moja ili aweze kumudu maisha yake ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili wananchi wa kipato cha chini na wananchi wote kwa ujumla waonje matunda yaliyoletwa na Serikali ya Awamu ya Nne kama Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ilivyoelekeza ninaomba la kwanza, ongezeko la kodi kwa mafuta ya taa labda ndugu yangu Ibrahim Mohamed Sanya aliangalia nilivyokuwa nimeandaa mchango wangu, lakini ninaomba ongezeko lolote la kodi lililopangwa kwenye mafuta ya taa na tozo zozote zilizolengwa kwenye misitu au miti itakayoashiria kuongeza bei ya mkaa isamehewe au iachwe kama ilivyokuwa awali. Upungufu utakaotokana na misamaha hiyo itafutwe katika maeneo mengine ambayo hayawagusi moja kwa moja wananchi wa kawaida.

Kwa mfano, zamani tulikuwa tunapigwa kodi kwenye *TV* zenye madishi na kadhalika ni mfano tu vitu kama hivyo ambavyo haviwagusi wananchi wa kawaida moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, langu la pili kama pendekezo ni leseni za vyombo vya usafiri vinavyotumiwa na wananchi wengi kama pikipiki, *Bajaj* na daladala vingepewa *flat rate* ya leseni ya mwaka kama shilingi 40,000 *flat* ili kuchochea *compliance* na kuzuia ongezeko holela la nauli za daladala na usafiri kwa ujumla wa magari mbalimbali.

Pendekezo langu la tatu ilikuwa ni kwamba magari yenye uzito wa engine ya *cc 4000* hadi *cc 5000* yangepewa nayo *flat rate* ya shilingi 150 nayo pia yasaidie kuepusha ongezeko la gharama za usafiri wa mazao na mizigo mbalimbali ambayo kwa kweli ndiyo tegemeo kubwa la wananchi wakulima katika barabara zetu ambazo ni mbovu. Ukiwaongezea mzigo mzito nauli zitakazopanda kutokana na gharama za leseni hizo watashindwa kumudu na hata kupata kichocheo cha kuendelea kuzalisha mazao mashambani.

Lakini *fall back position* wale ambao watashindwa kukidhi malipo ya leseni hizo kwa wakati unaotakiwa Serikali inaweza ikatunga na kuamua kuwapa adhabu kubwa kwa

namna fulani iwavute kuhakikisha mapato ya Serikali yanapatikana kwa wakati uliopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tunavyozungumza kwa siku hizi tatu, nne mpaka na kesho Watanzania wote nchini macho yao na masikio yao na kwa ujumla hatma ya maisha yao wameyashikilia mkononi wakingojea mwisho wa Bajeti hii kitatokea nini kwa Serikali ambayo bila kujali itikadi zao mbalimbali za vyama vyao waliamua kuichagua kwa kura nyingi na wanategemea kwamba inaweza kuwanasua katika kila aina ya majanga pamoja na Bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hiyo naiomba Serikali isikilize sauti ya watu. Nilipokuwa mdogo kidogo nilikuwa nasoma mambo ya kilatini na huwa nasikia pia, kuna kauli hata Baba Mtakatifu huwa anasema; *"vox poplin, vox day"* maana yake ni kwamba Sauti ya Watu ni Sauti ya Mungu. Siku zote tunaanza hapa Kikao cha Bunge kwa kumwomba Mwenyezi Mungu na kilio cha wananchi wa Tanzania kwa kipindi hiki ni kikubwa mno kama tungekuwa tunaweza kwa *wave length* zisionekane tukasikia yale yanayozungumzwa na wote huko nafikiri pangekuwa na sokomoko lisilokuwa la kawaida. Kwa hiyo, naomba tuwasikilize wananchi kilio walichokitoa kuhusu gharama za kupanda kwa maisha.

Jana usiku wakati natafakari nitakavyochangia leo saa 1:16 nilipata simu kwa mzee mmoja anatoka Kata ya Zombo akasema Baba nimekupigia mzee wetu tusaidie utuokoe. Nikamuuliza uko wapi na una tatizo gani? Akasema baba nauli huku zimekwishapanda Baba yangu ametoka Dar es Salaam kwenda Ifakara nauli ilikuwa shilingi 14,000 huko nyuma sasa tumeshaambiwa ni shilingi 18,000.

Sasa nazungumza na wenzangu ndiyo maana unasikia kelele tunaomba ututetee huko, nikamjibu Serikali na Wabunge wote kwa kauli moja wako pamoja wanajadili namna ya kuweza kuleta unafuu utakaowezekana kulingana na hali halisi ya nchi yetu ilivyo kwa wakati huu. Vuta subira! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ni mfano wa hisia za watu wengi tu ambao sasa hivi wako huko vijijini wakitusikiliza, niache upande huo wa masuala ya gharama niende kwenye mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwapongeze sana *TRA* kwa jitihada kubwa ambayo wameifanya kwa kuongeza sana kiwango cha makusanyo ya mapato ya ndani lakini kikubwa zaidi Serikali sasa ijikite katika kuhakikisha inaelekeza matumizi ya *investment* ya fedha zinazopatikana kwenye miradi hiyo inayoitwa *Quick Wins* ili maendeleo ya kiuchimi mtambuka yaweze kupatikana na kuwagusa Watanzania wote. Hapa ninaenda haraka haraka kwa kuwa kengele ya kwanza imekwishalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuiombe Serikali iwashawishi wahisani kuingia ubia ili Bandari ya Dar es Salaam iboreshwe na kupanuliwa kuwa ya kisasa sambamba na kuiimarisha reli ya kutoka Dar es Salaam mpaka Kigoma na itakavyojengwa basi ijengwe kwa reli zenye uzito wa paundi 120 ili tusiwaachie nchi jirani zetu wakachukua

ukiritimba wa kunufaika kusafirisha mizigo peke yao kwa nchi jirani ambazo sisi tuna nafasi kubwa ya kufarijika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haraka haraka nitaje suala la utalii kuchangia kwa kiwango kikubwa sana katika mapato ya nchi yetu. *Mikumi National Park* ni eneo moja ambalo ni kivutio kikubwa lakini kama limeachwaachwa hivi, miaka michache iliyopita kulikuwa na *Mikumi Wild Life Lodge* ambayo iko *strategically located* ilibinafsishwa halafu ikatokea mgogoro ikaingia kwenye kesi haijulikani kesi hiyo imeshakaa tayari mpaka sasa ni miaka sita au saba na hakuna kinachoendelea mpaka mwaka juzi ilishika moto, kinachoendelea hakijulikani. Tunakalia utajiri wakati sisi wenyewe tunatafuta fedha, Serikali ichukue hatua za haraka kumaliza tatizo hili kwani wawekezaji wanalimezea mate eneo lile kwa ajili ya kuwa tayari kuwekeza ili tuongezee mapato katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifurahi sana Waziri wa Fedha alipogusia suala la kuboresha malipo ya wazee wastaafu. Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, ukurasa wa 28 Ibara ya 105(b) inaeleza kabisa kwamba Serikali itakaposhika madaraka itaweka mikakati ya kuboresha malipo ya wastaafu yanayolingana na gharama za maisha za wakati huo. Wastaafu ndiyo msingi wa sisi tuliopo hapa leo wameilea nchi hii na kufanya kazi kubwa ambapo tumeendelea sisi kuwa kama tulivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwaenzi, maisha yao yanaondoka haraka kumalizika, kwa hiyo, wapeni nao raha waonje matunda ya Serikali ya Awamu ya Nne kwa kuongeza viwango vya malipo ya pensheni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shilingi 21,000 za mwaka uliopita piga tu hesabu za kisanyansi kwa *interest* na kadhalika na *loss value of money* sasa hivi angekuwa anapata hata shilingi 40,000/= au 50,000/= angalau basi Serikali inachukua muda mrefu mno kutimiza azma hiyo. Tunaomba Serikali iharakishe hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni matumizi ya mapato yatakayopatikana. Kanuni zibadilishwe ili wale watakaoonekana wamezembea au kusababisha hasara katika Idara mbalimbali za Serikali na Halmashauri wachukuliwe adhabu za papo kwa papo. Katika Idara za Serikali au Halmashauri, Idara ambazo zitakuwa zimepoteza fedha kwa mwaka ule wa fedha kiwango kilichopotea *automatically* kipunguzwe katika Bajeti itakayopangwa kwa mwaka ujao kama sehemu ya kuwadhibiti wasipate fedha za kuchezea chezea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja nikiamini kwamba Serikali itazingatia ushauri na mawazo mengi borefu yaliyotolewa na Bunge lako kupitia Wabunge. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Clemence Lyamba, naomba sasa nimwite Mheshimiwa Fuya Godwin Kimbita na Mheshimiwa Ali Khamis Seif, ajiandae.

**MHE. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na niseme kwamba tangu tumechaguliwa kuwa Wabunge kwa sababu sisi wengine ni wageni nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa sababu Bunge la Bajeti lililopita sikuwepo nilikuwa katika matibabu, kwa hiyo, namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa mimi kuwepo siku hii ya leo na ninalazimika tu kusimama hapa kwa sababu ya kuchangia hizi hoja zilizopo mbele yetu. Sina matatizo na Bajeti awali ya yote naiunga mkono asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitoe hongera na pongezi kwa Serikali ya Awamu ya Nne inavyojitahidi, tunafahamu iliyoyakuta baada ya kuingia madarakani lakini ikapambana nayo Mungu akawa pamoja nasi, mambo yakatekelezwa na kuwa shwari. Sasa cha ajabu kinachonishangaza kidogo kwa wale wacheza mpira kuna *penalt* inapigwa goli linaingia wavuni lakini upande wa pili wanasema hapana hiyo ni *offside,* umeshawahi kuona *offside* kwenye *penalt? (Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba ufikishe ujumbe kwa Mheshimiwa Rais, mpira uingie katikati mechi iendelee na sisi tusonge mbele. Hakuna *offside* kwenye *penalt* jamani tosonge mbele, naomba nianzie hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe pongezi kwa Serikali kwa kazi nzuri inayofanyika na niungane na Waheshimiwa Wabunge waliotangulia kutoa pole kwa ajali zote ambazo zimetokea, nadhani utararibu utafanyika katika kuimarisha vyombo vyetu hivi vya usafiri. Lakini, tunawaombea Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi, *Amin!*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitangulie kusema kwamba tafsiri ya hii Bajeti ni mwanzo wa kujitegemea. Ni mfano wa gari ambalo limenasa ndani ya tope, ili lile gari lianze kwenda tunalisukuma hapo katikati tunaanza kuogopa na kuanza kusema ah! turudi hili gari lirudi tena katika kunasa kwenye matope. Sisi tumenasa kwenye matope kwa kurudi nyuma tunataka tuondoke hapo na tuanze kujitegemea na haya mengine yote tunayoyapigia kelele hapa sawa ni gharama. Jamani wanasema hata starehe gharama pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliamua katika mkutano wa mwezi wa Aprili kwamba tutaishauri Serikali tufanye kila liwezekanalo tuweze kuimarisha miundombinu pamoja na shughuli nyingine zote za maendeleo. Mimi nashangaa sana leo tunaanza kulalamika sana kana kwamba tulikuwa tunawachuuza wenzetu, hapana! Tulikubaliana sote kwamba tusiwe na wasiwasi kwamba unapoamua jambo ambalo unaliamini ni vizuri ukaweza ukalitetea. Tutoke hapa twende kwa wananchi wetu majimboni tukawaelimishe nini maana ya hii Bajeti, nini maana ya kuondoka katika kutegemea ufadhili wa nje huu ni mwanzo tu. Mimi nina imani kubwa sana tukiendelea vizuri namna hii hatimaye Bajeti yetu utegemezi wa nje utapungua sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia kuungana Afrika Mashariki sasa hivi, wenzetu Kenya nadhani Bajeti ya mwaka uliopita nje walikuwa wanategemea kwa 7% tu lakini sisi tunataka tudidimie zaidi ili tuwe soko la Kenya, hapana! Tuendelee vizuri ili tuweze kukwamua Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza hii Bajeti ilivyo ukiiangalia kwa kina kipaumbele nina elimu, tumekuwa tukilalamika sana katika ku-*balance* maendeleo ndani ya nchi yetu. Malalamiko mengi yamekuwepo na kwa bahati mbaya masuala haya ni katika sehemu za nchi, Majimbo na wapi. Wenzetu wa Kusini wanalalamika na sehemu nyingine wanalalamika. Lakini tukiangalia sehemu zingine za nchi zilibahatika kidogo kutokana na jiografia, wale waliowahi kuja ndani ya nchi kutokana na hali ya hewa wakaenda sehemu zingine. Lakini Bajeti hii inatusaidia ili nchi yetu tuweze ku-*balance* maendeleo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningejishangaa mwenyewe pia kama nisingeunga mkono Bajeti hii. Kule kwetu Kilimanjaro, mimi ni Mbunge wa Hai. Watu wanadhani Kilimanjaro tumeendelea kupita kiasi, tuna shule nyingi, zile shule ni za Kitaifa. Hata ndugu zangu wengine wengi mmesoma huko, zile shule ni za Kitaifa, hatuna shule zile za kusema ni za watoto wa Kilimanjaro tu, ndiyo sasa hivi tumeanza kujenga shule. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kutuita ofisini kwake kutueleza kwa nini shule hatujazijenga na watoto wa shule za sekondari tuliokuwa tumewachagua ni wachache. Sisi tumeingia madarakani tangu tumechaguliwa mwaka mmoja na nusu sasa hivi karibu. Tulikuwa na uwezo wa kuwapeleka watoto asilimia 40.2 tu shule za Sekondari. Hivi ninavyozungumza tumewapeleka watoto asilimia 89. Maana yake zile shule ni za Kitaifa, walikuwa wanasoma watoto wa nchi nzima. Kwa mfano, Jimboni kwangu nina shule mbili za Kitaifa *Machame Girls* na *Njamongo Secondary School* ilijengwa na *KNCU* wazee wetu wa kahawa. Lakini kwa mwaka huu hata watoto walioingia kutoka Wilaya ya Hai hawafiki 10. Hivi tusingejenga hizo shule sasa hivi hao watoto wangeenda wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naishukuru Serikali kwa kasi hii tunayokwenda nayo, tuongeze mwendo. Kwa kipindi hiki tumeweza kuwa na shule za sekondari 17 mpya ndani ya Wilaya ya Hai ndiyo maana tumefikia hiyo asilimia 89. Wananchi wanashukuru. Sasa mtu anakuja kusema hapana Bajeti hii haifai, Bajeti hii ni nzuri, elimu ni kipaumbele. Elimu itatusaidia kuondokana na matatizo. Haya maendeleo tunayoyazungumzia hapa kuhusu wananchi wetu watakuwa na uelewa mkubwa zaidi wa kuelewa nini tunachokizungumza. Hivi jamani tusipowasomesha watoto wakati tunazungumzia sasa hivi tuingie katika dunia ya viwanda, hivi hao watu watakuja kufanya kazi viwandani bila kuwa na elimu. Kipaumbele cha elimu mimi nakipongeza na Mheshimiwa Waziri wa Fedha nampongeza sana kwa hilo pamoja watendaji wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu barabara ni kipaumbele kingine hicho. Kilio chetu siku zote kimekuwa ni barabara. Sasa mimi nisipounga mkono Bajeti hii ili barabara yangu ya Kwasadala- Masama Mheshimiwa Rais aliahidi kuiweka lami itajengwa na nini? Kama sikuunga mkono Bajeti hii itajengwa na nini? Kuna Mlima Kilimanjaro uko pale, cha kushangaza ni kwamba Mlima Kilimanjaro unavyoleta mapato ya Kitaifa tunashangilia. Lakini tunapotaka kurekebisha ile miundombinu ili kwamba yule mzee kutoka nchi zingine ambaye hana uwezo wa kuupanda ule Mlima anataka akae kwenye *van* yake nzuri azunguke ule mlima kwa kuangalia tunapiga kelele wapi na wapi. Fedha zikija tunazikubali, barabara ikijengwa tunaikataa, haiwezekani lazima

tuikubali. Naomba tuongeze mwendo, Bajeti hii ni nzuri, barabara ziendelee kujengwa katika nchi nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesikia matatizo makubwa sana kule Tunduru kwa Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, watu walinasa, kuna matatizo makubwa. Kuna kipande cha barabara kinazungumziwa kule Kusini kwa rafiki yangu Mudhihir Mudhihir, kule. Lakini tukikusanya mapato vizuri na tukiyaongeza barabara zitajengwa. Kwa hiyo, mimi naomba tukubaliane juu ya hilo hata kwa Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba jirani yetu huko. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi nazidi kusema kwamba Bajeti ni nzuri ili tuweze kujitegemea na asilimia kubwa tuweze kujenga hizo barabara zetu pamoja na kupata huduma zingine muhimu. Jamani tukitegemea wafadhili lazima tuseme ukweli, hakuna mfadhili yeyote aliyepo tayari kutusaidia sisi tuweze kunyanyuka, wanataka tuwe omba omba. Tunadanganywa danganywa na mipango mingi. Pale Wizara ya Fedha nadhani kuna *terminology* mbalimbali, mkakati huu, ahaa, mimi naipongeza Serikali kwa sababu tunataka tuanze kujitegemea. Tufikie mahali kwamba hatutegemei wafadhili tunaweza kujitegemea na kujiendesha sisi wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti yetu imetoa kipaumbele kwa mambo ya Afya. Itakuwa namna gani tunataka mambo mazuri halafu tunayalalamikia haya yanayoyaleta haya mazuri. Afya ni kipaumbele muhimu sana, tukiimarika kiafya nina uhakika kabisa tutaondokana na hayo maradhi, tutapata elimu nzuri, watoto wetu wataweza kupata elimu nzuri na watoto wetu wataweza kusoma kwenye hizo shule ambazo tunazijenga na tutaweza kuendelea mbele vizuri kushindana na wenzetu ili na sisi tusije tukaachwa nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yamekuwepo malalamiko kidogo kuhusu kilimo, mimi naamini kilimo hakijasahaulika sana. Kilimo kinaguswa kwa njia nyingi sana hizo fedha ambazo tumeambiwa zitaenda kwenye Halmashauri zetu. Kwenye Halmashauri zetu sisi ni wakulima, kwa hiyo ina maana kwamba hizo fedha zinakuja kwetu sisi wakulima na wakulima kazi yetu ni kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nisipounga mkono Bajeti hii nimezungumza na Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika na Manaibu wake kuna lile banio la pale Mijengweni litajengwa kwa kitu gain, si lazima tuwe na fedha tuweze kulijenga lile banio la maji kwa ajili ya umwagiliaji kule tambarare?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazidi kusisitiza kwamba Bajeti ni nzuri, vipaumbele vimetiliwa maanani kabisa, tusiogope twende tukawaelimishe wananchi wetu nao watatuelewa vizuri tu. Kwa hiyo, kilimo nacho natumaini kimezingatiwa fedha zitaenda huko na kilichowekwa pale ni kile tulichonacho. Mkono unajikuna pale unapofikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipaumbele kingine ni cha maji. Maji ni muhimu kwa ajili ya kuokoa afya zetu na kufupisha muda ili akinamama wapate muda wa kwenda kufanya shughuli nyingine za uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa tafsiri nyingine ningependa kusema tu kwamba tunaondoka kwenye *system* ya *analogue* kwenye Bajeti sasa tunaingia kwenye *digital* papo kwa papo. Tuachane na mambo ya zamani *analogue* ilishapitishwa na wakati, hii ni *digital*. Kwa hiyo, mimi nazidi kuipongeza Serikali na kusema kwamba tutilie mkazo. Lakini naamini yale mengine ambayo labda tuona kwamba itakuwa ngumu zaidi busara na hekima zitatumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka siku za hivi karibuni mwanzoni mwa mwaka huu kulikuwepo na *premium* kubwa kwenye viwanja Serikali ni sikivu ikasikia vile viwango vikubwa ambavyo walikuwa wameona kuimarisha miundimbinu kwenye viwanja vya mijini na wapi ikarekebisha *five percent* mambo yakawa mazuri. Sasa cha kuomba ni kile ambacho kaka yangu Felix Mrema analilia hapa *mortagage* kwenye mambo ya benki haya kukopesha watu wetu ili waweze kujenga nyumba bora.

Kwa hiyo, mimi ningeomba tulitilie mkazo ili wananchi wetu waweze kujenga bora na uchumi ulioimarika biashara ni nyumba. Unajenga nyumba unauza na nyingine unapangisha. Mimi ningeomba tuelekee huko ili kwamba na hivyo vyombo vya fedha viweze kutoa fedha tusije tena tukasema wale watu tuwanyang'anye vile viwanja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ufugaji ndugu zangu wameishalizungumzia sana. Kwa sababu kwa Ukanda wa kule tambarare nafahamika kama Fuya Kimbita . Kwa hiyo, lazima niwasemee ndugu zangu. Kwa hiyo, lazima tuzingatie sana ufugaji na Mheshimiwa Chrisant Mzindakaya nampongeza kwa sababu amesema ata-*export* nyama kwenda Ulaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa zile *cc* za magari wenzangu wameshalizungumzia niwaombe waangalie na tuwe na jicho la huruma pale. Kuna magari madogo kwa mfano, mimi pale Wilaya ya Hai kule milimani hatuna mabasi, tunatumia *pick ups*. Sasa hayo magari ambayo *cc* ziko chini ya 5000 lakini yanatoa huduma kwa wananchi, ningeomba tuliangalie. Pale Dar es Salaam nimeona *bajaj* ndizo zinazotumika sana sasa hivi nazo tuziangalie ili kwamba wale wananchi wasipandishiwe sana zile nauli baada ya mafuta kupanda bei, lakini na hizo *cc* tena zisiwe ndiyo mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utalii natumaini mipango iliyopo mbele yetu ni mizuri sana inayokuja. Utalii utaimarishwa vizuri na kudhibiti ile mianya yote. Katika kuuza zile hisa za *NMB* yasije yakatokea yale yaliyotokea katika kuuza hisa za *Twiga Cement.* Taasisi za fedha kubwa ziliruhusiwa kwenda kununua zile hisa, tuweke utaratibu ambapo zile hisa zitanunuliwa na wananchi tu wazalendo ili tusije tukajikuta na kile kilichotokea *Wazo Hill,* watu walinunua hisa, lakini walirudishiwa fedha zao. Kwa hiyo, tuwe waangalifu kwa maana ya kuwasaidia Watanzania na wala siyo hayo Makampuni. Kuna Kampuni moja ilinunua hisa za *three billion*, sasa sisi wananchi tutafanya nini? Kwa hiyo, ningeomba na hapo tupaangalie pia, tufanye haraka katika kuagiza mafuta kupitia *TPDC.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba pia baada ya makusanyo yote mazuri, niiombe Serikali iwe na usimamizi mzuri ili kudhibiti mianya yote ambayo inaweza

ikatuharibia. Mimi naipongeze *D by D*, miradi yote inayosimamiwa na wananchi ime-*improve* kwamba inaendelea vizuri, tunayo mifano ya miradi ya *PADP* ambayo naamini kabisa ile ni mifano hai katika kutuletea maendeleo na Miradi ya *TASAF.* Kwa hiyo, mpango wa *D by D* ni mzuri sana naipongeza Serikali kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe wenzangu wakiwa wametulia wakaanze kusoma kitabu cha Mheshimiwa Waziri wa Fedha kuanzia ukurasa 36 vile vipaumbele vya Bajeti ya mwaka 2007/2008 wataweza kuelewa vizuri kabisa ni kwa nini nimeunga mkono Bajeti hii na kuitetea kwa nguvu zangu zote. Kwa sababu ukishasoma kuanzia pale utaona mwelekeo. Kwa hiyo, niwaombe kabisa kwamba mpira urudi uwanjani tusonge mbele tusizidi kupoteza muda, kule nyumbani tunasema kwamba tumechelewa lazima tuanze haraka haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, mimi nizidi kusema kwamba naunga mkono Bajeti hii . Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia Bajeti ya mwaka 2007/2008. Lakini lingine niwapongeze Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na Mheshimiwa Kabwe Zitto kwa kuwasilisha maelezo mbadala kuhusiana na Bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wapinzani hatusemi kwamba wananchi wasitoe kodi wala sisi Wapinzani hatusemi kuwa miradi siyo muhimu, lakini tunachosema sisi Wapinzani kuwa kuongeza ushuru wa kodi ya mafuta kulikuwa hakuna ulazima kama Serikali ingekuwa makini zaidi katika vyanzo vingine vya mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia suala la uvuvi. Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kipindi cha mwaka 2007/2008 katika sekta hii inatarajia kukusanya 8,055,421,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hiki ni kiwango kidogo mno. Sasa sisi tunasema kuwa ili wananchi wasiongezewe ushuru wa mafuta basi kwa sababu kuna meli zinavua katika Bahari yetu ya Hindi; na kwa mujibu wa kikao cha tatu katika mwaka 2004 mwezi Februari, Serikali ilijibu swali hapa kwa kusema kuwa kuna meli 193 katika Bahari ya Hindi zinavua samaki. Sasa sisi kwa sababu hatutaki tukuze mapato kwa kiasi hicho, tukasema tuchukue meli 140 tu ambapo ushuru wa sasa ni dola 18,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli mtu kumkabidhi Bahari ana meli na ana zana za kisasa za kuvua samaki halafu kwa mwaka ukamtoza dola 18,000 kwa kweli ni kutokuifanyia haki nchi yetu. Sisi tunasema katika nyanja hii basi wamtoze kodi ya dola 100,000. Kwa maana hiyo, ukichukua meli 140 kwa hiyo, Serikali yetu ingepata shilingi bilioni 19. Sasa Wizara ya Maliasili na Utalii inatwambia mwaka 2007/2008 basi itakusanya shilingi bilioni 8, wakati sisi hapa tuna uwezo wa kukusanya shilingi bilioni 19. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine katika uvuvi ukiangalia mrahaba wa mauzo ya bidhaa za samaki, tulifanya makisio kuwa tukijaliwa kwa mwaka meli 140 kila meli

itapata tani 2000 na ukichukua thamani ya samaki tuseme ni dola 2.5 za Kimarekani tutoe mrahaba wa asilimia 10. Kwa hiyo, hapa tulikuwa na uwezekano wa kupata shilingi bilioni 740. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango huu kuna suala la bandari za samaki, Mtwara, Dar es Salaam, Tanga na Zanzibar. Bandari hizi ili ziuze mafuta, chakula na maji na mambo mengineyo. Hapa tunasema kuna uwezekano wa kupata bilioni 3.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Idara ya Uvuvi au sehemu ya uvuvi kuna uwezekano wa kupata shilingi bilioni 762. Sasa linganisha na shilingi 855,421,000 ambazo zinategemewa katika uvuvi kutokana na Wizara ya Maliasili na Utalii. Sasa tunaposema kuwa hakukuwa na haja ya kuongeza ushuru wa mafuta maana yake kwa kweli ni hiyo kuwa tufanye kitu mbadala ambacho kitakuwa haikiwaathiri watu wote. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia utalii, Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Bajeti hii ya mwaka 2007/2008 inategemea kupata shilingi 1,182,006,793. Hiki ni kiwango kidogo mno. Tanzania ina vivutio vizuri vya utalii. Kwa hiyo, kiwango hicho hakitoshelezi hata kidogo. Tanzania ilikuwa na nia ya kuleta watalii milioni moja, lakini imefikia kiwango cha 644,124. Sisi tunasema tusichukue 600,000, tuchukue nusu tu ya hao yaani 322,062 kati ya watalii hao kila mtalii atupatie dola 100 kwa siku, akikaa siku saba tu. Tutoze asilimia 30, kwa hiyo, hapa tuna uwezo wa kukusanya shilingi bilioni 67.5. Ukilinganisha na shilingi bilioni 1.1. Kwa hiyo, tunaposema kuwa hakukuwa na haja ya kupandisha ushuru wa mafuta. Hiyo ndiyo maana yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uwindaji wa vitalu hapa nimpongeza Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe kwa sababu Wizara hii kaichukua hivi karibuni amenishtua kidogo hapa ana nia ya kukusanya shilingi 49,664,881,000. Lakini bado sisi tunasema hapa kwenye uwindaji wa vitalu kuna uwezekano wa kukusanya shilingi bilioni 85. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu misitu ni jambo la kusikitisha sana kuwa Wizara imesema itakusanya shilingi bilioni 15, wakati ukiangalia taarifa ya *traffic* ambayo wamefanya utafiti wamesema kila mwaka Tanzania inapoteza dola milioni 58 za Kimarekani, tunazipoteza kila mwaka na ripoti hiyo ipo Serikalini. Sasa unapokuja kutwambia kwamba misitu itakusanya shilingi bilioni 15 inaonekana kuna upotevu unakuja, huamini na ni kitu ambacho kimefanyiwa utafiti. Sisi hapa katika bidhaa za misitu na nyuki tunategemea kukusanya shilingi bilioni 100 na maelezo yapo katika hotuba ya Waziri Kivuli wa Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya kuongeza viwango vya ada katika mambo mbalimbali, lakini pia Serikali ingeweza kuhifadhi fedha zake kama kungekuwa na utumiaji mzuri wa fedha. Wenzangu wameeleza kuhusu *Twin Towers*, lakini vilevile kuna upungufu wa mapato katika baadhi ya Wizara tano na Idara. Zimepotea shilingi bilioni 73.8 katika *Ferry* ya Kivukoni, zimepotea shilingi milioni 442 *VETA,* zimepotea shilingi milioni 762 na *TANSORT* zimepotea shilingi bilioni 72.3. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa fedha hizo zingeweza kuhifadhiwa zikawepo katika mfuko wa Serikali na zikawa zinachangia vile vile mapato ambayo yanaingia katika Wizara ya Maliasili na Utalii ili kuhakikisha kuwa hakuna ongezeko la ushuru wa mafuta. Kwa hiyo, sisi hatuungi mkono kwa sababu kuna uwezekano mkubwa kama Serikali ingekuwa makini zaidi basi kwa kukusanya mapato kutokana na sehemu ambazo nimeshazitaja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije katika suala la mgao wa 4.5%, limekuwa suala la muda mrefu inaonekana ni zito tumwachie Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri Kiongozi wa Zanzibar wakae wazungumze suala hilo. Lakini mimi nadhani ipo haja acha kiwango kipya kiwepo. Lakini kweli Zanzibar tufikishwe mahali kuwa tuijadili itusaidie nini. Nadhani hiyo siyo sahihi. Umefika wakati Zanzibar ipewe nafasi iweze kujitegemea. Haiwezekani katika ukoo achaguliwe ndugu awe anasaidiwa wakati ana uwezo wa kujitegemea wala haumwi. Sasa leo imefika mahali kila kikao cha Bunge, Zanzibar imefanywa hivi, Zanzibar haijakuwa hivi, nadhani hiyo siyo sahihi. Kwa hiyo, imefika wakati Zanzibar isaidiwe iachiwe nafasi nayo iweze kujitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazo langu ni kuwa nafahamu ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano, lakini imefika wakati suala la ushirikiano, najua kuna Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, lakini kama tunataka kuisaidia Zanzibar iweze nayo kujitegemea basi ipo haja ya ushirikiano wa Kimataifa ipewe nafasi Zanzibar nayo iweze kushiriki katika kutafuta Taasisi mbalimbali ili iweze kusaidiwa kifedha. Vinginevyo tutakaa na huo mgao mpaka lini. Hili kwa kweli si sahihi. Nadhani hata uamuzi utolewe kupitia kwa viongozi wakuu hao inawezekana bado yakaja malalamiko.

Kama kiwango kitakuwa kikubwa kidogo wapo wenzetu wa Tanzania Bara watasema kwa nini nchi ndogo ipate asilimia hiyo. Kama kiwango kitakuwa kidogo sana Wazanzibar watasema kuwa kwa nini wapate hivyo, wakati nchi hizo zilipoungana zilikuwa uhuru, Zanzibar ilikuwa Uhuru ilipoungana na Tanganyika. Kwa hiyo, tunahitaji tupate kitu ambacho kinatutosheleza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ili kuondoa malalamiko mimi nashauri kuwa ipo haja Zanzibar iachwe iwe na Ushirikiano wa Kimataifa ili iweze kujiunga katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, Mashirika ya Kifedha na Taasisi nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ni la mwisho ni kuwa ili kuisaidia Zanzibar ambayo ni visiwa, kilimo hakiweze kikaendelezwa kwa kiasi hicho. Tegemeo kubwa la Zanzibar ni biashara. Kwa hiyo, ile bandari huru ambayo inazungumzwa nadhani kama tuna nia nzuri ya kuisaidia Zanzibar basi ijengwe Zanzibar ili ikuze mapato ya Tanzania na kwa Zanzibar kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa sababu uongezekaji wa ushuru wa mafuta hakuzingatia sana mapato mengine, natamka kuwa siungi mkono Bajeti hii. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. ELIETTA N. SWITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Bajeti hii kama ilivyokwishaandaliwa na Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda niwapongeze sana *Taifa Stars* kwa kutuweka katika ramani ya michezo ulimwenguni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia niipongeze Serikali yetu na hasa Wizara zetu hizo mbili kwa kuandaa Bajeti inayozingatia yale yaliyokwishaandaliwa kutekelezwa na Ilani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia niipongeza Serikali kwa kujitoa katika kukopa mikopo ya hati fungani na dhamana. Hali hii itasababisha Benki zetu kuwa na fedha nyingi ambazo watu wetu wanaweza kukopa na kuwawezesha kufikia maisha bora kwa kila Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kushusha utegemezi toka asilimia 50 mpaka asilimia 39 ni hatua kubwa, lazima tujipongeze. Lazima tujipongeze kwa sababu utegemezi ni fedheha na sisi tumeamua kwamba fedheha hii hatuitaki, kwa hiyo lazima tujitegemee kwa vyovyote vile itavyokuwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania tumekwishazoea kujifunga mikanda. Tumejifunga mikanda katika mambo mengi, katika ukombozi wa nchi za Kusini mwa Afrika na pia tulijifunga mikanda wakati tukipigana na Idd Amin. Watanzania tukiwaeleza vizuri hawawezi kuona kwamba Bajeti hii ni mbaya kwa sababu sisi sote tunapaswa kusonga mbele na Watanzania wako tayari kufanya vitu vya namna hiyo. Maana sasa tunayo vita ya sisi wenyewe ya kupambana na hali mbaya ya uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulipambana na mambo mengine, hili Watanzania wanaliona ni suala ndogo na hasa kama tukienda Rukwa ambapo watu hulima kwa kutegemea kwamba hapo baadaye wanaweza wakakuza maisha yao na watoto wao wakasoma kwa kweli wako tayari kwa vitu kama hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu hujikuna pale mkono unapofikia, Bajeti yetu kwa kuchangia shilingi trilioni 250 tayari tumejikuna mpaka pale mkono wetu unapofikia. Maoni ya Waheshimiwa Wabunge ya mwezi Aprili, 2007 tulisema kwamba tuongeze bei kwenye mafuta ili tuweze kujenga barabara zetu yaani *feeder roads*, wahisani hawatakuwa tayari kuja kujenga *feeder roads* wakati hata barabara zile zinazounganisha Mkoa kwa Mkoa bado wanasuasua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakumbuka mwaka jana wakati Mheshimiwa Basil Mramba akiwa Waziri wa Miundombinu, siku moja aliniambia kwamba niende kwetu nikatangaze kwamba mwanzoni wa mwaka huu baragara ya Tunduma-Nyakanazi itaanza kujengwa. Lakini kwa mtindo ule ule wa wafadhili wakasuasua huko mpaka leo hii ile barabara haijaanza kujengwa japo maandalizi yake yapo njiani, lakini hiyo barabara haijaanza kujengwa. Ingekuwa fedha hizo ziko mfukoni mwetu hiyo barabara kwa kweli tangu mwezi Januari, mwaka huu ingekuwa imeanza kujengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge, tulipokuwa tunasema kwamba mafuta yaongezwe bei hatukusema kwamba mafuta ya taa yasiongezwe bei. Mimi nafikiri hapo na sisi tulikosea. Sasa labda tujikosoe hatukusema kwamba mafuta ya taa yasiongezeke bei. Tulisema tu mafuta yaongezwe bei ili tuweze kuunda Mfuko utakaoweza kujenga barabara zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mauzo madogo ya nchi yetu ukilinganisha na mauzo mengine ni kikwazo kikubwa. Wale wachumi wanafahamu ule msemo wao unaosema; "*the more you produce the rest the cost*." Sasa sisi tunakufa na hili kwa sababu tunazalisha kidogo sana. Tukizalisha kwa wingi na tukinunua kidogo maisha ya Mtanzania yatakuwa bora zaidi na hatutakuwa na matatizo makubwa kama tuliyonayo. Lakini suala la kupiga hatua kutoka kwenye Bajeti tegemezi kwenda kwenye Bajeti ya kujitegemea ni muhimu na ni lazima. Kwa hiyo, naomba tuendelee na Bajeti yetu na nasema ninaiunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tukiweza kuuza mazao mengi zaidi na vitu vingine na vile tunavyozalisha tutajenga barabara nzuri, tutajenga shule zetu nzuri na tutaendelea kujenga kama tunavyofanya sasa na tutakuwa na kilimo chenye tija na tutaweza kueneza umeme. *(Makofi)*

Nakumbuka hivi juzi Mheshimiwa Rais alifika kwetu Rukwa akawa ametupa moyo kwamba hivi karibuni Serikali yetu iko tayari kutusaidia sisi Wanarukwa kujenga barabara nzuri kwa kupitia wafadhili yaani barabara ya kutoka Tunduma kwenda Nyakanazi, kutoka Chala kwenda Kipili na Kirando. Kutoka Sumbawanga kwa kupitia Matai kwenda mipakani Zambia lakini pia Mheshimiwa Andrew Chenge ninaomba asije akatuchengesha huko mwishoni, alitoa ahadi kwamba yeye atasimamia ujenzi wa barabara zote za *TANROAD* na hasa hizo ambazo wafadhili wa *World Bank* walikuwa wamekwishaahidi. Kumbe Bajeti yetu kama inatosha zile barabara za *Feeder Roads* nina hakika zitajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu mara kadhaa kuanzia mwaka jana alisimama mbele ya Bunge hili letu Tukufu akatuhamasisha sisi wote Wabunge kwenda kuhamasisha ujenzi, kilimo cha mazao ya *bio-diesel*. Je, ni Wabunge wangapi wamekwenda kuhamasisha *bio-diesel crops*. *Bio-diesel* itatusaidia Watanzania kutokana na hizi bei za mafuta tunazolalamika hapa kwa sababu kwa mfano kilimo cha Mbono tutapata *bio-diesel* ambayo itatusaidia kuendesha mitambo yetu yote. Lakini pia mafuta yake yanaweza kutumika kama mafuta ya taa, kwa hiyo, hatutakuwa na tatizo la kupiga kelele juu ya mafuta ya taa, kila mtu huko nyumbani atazalisha mafuta kutokana na yale mazao aliyolima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri zetu zinatuumiza sana. Waendeshaji wa Halmashauri wana matumizi mabaya ya fedha za wananchi. Kwa mfano, Sumbawanga mara mbili wamepata hati chafu, hawa watu hata ungewaambia wafunge mkanda watakuuliza mara mbili lakini nafahamu kwamba Watanzania wengine huwa hawaulizwi maswali ili mradi wanajua kwamba wanapojifunga mkanda watafaidika na suala walilolifanya. Lakini kwa upande wa Sumbawanga labda mahali pengine pia ningeomba

Serikali isimamie matumizi ya fedha za wananchi ili Bajeti yetu isije ikayumba. Uwezeshaji wa wananchi ni kitu muhimu na hasa pale ambapo Serikali imekubali katika Bajeti yetu kuwawezesha wananchi kujenga nyumba kwa kutegemea mikopo, lakini pia kufanya biashara kwa kutegemea mikopo na kwa kuwa Serikali haiwezi kujihusisha katika kukopa basi hizi fedha ningependa ziende moja kwa moja kwa wananchi ili waweze kujenga nyumba na kila mtu awe na maisha bora. *SACCOS* zetu nyingi bado hazijawa na nguvu. Kumbe ningewaomba Waheshimiwa Wabunge wote pamoja na kwenda kuhamasisha na kuwaelezea juu ya Bajeti hii iliyo nzuri waende wakahamasishe *SACCOS* zetu ziwe na nguvu ziweze kukopesheka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukaguzi wa mizigo bandarini ni kitu muhimu kwa usalama wa nchi yetu lakini pia kwa mapato kwa sababu walio wengi si waaminifu watapitisha ile mizigo pasipokukaguliwa watakuwa wameweka kitu kingine halafu juu anaweka *label* anayoifahamu yeye. Vyanzo vipya vya uchumi ni muhimu, vyanzo vipya na masoko ya mazao yetu yatafutwe ili Bajeti yetu iweze kupata *support* kutokana na vile vyanzo vitakavyokuwa vimeongezeka ili tutakapofika mwakani basi tuweze kulegeza mikanda na kuendelea na maisha yetu vizuri zaidi. Katika vyanzo vipya naiomba Serikali iweze kuwaleta wawekezaji wengi Mkoa wa Rukwa kwa sababu sisi tuna uvuvi, madini, kilimo, tuna ardhi nzuri na watalii watakuta wanyama kibao, wa hiyo mwakani bajeti yetu itazidi kuwa rahisi.

Leo tunapiga kelele kupanda kwa mafuta kama ilivyoelekezwa katika Bajeti yetu. Je, watakapopandisha wenzetu wanaozalisha mafuta tutasema nini? Mimi naona tuendelee na Bajeti yetu bila ya kurudi nyuma ili tuweze kupiga hatua. Sipendi nikaendelea kupigiwa kengele ya pili, ninaomba niishie hapo. Ahsante sana Mwenyekiti. *(Makofi)*

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia kwa kiasi fulani Bajeti ya Wizara ya Fedha ikiwa na mpango kamili wa Wizara ya Mipango. Hizo Wizara mbili zinakwenda pamoja kama mapacha kwa sababu Wizara ya Mipango inaandaa na Wizara ya Fedha inapokea halafu na Wizara zingine mnaunga kwenye fikra hiyo ndiyo tunakwenda tunafanya kazi hii.

Niwapongeze sana Mawaziri wa Wizara hizo pamoja na wasaidizi wao kwa Bajeti nzuri kabisa ambayo imeandaliwa, Bajeti ambayo imeletwa kwetu tumesomewa hapa kila Mheshimiwa Mbunge humu ndani ameifurahia na wananchi wamefurahia pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda kabla ya kuendelea niungane na wenzangu kwanza kwa kuwapa pole wale wananchi waliopatwa na ajali ya kupoteza maisha yao kule Singida na pia wale ambao waliopoteza maisha nao niwatakie ama niwaombee kwa Mwenyezi Mungu roho zao ziweze kufika huko milele na milele. *(Makofi)*

Mimi kuanzia mwanzo nasikiliza malumbano humu ndani kweli ilifikia mahali nikasema sasa mwelekeo tunakokwenda ni kwamba kuna giza ambalo kama hatutakuwa makini tukiingia mle ndani itakuwa ni kazi kubwa sana kujikwamua. Nilikuwa nafikiria

siku moja nilikwenda kule Nairobi nikawa nje ya ukumbi wa Wabunge walikuwa wanazungumza humo ndani. Mbunge anatoka humo ndani akimbizane na mwenzake kwa sababu humu ndani amezungumza kitu cha kumuudhi mwenzake. Niliona hili ni hatari, sio hali ya kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, michango mingi imetolewa lakini ile inayotolewa inakanusha moja kwa moja kwamba Serikali ya Awamu ya Nne haijafanya kazi, mimi nashindwa kuelewa. Nashindwa kuelewa kwa sababu leo hii Waziri Mkuu akisema kwamba aende kwenye jimbo la kila Mbunge, Mbunge ambaye amekuwa Mbunge kwa muda wa mwaka mmoja na nusu kama tulivyo humu ndani kuangalia Mbunge amefanya maendeleo gani jimboni, Mheshimiwa Waziri Mkuu atatufukuza kazi, leo hii. Sasa leo tunaiweka kizimbani Serikali kwamba haijafanya kitu kwa muda huo huo ambao Mbunge ulitakiwa pia uwe umefanya kazi, sasa hapo tunakwenda wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niipongeze Serikali ya Awamu ya Nne kwa kasi ambayo inakwenda nayo, na pia napenda nimpongeze Waziri Mkuu anavyoongoza Baraza. Hawa Mawaziri jamani sijaona Waziri aliyenenepa humu ndani, wote wamekonda. Wamekonda kwa sababu wanafanya kazi, hawakai kwenye viti, saa zote wako safarini na Waziri Mkuu anawaendesha kweli kweli wanafanya kazi, Waziri Mkuu endelea na uzi huo huo. Hapa mkisema Mheshimiwa Waziri Mkuu amesema uteua Waziri kutoka huku kwa *back bencher* wengine watasema hapana Uwaziri wako chukua, kwa sababu wanaogopa suluba ambazo wanazipata Mawaziri hawa. Sasa *from nowhere* tunaanza kulinganisha Baraza la Mawaziri la Ufaransa na Baraza la Mawaziri hapa Tanzania. Ufaransa ambayo imeendelea, Mbunge humu ndani unazungumza unasema kule Mawaziri wa Ufaransa ni wachache, Baraza la Mawaziri la Tanzania ni kubwa linatakiwa kupunguzwa wakati tunatafuta maendeleo na bila hao Mawaziri hatuwezi tukaendelea, Waziri ana kazi yake ya kufanya humu ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge kabla ya kuzungumza kama huna la kuzungumza afadhali ukakaa tu sio lazima uzungumze. Mimi nasema kwamba kila asubuhi tunapoingia hapa Bungeni huwa tunaombewa dua hapa. Mheshimiwa Spika anasoma dua, hii kama ishara ya kuonyesha kwamba mambo yote tutakayozungumza humu ndani yatabarikiwa na Mwenyezi Mungu ndiyo maana ya dua hii. Sasa tukikiuka dua tunayoombewa humu ndani kwa kweli tunakuwa tunakwenda mbele na nyuma kama msumeno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napenda kuzipongeza hizo Wizara kwa Bajeti nzuri lakini tuna chombo cha *TRA,* chombo kinachokusanya mapato, kilio chetu humu ndani ni mapato tunasema sungura mdogo, sungura ni mdogo kwa sababu hatuna fedha, tuna chombo kizuri cha kukusanya fedha. Wameweza kukusanya asilimia 109 mpaka mwezi Mei mwaka huu na tunapokaa humu ndani mikakati walionayo *TRA* ni kukusanya 3.4. Sasa kama hatuwezi tukakaa tukapongeza tukasema tuna mwelekeo mzuri, mimi nasikitika kusema kwamba ambaye atakwenda tofauti na hapa atakuwa anapoteza dira yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia kuuza ndege ya Rais, ndege ya Rais wa nchi. Tumetumwa na wananchi wetu kuja kuzungumzia ndege ya Rais humu ndani.

Tutaiuza namna gani? Kama ni mtoto wa kuzaa unamwambia ni utovu wa nidhamu, ndiyo. Mtoto wa kuzaa anakwambia baba uza hilo gari utamwuliza kwa nini niliuze. Sasa kusema kweli ni kama kitendawili sielewi, kama ndiyo siasa, siasa haiendi namna hiyo. Hata huko aliko huyo Rais wa nchi akisikia Wabunge tumekutana humu ndani na tunazungumza kuhusu kuuza ndege ya kwake eti tuongeze kipato nadhani atasononeka sana. *(Makofi)*

Napenda kwa pekee kabisa nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa sana anayoifanya. Tulipokutana hapa kwa mara ya mwisho alipanga safari kwa Mawaziri wote wakatimuka. Tulikuwa na matatizo katika lengo la kufanikisha elimu. Mawaziri walitimka Mikoa yote, Wilaya zote, wamekwenda wamezunguka kule na leo hii kila Mbunge akitoka humu ndani akienda jimboni kwake atakachojivunia ni elimu kwa sababu madarasa yamejengwa, huna utakachojivunia zaidi ya elimu ambayo kwa kweli aliyeanzisha ni Waziri Mkuu kuwatuma Mawaziri waende wasimamie na Wabunge tumekwenda kule nyuma kwenda kusimamia na ndiyo tukienda tutajivunia hilo.

Nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu kama ulivyofanya kwenye elimu basi hata kwenye afya na kilimo ufanye hivyo, utusaidie Wabunge, fanya hivyo hivyo Mawaziri watimuke wakafanye kazi hiyo.

Mheshimiwa Waziri Mkuu mbali na kazi nzuri ambayo imefanyika kwa kuboresha suala la elimu kwa kweli kuna tatizo ambalo ni vizuri sasa Wizara ya Elimu ama Wizara inayohusika iangalie namna ya kulitatua. Kuna mikoa ambayo ina matatizo, mikoa ambayo haina umeme. Juzi Mheshimiwa Rais amekuja Kigoma na kule tumempokea kwa shangwe sana. Uwanja wa Ndege watu walikwenda na majembe, watu wamekwenda na vibatari na majembe. Vibatari vile, ndiyo ilikuwa inaonyesha kwamba wananchi wa Kigoma wanataka umeme na wanataka vyombo vya kisasa vya kulimia, ndiyo asili ya mapokezi mazito ya Rais ya namna ile. Sasa mimi naongeza lingine kwamba pamoja na ufanisi mzuri ambao kusema kweli Serikali imesimamia nilikuwa nadhani kwamba ni vizuri kwa mikoa ile ambayo ina matatizo kama Mkoa wa Kigoma basi tuanzishe zoezi la kuweka *solar* kwenye shule hizi za *boarding* ili watoto wasome.

Mimi nimejitolea mwenyewe nina utaratibu wa kuweka *solar* kwa shule za sekondari na Mbunge mwenzangu Mheshimiwa Christopher Chiza, Mbunge wa Buyungu. Tunafanya hivyo kwa kuweka *solar*. Watoto ambao walikuwa wanaondoka shuleni saa nane wanasoma mpaka asubuhi kwa ajili ya kufurahia umeme. Sasa nilikuwa naomba Wizara inayohusika ili Wabunge tusije tukajitolea sana mwisho tutashindwa kusomesha watoto. Lakini katika suala la elimu pia nitakuwa kwa kweli sina shukrani kama sitashukuru hii Benki ya *NMB.* Benki ya *NMB* imesaidia sana katika ujenzi wa madarasa. Kampuni ya Simu ya *Celtel* na *Vodacom* nao wanaonekana wanajitolea sana hawa watu lazima tuwapongeze kwa kazi ile ambayo wanaifanya.

Lakini narudi kwenye ukusanyaji wa mapato. Kuna matatizo ambayo yamejitokeza kule bandarini ya ukusanyaji wa kodi haya matatizo yanatokana na utendaji mbovu wa *TISCAN* iko kule. Mimi nilikuwa napendekeza kwamba kwa kweli hiyo kazi itafanyika vizuri kabisa kama itasimamiwa ama itafanywa na Mamlaka ya Kukusanya

Mapato *(TRA)*. Watakusanya vizuri kwa sababu wameshatuonyesha mwelekeo kwamba wanakusanya mapato yao vizuri sana ili ile *TISCAN* itoke kule ni chombo kinacholalamikiwa na kila mtu lakini tunakionea aibu kuwatoa pale, sijui kwa nini tunakuwa na kigugumizi hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirudi kwenye suala la mafuta, ongezeko la mafuta ya taa nilikuwa naomba Serikali ilifumbie macho, niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba tuangalie namna ya kulipunguza. Lakini nikirudi kwenye *fast track* kule ambayo kwa kweli Bajeti imeeleza na ni kwa utaratibu mzuri tu. Wafanyabiashara waliopo wanaozungumziwa wako 80, hawa 80 ambao ndio kwa kweli *TRA* wanapata kodi kutoka kwao. Nilikuwa naomba hawa watu wala hili lisiwe na mjadala, waruhusiwe ili tuweze kupata kodi vinginevyo tutashindwa kufikia kwenye malengo ambayo kwa kweli wataifikisha Awamu ya Nne kwa kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ambayo kusema kweli Mwenyekiti ambayo ni Rais sasa hivi alizungumzia mwenyewe tutashindwa kufikia hayo malengo kama hatutakusanya kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie uchimbaji wa madini. Juzi vyombo vya habari vimezungumza kwamba *container* zinajazwa mchanga, mchanga unapelekwa nje, lakini ule hauendi kama mchanga ndiyo dhahabu yenyewe inakwenda. Ninaomba tuwe na usimamizi mzuri kwa maana kwamba Wizara inayohusika basi ihusishe vyombo vya kwenda kusimamia ili tuhakikishe kwamba mali yetu haitoki nje ya nchi. Lakini pia hayo Makampuni yanayochimba madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuwa Msemaji angalau wa nafasi ya mwisho mwisho kwa jioni hii ya leo. *(Makofi)*

Kwanza kabisa napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru wananchi wote wa Mtwara kwa ushirikiano mzuri sana ambao wamenipa kwa kipindi chote hiki ambacho nimechukua nafasi ya Ubunge. Wananchi wote wakiwemo Madiwani, viongozi wa Chama na Serikali pamoja na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa. *(Makofi)*

Kabla sijaendelea basi naomba niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri, Waziri wa Mipango, Uchumi NA Uwezeshaji pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa hotuba yao nzuri na Bajeti ambayo wameiandaa kwa umakini kabisa, kwa hiyo, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Mtwara una matatizo yake sawa na mikoa mingine yakiwemo matatizo ya bei ya mazao ya korosho, bei ambayo haina msimamo mzuri, matatizo ya maji na umeme, lakini haya yote hayawezi yakatuzuia kuyakubali na kuyatambua pamoja na kuyathamini yale mazuri yote ambayo Serikali ya Chama cha Mapinduzi inatufanyia Watanzania. Kwa maana hiyo basi wananchi wa Mkoa wa Mtwara wameniomba niunge mkono hoja hii iliyoko mbele yetu kwa asillimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanzia mimi nijikite kwenye hitimisho la Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji ambapo alionyesha kwamba kuna changamoto kubwa kati ya uwiano wa ukuaji wa uchumi na maendeleo ya Mtanzania. Yapo matatizo mengi kwa Watanzania wa kawaida ni mengi na hii itatishia sana mabadiliko haya ya kodi, yatatishia sana hali hii ya Mtanzania wa kawaida kama endapo kabla tu ya Bajeti hii kulikuwepo tayari na matatizo ambayo wananchi hawa wamekuwa wakiyalalamikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nianzie kwa yale makundi ya chini hasa wanawake ambao wanajihusisha na biashara za mama lishe. Kwa kweli akinamama hawa wana maisha duni na wamekuwa wakilia, wakilalamika kutokana na ukosefu wa mitaji ya kufanyia biashara zao. Akinamama hawa mitaji yao tuseme ni *negative* kwa sababu wao kawaida huwa wanakopa kwa wafanyabiashara. Wanakopa reja reja, wanapika asubuhi katika vibanda vyao sokoni na jioni kurejesha mikopo ile. Lakini faida wanayoipata kwa kweli ni kidogo mno na faida yenyewe inapimwa kwenye chakula tu wanachokula. Wanakusanya watoto wao asubuhi na wanakwenda kula sokoni pale, ni wachache sana ambao wana mitaji ya kuanzia shilingi 15,000 na wakaweza kulimbikiza kidogo faida ambayo inaweza ikawasaidia kupata hata matibabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa maneno mengine basi akinamama hawa wanapokuwa wakifanya hizi biashara atakapougua ina maana siku hiyo familia yake haipati lishe. Wamekuwa wakijiuliza kwamba watafanya nini kutokana na hii hali ngumu ambayo wanaipata wanapokwenda Benki kufuatilia mikopo kwa sababu inahitaji siku nyingi na kupoteza muda mwingi. Kwa hiyo, akinamama hawa wanauliza Serikali itawasaidiaje ili kusudi waweze kujikwamua na kupata maisha bora?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna makundi mengine pia ya vijana ambao hawana ajira kabisa na wengi unakuta wamemaliza kidato cha nne, wengine darasa la saba na wengine kidato cha sita na hawana mahali pa kuanzia. Lakini masharti ya Benki yanawataka wawe tayari walishakuwa ni wajasiriamali tangu mwanzoni wana biashara ya aina fulani. Sasa wanachouliza ni kwamba wataanzisha vipi wakati hawana mitaji na kwa hiyo basi wanaomba Serikali iwasaidie kwa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna makundi ya waathirika wa UKIMWI ambao baadhi yao wanashindwa kupata zile dawa za *ARV* kutokana na kukosa uwezo wa kupata chakula, hawa pia wanauliza Serikali itawasaidiaje kama wananchi wa kawaida? Kuna kundi lingine la wazee ambalo wamelalamikia gharama za nauli za mabasi kutoka Dar es Salaam kwenda Mtwara. Hii imekuwa ni kero ya kuwatenganisha wao na vijana wao ambao wanaishi Dar es Salaam. Kwa kipindi cha mpaka mwezi Mei, 2007 nauli ilikuwa ni shilingi 25,000 ambayo ni kama mara mbili hivi ya nauli ya kutoka Dar es Salaam hadi Moshi. Wakati ukiangalia umbali ni karibu ule ule. Sasa wanajiuliza na wanaiuliza Serikali kwamba hii barabara kipande kile cha kilomita 60 itakamilika lini ili angalau waweze kupata ahuweni na hili nalo pia huwa linapelekea matatizo ya bei za juu madukani na kukosa mahitaji ya lazima kama sukari, sabuni pamoja na mafuta ya kupikia. Kwa hiyo, ni swali ambalo wameniagiza niiulize Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la makundi ya *SACCOS.* Makundi haya yanaonyesha kutoridhishwa na hii riba ya asilimia 10 inayokwenda *CRDB* na asilimia 2 ndiyo ibaki kwa *SACCOS.* Kwa mfano umoja *SACCOS* wenyewe ambao walipata mkopo wa shilingi 30,000,000 lakini walitumia shilingi 600,000 kuja kupata huu mkopo. Hizi shilingi 600,000 ni asilimia 2.

Kwa hiyo, wanachouliza kwamba kama Serikali kweli ina nia ya kuimarisha *SACCOS* hii asilimia 2 tayari imeshatumika kupata huu mkopo, je, wataendeshaji hizi *SACCOS* zao na watawezaje kufuatilia mkopo kama hawataweza ku-*charge*. Kwa matokeo mengine ni kwamba *Masasi SACCOS* ambayo yenyewe imeamua kuachana kabisa na huu mkopo wa wajasiriamali inaendelea na ule utaratibu wake wa zamani ambao wanatoza riba kubwa kidogo na wanadai kwamba tatizo sio riba tatizo ni ule upatikanaji wa mkopo. Kwa hiyo, hayo ni maswali ambayo *SACCOS* hizi zinaiuliza Serikali.

Kuna kundi la wanafunzi ambao wameshindwa kwenda shule kutokana na ada na mahitaji mengine ya shule pamoja na wakulima. Hawa hasa tatizo lao kubwa ni ile bei ya korosho ambapo inazidisha umaskini miongoni mwa wakulima na kuwafanya wanafunzi hawa wachelewe kuripoti shuleni wanapofaulu na wengine hawaripoti kabisa. Kwa mfano, kuna kata ya Marika ambapo kati ya wanafunzi 80 waliofaulu kwa taarifa nilizozipata mwezi Mei, 2007 ni wanafunzi 30 tu ambao waliweza kuripoti shuleni na hii inasemakana ni kutokana na matatizo ya kiuchumi.

Sasa baada ya hapo ningependa nitoe mapendekezo kuhusiana na hali hii. Kwanza kuna matatizo haya ambayo tayari yapo, matatizo ya gharama kubwa za maisha na hii ni kabla ya ongezeko la kodi ya mafuta. Nami niungane na wenzangu kuomba kwamba kodi hii iangaliwe upya, kodi ya mafuta ili kusudi wananchi hawa wasizidi kuumia kutokana na ongezeko la mfumuko wa bei ya vitu na kushindwa kuyakabili maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipendekeze pia kuhusiana na bei ya mazao ya kilimo kwa sababu katika mpango wa mwaka 2007/2008 sikuona lolote linalozungumziwa kuhusu bei ya mazao ya kilimo pamoja na kwamba kuna kuboresha kilimo cha umwagiliaji, kugawa pembejeo kwa wakulima, mbegu bora, kuimarisha huduma za ugani lakini sijaona chochote kinachozungumziwa kuhusu bei. Lakini katika kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri kuna tatizo moja ambalo nimeliona tangu mwaka 2004 mpaka 2006 bei ya korosho inashuka kutoka shilingi 1,025 mwaka 2004, shilingi 947 mwaka 2005 na shilingi 749 mwaka 2006 kwa kilo moja ya korosho katika soko la dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaonekana kwamba hata sasa hivi hatuna uhakika bei ya korosho itakuwa kiasi gani pengine itashuka zaidi, wakulima wanauliza wafanye nini? Hili linajitokeza sasa hivi wananchi wengi wameanza kuuza mashamba yao kwa sababu hawana *incentive* yoyote ya bei na hata kama wataahidiwa kuboreshewa huduma zingine kwa sababu tunapoboresha hizi huduma ina maana kwamba tunaongeza gharama za uzalishaji. Sasa gharama za uzalishaji zitakapoongezeka je, mkulima huyu yeye atauza kwa bei gani? Kwa hiyo, naomba Serikali iangalie suala hili la bei za mazao kwa sababu

ukiangalia upande wa pamba bei inapanda kidogo, korosho bei inapanda kidogo tangu mwaka 2004 mpaka 2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia suala la mikopo hii nadhani ni vizuri sehemu ya fedha zilizobaki zikapelekwa *SELF* ili kusudi wananchi wengi kufikiwa. Vile vile suala la riba liangaliwe vizuri, liangaliwe upya na pengine makundi maalumu yazingatiwe. Kwa takwimu inaonekana kwamba wanawake sio wengi ambao wanapata mikopo katika mikoa mingi takwimu ambazo tumepewa katika kipindi killichopita wanawake wameachwa nyuma na wakati wao ndio watu ambao wenye kipato cha chini. Kwa hiyo, nadhani ni vizuri tukaliangalia sana hili ili kusudi tuweze kutimiza ile kauli ya Mheshimiwa Rais aliyosema kupunguza lile pengo kati ya wasionacho na walionacho kwani ndilo lengo letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa pia kuzungumzia ku-*promote* teknolojia. Wapo Watanzania wengi sasa hivi ambao wanajitokeza kuvumbua mambo mengi, labda nitoe tu mfano kuna kijana mmoja ambaye anaitwa Zacharia Mberuzi amefanya jitihada zake mwenyewe na ni kijana ambaye alimemaliza darasa la saba na kila mwaka kwa miaka mitatu amekuwa akipata ushindi kutokana na kutengeneza *incubator* ya kutotoleshea vifaranga vya kuku. Nadhani ni vizuri Serikali ikasaidia sana kuwa-*promote* hawa wanaojitokeza kubuni teknolojia ya nyenzo za uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la China ambayo imeonekana katika hotuba ya Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji kwamba China imejitahidi sana kuongeza uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya kumsikiliza Mheshimiwa Anastazia Wambura kama msemaji wetu wa mwisho muda unaobakia nilikuwa nawasiliana na wasemaji wanaofuata kama wangeweza kutumia hizo dakika chache zilizobakia, lakini wote wameniomba sana kwa umuhimu wa Bajeti hii na maandalizi waliyoyafanya wangependa kuwa na muda kamili wa dakika zote 15 bila ya kupungua. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kutokana na hivyo basi nafikiri orodha ya wachangiaji kwa siku ya leo tutaishia nayo hapa. Nitakuwa na matangazo machache ambayo yako hapa mezani ili tuweze kufahamishana. Lakini kabla ya hayo matangazo niseme tu kwamba kesho kwa kuwa Mheshimwia Adam Malima simuoni ndani ya ukumbi huu kama kesho atakuwepo basi atakuwa ni msemaji wetu wa kwanza kwa siku ya kesho, lakini kama hatakuwepo basi Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir atakuwa msemaji wetu wa kwanza atafuatiwa na Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe na yeye pia simuoni humu ndani lakini kama kesho atakuwepo basi ajiandae kama msemaji wa pili na Mheshimiwa Benson Mpesya, Baba Askofu atakuwa msemaji wetu wa tatu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa napokea hapa malalamiko kidogo Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakilalamika kwamba *screen* zetu humu ndani haziwaonyeshi wanapokuwa wanachangia michango yao. Kwa hiyo, tumewasiliana na wahusika wao wametuambia matatizo ya humu ndani yatarekebishwa, tatizo la umeme pia limekuwa likichangia. Lakini kwa suala la kurusha matangazo yetu huko nje TVT wanasema hakuna matatizo tunaonekana na wapiga kura wetu wanatuona kama kawaida. *(Makofi)*

Mwisho tu labda nimwombe sana Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Sanya, zile pongezi alizosema atampongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha kule nje kwa utaratibu mzuri ningeomba tu nimwombe akijisikia kupongeza ampongeze humu humu ndani badala ya nje. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kutoa matangazo hayo machache basi naomba sasa niahirishe Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.35 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi, Tarehe 21 Juni, 2007 saa tatu asubuhi)*